**8 NOVEMBA, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Nane – Tarehe 8 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mrisho Gambo.

Na. 107

**Kufanya mapitio ya kikokotoo**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya malipo ya mkupuo (kikokotoo) ya asilimia 33 kwa wafanyakazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitangaza matumizi ya Kanuni mpya ya mafao ya pensheni kuanzia tarehe 1 Julai, 2022. Kanuni hiyo iliandaliwa kwa kushirikisha wadau wote (Serikali, wafanyakazi na waajiri) kwa lengo la kufanya maboresho ya pensheni ili kuwianisha mafao ya wanachama na kuifanya mifuko kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao ya pensheni ikijumuisha malipo ya mkupuo kwa wafanyakazi. Sheria inaitaka Mifuko kufanya tathimini ya kupima uhimilivu kila baada ya miaka mitatu na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ikijumuisha maboresho ya mafao ya wanachama na kuifanya Mifuko kuwa endelevu. Kwa kuwa Mifuko itafanya tathmini kwa hesabu zinazoishia mwezi Juni 2023, Serikali itazingatia ushauri wa mtaalam ambaye atafanya tathimini hiyo ili kuongeza Pensheni ya Wastaafu ambayo inajumuisha malipo ya mkupuo wa asilimia 33, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kanuni mpya ya mafao kwa wafanyakazi imekwenda kupunguza asilimia 50 ya malipo ya mkupuo ya wastaafu. Pia imepunguza miaka inayokadiriwa mtumishi kuishi baada ya kustaafu kutoka miaka kumi na tano na nusu mpaka miaka kumi na mbili na nusu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha Kanuni ya mwaka 2017 ambayo ilikuwa imeweka maslahi mapana zaidi kwa wastaafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwenye majibu ya Serikali imesema kwamba mifuko itafanya tathimini ifikapo mwezi Juni mwaka huu 2023, mpaka tunavyozungumza tayari imeshapita miezi mitano.

Je, tunaweza tukapata majibu ya tathimini hiyo ya Serikali kupitia Bunge lako tukufu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Gambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni katika mifuko hii. Wote tunatambua tulikuwa na mifuko mingi hapo awali, mifuko ya *PPF, LAPF, PSSSF* na mifuko mingine mingi tu. Uendeshaji wake ulikuwa wa gharama kubwa sana kwa sababu ya menejimenti lakini ilitengenezwa katika misingi ya kuwa na ushindani. Ikawa ni wazo na mfumo wa Serikali wa kuweza kuboresha zaidi na kuangalia maslahi kwa sababu ya uhalisia na sera za wakati huo na mabadiliko ya hali ya kiuchumi ikaona ifanye *actuarial evaluation* ambayo ilileta majibu kwa wakati huo kwamba ilifaa kuweza kuangalia walio wengi zaidi na kuweza kuwapa manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, asilimia 81 ya hali ya kikokotoo cha sasa inawapa manufaa ya kuwa na mkupuo mkubwa. Asilimia 19 wanabaki kuwa na mkupuo ambao ni wa wastani lakini mapato ya kila mwezi yameongezeka. Kwa hiyo, tathimini baada ya miaka mitatu ambayo tumeifikia sasa na nikijibu hoja yake ya swali la pili kwamba tunaendelea na tathimini na sasa tumpe majibu ya tathimin.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ni tafiti sasa huwezi ukataka kwa wakati wowote kuweza kupata majibu yake ni mpaka pale ambapo itakamilika. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge

kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ina nia njema sana kukitoa kikokotoo hiki asilimia 25 mpaka 33. Si ajabu tathimin hii itakapotoa majibu tukiangalia ustahimilivu wa mfuko na maslahi ya wafanyakazi wetu ambao ni vipenzi vya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan tutaenda kutoa faida kubwa kwa upande wao na kuweza kuwasaidia Watanzania ambao wametumikia Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Umejibu vizuri ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

Na. 108

**Kukarabati Hospitali ya Wilaya ya Manyoni**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Wilaya ya Manyoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa shilingi millioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi mbili za wanawake na wanaume pamoja na jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni. Aidha, majengo haya yamekamilika na yataanza kutoa huduma mwishoni mwa Novemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepeleka shilingi billioni 1.4 Oktoba, 2023 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri inaendelea na taratibu za kupata mzabuni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji wa dharura, jengo la X-ray, stoo ya kuhifadhia dawa, jengo la kliniki ya Mama na Mtoto, jengo la kufulia, njia za kutembelea wagonjwa pamoja na kufanya ukarabati wa majengo mengine ya Hospitali ya Wilaya ya Manyoni, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusikia kilio chetu na kuikarabati Hospitali ya Wilaya ya Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa sasa ni ukosefu wa vifaa tiba.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka vifaa tiba vya kutosha hususan katika Jengo la Mama na Mtoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa hospitali hii inakabiliwa na uhaba wa watumishi, ningependa kujua, ni upi mkakati wa Serikali wa kuwapatia watumishi 169 ili kuendana na mahitaji yaliyopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aysharose Mattembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kujali afya za Watanzania na kupeleka fedha nyingi katika halmashauri zetu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya huduma za afya. Sambamba na hilo, vifaa tiba vimeendelea kupelekwa katika vituo vilivyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Halmashauri ya Manyoni na hospitali hii imeshapokea zaidi ya shilingi milioni 750 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Bado Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na vifaa tiba vya kutosha zaidi katika Jengo la Mama na Mtoto na katika majengo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na upungufu wa watumishi, Serikali imeendelea kuajiri watumishi kwa awamu na kuwapangia katika halmashauri kote nchini ikiwemo Halmashauri hii ya Manyoni. Nimhakikishia kwamba tunatambua kuna upungufu wa watumishi hawa na Serikali itaendelea kuajiri kwa awamu kuhakikisha kwamba watumishi wanapelekwa katika hospitali hii, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kabula.

Na. 109

**Hitaji la Chumba Maalum cha Mama na Watoto Njiti - Ukerewe**

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga chumba maalum yaani *Incubator* kwa ajili ya Mama na Watoto njiti katika Hospitali ya Wilaya Ukerewe?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe inatoa huduma kwa watoto wachanga na wale waliozaliwa kabla ya muda yaani Njiti. Hata hivyo, nafasi inayotumika kutolea huduma hiyo ni ndogo kwa mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya inaendelea na uhakiki yaani *assessment* kwenye Hospitali zote za Halmashauri nchini ili kuweza kubaini mahitaji ya vyumba vya kuhudumia watoto njiti na kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa majengo hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabula swali la nyongeza kama lipo.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sina swali la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. Profesa umetaka swali la afya?

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Nicholaus Ngassa.

Na. 110

**Kupandisha hadhi Shule ya Sekondari Igurubi**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Igurubi iliyopo katika Wilaya ya Igunga kuwa ya kidato cha tano na cha sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Jimbo la Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shule zilizopendekezwa katika Tarafa ya Igurubi kuwa shule za *A level* ni Igurubi Sekondari na Mwamakona Sekondari. Suala lililokwamisha shule ya Igurubi kutosajiliwa ni kutokuwa na miundombinu Kama bweni, bwalo na miundombinu mingine wezeshi. Hivyo shule ikikidhi vigezo kwa mujibu wa miongozo na taratibu, itasajiliwa kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru na kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu. Wiki iliyopita walitupatia shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, Shule ya Sekondari ya Igurubi ilianzishwa mwaka 2000 na sasa ina miaka zaidi ya 20. Ina madarasa 19 lakini yanayotumika ni tisa tu, madarasa kumi yamebaki, ambayo inaongeza idadi ya miundombinu ya majengo ambayo tunaweza tukaibadilisha ikawa mabweni na mabwalo. Je, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha tunapata kidato cha tano na sita kwenye Shule ya Sekondari ya Igurubi? Aahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa, kwanza naanza kwa kumpongeza yeye Mheshimiwa Ngassa kwa kuweza kufuatilia sana suala hili ya Shule ya Igurubi. Amekuja ofisini mara kadhaa kwa ajili ya kufuatilia iweze kupandishwa hadhi na kuwa shule ya *A level.*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hii kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, tayari Serikali imeshapeleka fedha nyingi kwa ajili ya miundombinu mingine ya madarasa. Tutaendelea kutafuta fedha kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa ajili ya kujenga miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kusajiliwa. Baada ya miundombinu hiyo kuweza kujengwa tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kuweza kuipandisha hadhi shule hii na kuwa ya kidato cha tano na sita. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Shule ya Sekondari ya Kilolo ambayo iko Makao Makuu ya Wilaya haina Kidato cha Tano na Sita. Kuna wadau wameshajitolea kujenga madarasa. Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa ajili ya mabweni ili kuanzisha Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu swali la Mheshimiwa Justin Nyamoga Mbunge wa Kilolo. Serikali iko tayari kuweza kutafuta fedha kadri ya upatikanaji wake kwa ajili ya kujenga miundombinu katika Shule ya Sekondari Kilolo. Baada ya ujenzi wa miundombinu hiyo kuanza kufuata taratibu za kusajili shule hiyo kuwa na Kidato cha Tano na Sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali iliahidi kupandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Lemira kuwa ya Kidato cha Tano na Sita na ikatupa utaratibu wa kufuata. Tumefanya hivyo, tumeandika barua na tumefuata utaratibu wote. Je, lini sasa Serikali itapandisha shule hii ya Lemira iwe ya Kidato cha Tano na cha Sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe. Serikali itapandisha hadhi shule hii pale taratibu zitakapokuwa zimefika Wizara ya Elimu. Tutafuatilia kwa kushirikiana na Afisa Elimu wa Wilaya na Mkoa kuona kama barua zile zililetwa Ofisi ya Rais TAMISEMI na kisha kupelekwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kupandisha shule hii hadhi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

Na. 111

**Ujenzi wa barabara ya Msambiazi – Lewa – Lutindi hadi Kwa Blue**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Msambiazi – Lewa – Lusindi hadi kwa Blue kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya kiasi cha shilingi milioni 470 zilitumika kujenga barabara kwa kiwango cha zege mita 824, mifereji urefu wa mita 600, kuchonga na kushindilia barabara urefu wa kilometa 16.5, kujenga madaraja madogo yaani *box culverts* matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 Serikali imetenga jumla ya Shilingi millioni 400 kwa ajili ya kujenga mifereji na barabara kwa kiwango cha zege urefu wa mita 700 na kujenga madaraja madogo yaani *box culverts* matatu ambapo ujenzi umefikia asilimia 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha barabara hii kwa kuijenga kwa kiwango cha zege katika maeneo yote yenye changamoto hasa kwenye miinuko na utelezi kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naishukuru Serikali kwa kazi ambayo imefanyika kwenye barabara hii.

Nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza; barabara hii ni muhimu sana, barabara hii pamoja na barabara za Kwetonge – Donge - Kizara, barabara ya Mombo - Mzeri, barabara ya Makuni - Zege Mpakani zimeunganisha Wilaya ya Korogwe na Wilaya ya jirani.

Ni lini Serikali itatimiza ile ahadi yake ya kuzipandisha hadhi barabara hizi kuwa kwenye hadhi ya barabara za mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara nyingi zinazosimamiwa na *TARURA* ni za changarawe na udongo na zinahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Serikali haioni sasa ni wakati sahihi kununua vifaa kwa *TARURA* kila mkoa ili matengenezo madogo madogo ya barabara yafanywe na *TARURA* wenyewe kwa kutumia wataalam wao wa ndani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya Mheshimiwa Timotheo Mnzava; la kwanza hili la barabara hii kupandishwa hadhi, barabara ambazo ametaja Mheshimiwa Mnzava taratibu ziko wazi kwa mujibu wa sheria. Vikao vile vya kisheria lazima vikae, wanaanza kwanza wao kwenye *DCC* vinatoka vinakwenda kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa na kisha wanamuandikia Waziri mwenye dhamana ya barabara hizi za mikoa yaani *TANROADS* kuomba kupandisha hadhi. Tutafuatilia kuona maombi hayo yamefikia wapi kwa ajili ya kuweza kupandisha hadhi barabara hii kwa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la mitambo, *TARURA* kuweza kununua mitambo. Tayari mkakati wa Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kutoa fedha kwa wenzetu wa taasisi ya *TARURA* kuweza kununua mitambo hasa katika maeneo ambapo upatikanaji wa mitambo ni mgumu. Tayari mpango huu umeanza kufanya kazi kule visiwani Mafia. Maeneo mengine ni pembezoni mwa nchi yetu ambapo tayari wameanza na kadri ya upatikanaji wa fedha tutazidi kufanya hivyo ili mitambo ile iweze kutumika wakati wa dharura.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Holili - Tarakea kwa kuwa

kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika barabara ya Rombo ambayo inabeba malori mengi, inachukua malori yanayopeleka mchanga katika nchi ya Kenya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hilo swali ni la kwako au la Wizara ya Ujenzi? Mheshimiwa Waziri kama una majibu jibu, kama huna liletwe kama swali la msingi kwa Wizara husika.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Bushiri, Barabara hii ya Holili – Tarakea, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kuona ni namna gani ambavyo bajeti imetengwa kwa ajili ya kupanua barabara hii ili iweze kupitika wakati wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Barabara ya Bukama – Salamakati – Mkomalilo, taarifa zote za kuipandisha kutoka kwenye Halmashauri, kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* zimeshafanyika. Je, ni lini sasa itakwenda *TANROADS*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere la Barabara hii ya Nkama – Nkomalilo kupandishwa hadhi. Taratibu za kisheria zipo wazi, wao wamekamilisha taratibu zile kwenye ngazi yao ya Halmashauri na sasa lipo katika Wizara ya Ujenzi kwa Waziri mwenye dhamana wa kuweza kupandisha hadhi hii. Tutalifuatilia kwa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi na kuona limefikia wapi na ikiwezekana timu iweze kwenda kuweza kukamilisha taratibu hizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, juzi Mheshimiwa Profesa Kitila alikuwa anatuambia hapa *a good government is good*

*people*. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, umejibu maswali ambayo wala siyo ya wizara yako.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Anne Kilango.

Na. 112

**Motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa motisha za kifedha na zisizo za kifedha kwa watumishi wa Umma wakiwemo watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu kwa kuboresha viwango vya posho za kazi baada ya masaa ya kazi, posho ya kujikimu wakati wa kusafiri, posho za mawasiliano, kufikisha huduma za umeme katika maeneo yao, kutoa magodoro na nyumba za walimu zenye staha na mengineyo mengi

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Halmashauri yalipo maeneo yenye mazingira magumu kwa kutambua umuhimu wa kutoa motisha, zinatekeleza mipango yao ya motisha kwa kufuata

miongozo inayotoka kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kusimamia utoaji wa motisha mbalimbali kwa watumishi hao kutegemeana na hali na mazingira magumu ya sehemu wanapofanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu ya Serikali, naomba kuuliza swali la nyongeza moja tu. Kwa kuwa Jimbo langu la Same Mashariki, theluthi mbili au zaidi ya theluthi mbili wananchi wangu wanaishi kwenye milima mirefu na huko wanakoishi kuna mashamba makubwa ya tangawizi. Naomba nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri, haya sliyoyazungumza kwangu hayajafanyika. Je, Serikali inaona umuhimu sasa wa kwenda kuangalia vizuri Jimbo la Same Mashariki muone watumishi wanavyoishi kwa shida hasa Walimu na Waganga na wakatoe motisha ili wale watumishi waweze kufanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko naye bega kwa bega kuhakikisha kwamba mazingira ya watumishi wake yanakwenda kurekebishwa na kuwekwa sawa. Pia nataka kulikumbusha Bunge lako kwamba mwaka 2020/2021, Serikali iliteua timu ya wataalam ambao walikwenda katika Mikoa 27, Halmashauri 117, Manispaa tano, Miji minne, Majiji manne, Tarafa, Kata na Vijiji mbalimbali kuangalia na kujiridhisha juu ya mazingira magumu wanayoishi watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba mazingira hayo wanayoishi wafanyakazi wetu au watumishi wetu, yalionekana na kwamba Serikali inajipanga. Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba

kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafika katika Halmashauri ya Mheshimiwa Mbunge na kuona hali hiyo na kurekebisha ili watumishi wetu waweze kutoa huduma zilizo nzuri kwa wananchi wetu. *(Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kuongeza majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa sababu namwamini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili alilouliza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ni suala la msingi sana. Nimetamani kuongeza maneno machache tu kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu yenyewe tu yanajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la motisha ni sehemu ya haki za watumishi wetu. Ni haki, ipo kwa mujibu wa sheria. La pili, wajibu huo wa kutoa motisha ni wa mwajiri, kwa maana ya zile Halmashauri zetu zinaweza kutengeneza utaratibu wa kutoa motisha kwa watumishi wake kulingana na mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama waangalia sekta nzima, maelekezo yetu ni kwamba Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ndiyo zinazowajua watumishi wao. Namna wanavyokuja mathalani, unaweza ukaweka utaratibu watumishi wako wa kuwanunulia magodoro na vitu kadhaa kadhaa vya kuanzia maisha, unaweza ukatoa mikopo yenye …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu mazuri, hongera sana kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Na. 113

**Manufaa yatokanayo na kero za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, kero 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi zimeleta manufaa kiasi gani katika utekelezaji kwa pande zote mbili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyotokana na ufumbuzi wa changamoto 11 za Muungano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa hasa katika maeneo ya ajira kwa Watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi katika Taasisi za Muungano, wameendelea kunufaika na ajira hizo ikiwa ni 79% kwa Tanzania Bara na 21% kwa Zanzibar. Mgawanyo wa Fedha za Mapato yatokanayo na Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti *(GBS)* imeendelea kuongezeka tangu kupatiwa ufumbuzi kwa changamoto hii na kuendelea kuimarisha Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kodi ya Mapato yatokanayo na mishahara ya watumishi wa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.75 kimekuwa kikitolewa kwenda SMZ kila mwezi kuanzia mwaka 2012/2013 kama malipo ya *PAYE*; na Kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara na zenye matawi Zanzibar zimeanza kulipa Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)* kwa upande wa Zanzibar. Aidha, mapato yanayotokana na Tozo za *VISA* kutumika

pale yalipokusanywa kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, suala hili limepatiwa ufumbuzi na sasa wafanyabiashara kulipa kodi inayostahiki kwa tathmini ya bidhaa inayotumika Tanzania Bara. Kwa muktadha huo, suala la ulipaji wa tofauti ya kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara imewekwa vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; pamoja na kutatua kero hizi, kero hizi ni kero ambazo zimeonekana kwa utendaji wa Serikali. Je, Serikali sasa iko tayari kushirikisha Tume, Kamati za maridhiano zilizoundwa na Marais wetu wawili hawa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ile iliyoundwa na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; baada ya kutatua kero hizi, je, Serikali itakuwa tayari kutengeneza Mkataba Mpya wa Muungano ambao utashirikisha wadau?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Said Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuasisiwa kwa Muungano huu, baada ya kuona kwamba tumeungana, Serikali zote mbili ziliona

kuna haja ya kuunda Kamati ambayo itakuwa inashughulika na kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hizi zipo katika ngazi ya Makatibu Wakuu, Wataalam, ipo katika ngazi ya Mawaziri lakini Kamati hii ipo katika ngazi Kuu ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati hii iko *strong* na inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi tumetoka kutoka changamoto zilizokuwepo mpaka leo zimebakia nne, maana yake Kamati imefanya kazi kubwa. Wazo alilolitoa Mheshimiwa Mbunge ni zuri, tunalichukua, tunakwenda kulifanyia kazi kwa sababu Kamati ya Maridhiano kazi yake ni kutuliza amani, kusaidia katika kuleta maelewano na ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, kuhusiana na kuiweka kwenye Mkataba Maalum. Tarehe 6 Desemba, 2022 tulikuwa na kikao cha Kamati yetu ya Maelewano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, hii ya Muungano. Hii hoja iliibuka ya kuiweka kwenye *document* maalum ya kisheria, tukawapa kazi wataalam wetu, tukawapa kazi Wanasheria wetu waende wakaone namna ya kufanya ili kikao chetu kijacho cha Kamati, watuletee majibu ya kuona namna ambavyo tunaweza tukaingiza kwenye Mkataba ama *document* maalum ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Najma, jiandae Mheshimwa Asya Mwadini.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali langu la nyongeza ni, je, Serikali ina mikakati ipi ya kuweza kudhibiti madhara ambayo yanaweza kutokea kwa changamoto ambazo hazijafanyiwa kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Najma Giga wa Murtaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo tunakwenda kulifanya kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tunazo Kamati zetu za Maelewano ambazo huwa tunakaa kwa ajili ya kutatua changamoto hizi na vikao bado vinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Kamati hii iko makini na inafanya kazi kwa uangalifu kwa mujibu wa taratibu zote. Tutahakikisha kwamba changamoto zote zinatatuka kama ambavyo tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asya Mwadini, jiandae Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; je, Serikali haioni haja ya kuleta taarifa ya mchakato mzima wa utatuzi wa kero za Muungano katika vyombo vya kutunga sheria, Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Zanzibar na Bunge kwa Jamhuri, ili tuweze kupata picha halisi ya mchakato mzima wa utatuzi wa kero za Muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri sana kuhusu masuala ya Muungano. Naomba kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Asya kwa swali lake zuri. Katika hili, kupitia Kamati ya Utawala na Sheria ambayo ndiyo ina jukumu la

kusimamia Wizara yetu ambayo tunaiongoza, mara nyingi inakuwa ikipata taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni katika vikao vya Kamati, miongoni mwa jambo kubwa ambalo limeletwa katika Kamati ni suala zima la Hoja zote za Muungano zilizofanyiwa kazi na zile ambazo zimebaki. Naomba nimtaarifu Mheshimwa Mbunge kwamba Wizara yetu inaendelea kufanya hivyo na wakati wa vikao mbalimbali tutaendelea kuleta taarifa hizi katika Bunge letu hili hususani katika kipindi cha bajeti. Mheshimiwa Mbunge asiwe na mashaka katika eneo hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali. Kwa kuwa msingi wa kutozwa mara mbili ushuru kwa bidhaa iliyokuwa inatoka Zanzibar inatokana na tofauti ya kodi au ushuru uliokuwa unatozwa kwa upande wa Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara. Hivyo tofauti ndiyo iliyokuwa inatozwa kama ushuru mara mbili. Kwa kuwa Waziri amesema kwamba wamemaliza na sasa Wazanzibar hawatatozwa ushuru mara mbili, wamesema wameweka mambo vizuri. Je, Waziri anataka kutuambia kwamba sasa ushuru unaotozwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa bidhaa inayoingia na inayoingia Zanzibar sasa ni sawa au kuna utaratibu gani ambao wameweka, kuzuri huko ni kwa namna gani, tueleze?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa. Utaratibu ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameusema, ni ule ambao unahusisha tofauti. Unahusisha ile *difference* ambayo inatokana na viwango vya *VAT* vinavyotozwa Tanzania Bara na vile vinavyotozwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama bidhaa itakuwa imelipiwa kodi Tanzania Bara na ikawa imelipiwa *VAT* ambayo ni kubwa kuliko ile inayotozwa Zanzibar, kama bidhaa hiyo ni ya Zanzibar, maana yake mfanyabiashara huyo ana-*refund*. Kama mfanyabiashara amelipa kodi Zanzibar na bidhaa hiyo inatumika Tanzania Bara, maana yake itakapotumika Tanzania Bara, atalipa tofauti ile ili kuweka bidhaa ile iwe sawa, inapotumika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa zinapotumika, kodi yake yote iko sawa. Ikitumika kule ambako ilitozwa kidogo, maana yake ikitumika *Mainland* inatakiwa kulipia ile tofauti ili iwe sawa na iliyoko huku. Ikitumika Zanzibar, maana yake pana-*refund* ili iwe sawa na kodi inayotozwa kwa kule Zanzibar. Kwa maana hiyo, haya tumeshayafanya kwenye vikao na elimu kwa wafanyabiashara inaendelea ili jambo hili lisilete tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoza ama imepata msamaha Zanzibar, ikiingia bila kulipiwa tofauti huku, maana yake patakuwepo na bidhaa ambayo imeingia ndani ya nchi bila kuwa na kodi stahiki. Tumeshayawianisha yote yale na tumefanya haya kwenye vikao na tunaendelea kuwapa elimu wafanyabiashara. Kimsingi ile haikuwa kutozwa mara mbili kwa sababu ni tofauti. Kutoza mara mbili maana yake ni kutoza kule na utoze na huku. Ile ilishasuluhishwa haipo tena. Kwa maana hiyo sasa hivi tumewianisha ili mtu alipe kodi ambayo inastahili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Massare.

Na. 114

**Kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mbuga inayozunguka Mji wa Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

Je, lini Tume ya Umwagiliaji itatimiza ahadi yake ya kuvuna maji ya mvua katika Mbuga inayozunguka Mji wa Itigi ili kuepusha mafuriko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, ngoja kidogo. Waheshimiwa kuna vi-*note* vingi vinakuja hapa tano moja, tano moja, vikiendelea nitasitisha Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya imetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuweza kuchimba na kujenga mifereji ya kuongoza maji kutoka bonde linalozunguka Mji wa Itigi na kuelekeza maji hayo mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utekelezaji wa ujenzi wa mifereji hiyo utasaidia kuepusha mafuriko yanayojitokeza katika Mji wa Itigi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali hili niliuliza Bunge la Kumi na Moja na majibu ya Mheshimiwa Omary Mgumba yalikuwa hivi hivi kwamba wataenda, akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Sasa leo na mwaka huu kuna *El-nino*, wanatuambiaje watu wa Itigi kwamba tufe kwa sababu Serikali haitimizi ahadi? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Halmashauri ya Itigi ina *scheme* moja tu ya umwagiliaji na ambayo haifanyi kazi vizuri. Je,

Serikali inaweza kuniahidi mbele ya Bunge lako Tukufu, kwamba wataenda kutekeleza angalau mradi mmoja wa *scheme* ya umwagiliaji kwa ajili ya wananchi wa Itigi wakati Wizara hiyo imepata fedha nyingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Massare, Mbunge wa Manyoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina nia ya kuona wananchi wa Itigi wanakufa kwa sababu ya mafuriko. Jukumu letu sisi kama Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha kwamba tunawajengea miundombinu itakayowasaidia wao kwenye kulima, lakini vilevile itaongeza pato ya Halmashauri ya Mji wa Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichoahidiwa katika Bunge la Kumi na Moja na ambacho hakikutekelezwa, ilikuwa ni kwa sababu ya changamoto za kifedha. Sasa hivi fedha tunayo, ndiyo maana mwaka huu tumetenga fedha na tunakwenda kulifanyia kazi. Kwa hiyo, nimwondoe shaka Mbunge kwamba, jambo hilo litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Mradi Halmashauri ya Itigi iko sehemu ya mipango yetu, kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kulingana na mvua zinazoendelea kunyesha Wilayani Lushoto na kusababisha uharibifu hasa wa miundombinu ya barabara. Je, Tume ya Umwagiliaji haioni kwamba kuna haja ya kujenga mabwawa katika Kata za Kwai, Makanya pamoja na Ubiri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimjibu Mheshimiwa Shekilindi kwamba mipango yetu sisi kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ni kuhakikisha tunayafikia maeneo yote yanayofaa kwa kilimo na tutahakikisha tuna-*tap* maeneo yote ambayo tunaweza tukapata maji ya kutosha ambayo yatasaidia kufanyika kwa kilimo katika msimu wote wa mwaka. Kwa hiyo, hata maeneo ambayo ameyataja tutayapitia tuone tutakapofanya tathmini ili kama yanafaa basi maeneo yote hayo tutayaingiza katika mpango wetu ili yaweze kutumika kwa kilimo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Daktari Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Shinyanga hasa vijijini kuna mbuga kubwa na mabonde. Je, ni lini Serikali itajenga mabwawa katika mbuga hizo hasa Mwakitolyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama nilivyojibu katika swali la awali ni kwamba, mpango wa Serikali ni kujenga mabwawa katika maeneo yote ambayo yanafaa kwa kilimo na katika mwaka wa fedha huu, katika bajeti yetu tunatarajia kujenga mabwawa 100 nchini, ambayo yatasaidia wakulima pamoja na Halmashauri katika kufanikisha shughuli hii ya kilimo. Kwa hiyo, nimwondoe shaka tu tutafikia maeneo mengi kadri iwezekanavyo na katika mwaka wa fedha ujao, vilevile tutapanga maeneo mengine, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Salim Mussa Omar, kwa niaba Mheshimiwa Sanga.

Na. 115

**Baadhi ya Mechi za Ligi Kuu Tanzania kuchezwa Zanzibar**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, kwa nini baadhi ya mechi za Ligi Kuu ya Tanzania zisichezwe kwenye viwanja vya Gombani na Amani vilivyopo Pemba na Unguja?

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Omar Salim, Mbunge wa Gando lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Festo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kupongeza mahusiano mema yaliyopo baina ya Wizara zinazohusika na Michezo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, suala la viwanja vya Gombani - Pemba na Amani Unguja, kutumika kwa michezo ya Ligi Kuu ya *NBC* ni wazo jema sana katika kudumisha ushirikiano na Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba Ligi Kuu ya *NBC* inaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* na utekelezaji wake unasimamiwa na Bodi ya Ligi Tanzania ambapo, kabla ya Ligi kuanza timu zina uhuru wa kuchagua uwanja wake wa nyumbani ambao utatumika kwa michezo yake yote ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo timu yeyote itawiwa kuchagua Uwanja wa Amani au Gombani kuwa uwanja wake wa nyumbani hakutakuwa na kikwazo chochote ikiwa watakidhi makubaliano na uongozi unaosimamia taratibu na matumizi ya

uwanja husika bila kuathiri Kanuni na Miongozo ya Kamati za Ligi za *TFF* na *ZFF*.

Aidha, kanuni ya 9(7) ya Bodi ya Ligi inaruhusu timu ya Ligi Kuu kuteua viwanja vingine miongoni mwa viwanja visivyokuwa na michezo ya Ligi Kuu katika michezo yake miwili ya nyumbani na kuwasilisha uteuzi wake siku ishirini na moja kabla ya mchezo husika inayokusudiwa kuchezwa kwenye uwanja ulioteuliwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanaonesha mshikamano wa pande zote mbili. Swali langu la kwanza dogo la nyonyeza:

Kwa kuwa, umeona kwamba haya yanaleta muungano mzuri ni lini Serikali itarejesha ligi ya muungano ili kuendelea kudumisha Muungano wetu?

Swali la pili; kwa kuwa kumekuwa na viashiria vya rushwa michezoni, ikiwemo kwenye mchezo uliopita ambapo jana Bodi ya Simba imesimamisha baadhi ya wachezaji.

*(Hapa baadhi ya Wabunge wazilizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni haki ya mwenye swali kuuliza swali, kupiga kelele kwenye Bunge bila utaratibu ni kosa la kinidhamu. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na viashiria vya rushwa michezoni, na jana tumeona Bodi ya Simba imesimamisha baadhi ya wachezaji wakihusishwa na vitendo hivyo. Ni upi mkakati wa Serikali kupambana na vitendo vya rushwa michezoni ili ligi yetu iwe *smart?* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye Wizara ya Michezo tunafahamu umuhimu wa kuwa na ligi ya Muungano na tuna hamu ya kuona ikirejea. Kwa kuthibitisha hilo Wizara zenye dhamana ya michezo za Tanzania Bara na Zanzibar kwa miongozo ambayo zimeitoa *TFF* na *ZFF* wameshaanza vikao vya kuona namna bora ya kurejesha ligi ya Muungano. Kama ambavyo nimesema, tuna hamu ya kuona ikirejea na tunatafuta namna bora tu ya kufanya isiingilie ratiba za timu ambazo zinazipitia sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mwanzoni mwa msimu huu *TFF* kwa kushirikiana na TAKUKURU ilianzisha mradi ambao unaitwa Kataa Upangaji wa Matokeo Linda Hadhi ya Mpira wa Miguu. Nafahamu hili siyo suala ambalo linaweza kutatuliwa siku moja, malalamiko ni mengi lakini tunafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kupunguza au kuondoa kabisa viashiria na vitendo vya rushwa kwenye mchezo wa mpira wa miguu. Kwa kudhibitisha hilo TAKUKURU wameshaanza kukaa na wadau mbalimbali, kuhakikisha wanatoa elimu na kuwaelimisha kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa kumaliza vitendo vya rushwa katika michezo na kupanga matokeo vikibainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU imeshakaa na Chama cha Wachezaji wa zamani, imeshakaa na Chama cha Waamuzi, vilabu vya ligi kuu, taasisi za fedha, kampuni za michezo ya kubashiri na wadau wengine mbalimbali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na sisi jambo hili hatutaki kuliona likiendelea chini ya usimamizi wetu na tunafanya kila lililopo ndani ya uwezo wetu, ikiwemo kushirikiana na taasisi nyingine za kupinga mambo yasiyofaa kwenye michezo kama TAKUKURU ili kuhakikisha linakomeshwa kabisa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nakushukuru sana ameelezea vizuri sana juu ya *coordination* kati ya TAKUKURU na vyombo vingine katika kusimamia sekta mbalimbali, ikiwemo hii ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa michezoni haikubaliki, kama mchezo wa juzi wa Yanga na Simba una viashiria vyovyote vya rushwa, niwaombe sana Timu ya Simba waende wakaripoti Ofisi ya TAKUKURU - Temeke, kama zile tano zimetokana na rushwa ili TAKUKURU waweze kuchukua hatua. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kaa chini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninataka kujua ni lini Serikali itaweka mkakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, Mikoa yote inakuwa na viwanja vya mpira ambavyo ni rafiki kuweza kucheza kwenye Ligi Kuu ili kuweza kutoa motisha na hiyo Mikoa iweze kushiriki kwenye Ligi Kuu, tofauti na sasa ambapo unakuta Dar es Salaam ni *dominant* kwenye Ligi Kuu, inakuwa na timu nne au saa nyingine ni timu tano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango siyo kwamba haipo, mipango imeshaanza na itakuwa ikitekelezwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa sasa mpango wetu ni kurekebisha viwanja Saba vya Mikoa Saba tofauti ambavyo vinaweza kuwa na viwango vya kuchezea Ligi Kuu. Uwanja wa Uhuru, Uwanja wa Jamhuri, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, pia Uwanja wa Mkwakwani na viwanja vingine vitatu siwezi kukumbuka kwa haraka lakini tunavyo viwanja Saba ambavyo vinaenda kufanyiwa marekebisho katika kipindi hiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, ulileta ki-*note* hapa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza vipaji vya vijana wanaocheza timu za daraja la nne ili waweze kupanda kwenye daraja zingine kwa mchujo ambao hautakuwa na uonevu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia *TFF* inaendeleza programu mbalimbali za soka kwa vijana chini ya miaka 15 na 17. Sasa hili la vijana ambao wanacheza ligi za chini kama Ligi Daraja la Nne kupata nafasi ya kucheza ligi kubwa zaidi, hili ni suala la binafsi la timu na kama zitaona wana uwezo wa kutosha wa kupandishwa zitaendelea kufanya hivyo kama ambavyo zinafanya sasa hivi. Najua mchezo wa mpira wa miguu unahitaji muda na uwekezaji mkubwa ikiwemo *scouting* na timu hizi zinafanya kila linaloweza ili kupata wachezaji wazawa wa ndani, kwa ajili ya kuchezea *club* zetu na hatimaye Timu za Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Yeyote sasa atakayesimama humu kuonesha alama ya mitano tena atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir. *(Kicheko)*

Na. 116

**Mchango wa Diplomasia ya Uchumi katika sekta ya uzalishaji**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza: -

Je, Diplomasia ya Uchumi ina mchango gani katika kuleta mapinduzi kwenye sekta ya Sayansi, Teknolojia na Uzalishaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile leo ni mara yangu ya kwanza nasimama hapa kujibu swali, baada ya kupata nafasi ya kuaminiwa katika Baraza la Mawaziri na kuhamishwa kutoka Wizara ya Nishati, kupelekwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kumsaidia kazi katika Wizara ya Mambo ya Nje, kwa nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inayoshughulikia mambo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuahidi Mheshimiwa Rais utendaji uliotukuka lakini nawaahidi Waheshimiwa Wabunge wenzangu ushirikiano zaidi ya ule niliokuwa nao, lakini ninawaahidi Watanzania wote kwa ujumla utendaji na uwakilishi wema katika majukumu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia ya uchumi ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ambayo inajumuisha mipango na mikakati yote ya kulinufaisha Taifa letu kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia ushirikiano baina yetu na mataifa mengine, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Mikakati hiyo ni pamoja na utafutaji wa masoko nje ya nchi, kuvutia uwekezaji, biashara na watalii, kutafuta fedha zenye masharti nafuu, ufadhili wa masomo nje ya nchi na uhaulishaji wa teknolojia za kisasa ambazo hutumika kwenye sekta za uzalishaji zikiwemo viwanda, kilimo na nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, nchi yetu inapata mapinduzi makubwa kwenye sekta ya sayansi na teknolojia na kuchangia maendeleo ya Taifa letu. Kwa mfano, Serikali ya Marekani kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania inaendelea na taratibu za kukamilisha ujenzi wa kiwanda kikubwa nchini cha kuchakata madini ya kutengeneza betri za magari ya umeme kinachotarajiwa kukamilika mwaka 2026. Kiwanda hiki kitaleta teknolojia mpya ya utengenezaji wa vifaa vya magari ya umeme, kuhaulisha teknolojia nchini na kuibua vipaji vipya kwa vijana watakaopata ajira katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya uzalishaji diplomasia ya uchumi inasaidia upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi. Kwa mfano, hadi kufikia mwezi Septemba, 2023 Tanzania imeuza tani 13,708 za nyama ikilinganishwa na tani 1,777 zilizouzwa mwaka 2020/2021. Masoko hayo yamepatikana kutika nchi za China, Kuwait, Oman, Qatar, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Naomba utulivu ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, masoko haya yamechochea sekta ya uzalishaji kwa ujumla wake, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uvuvi wa Bahari Kuu ni eneo ambalo bado halijafikiwa vizuri na kwa kuwa, Zanzibar imejikita zaidi katika uchumi wa bluu.

Je, ni upi mpango wa Serikali kupitia diplomasia ya uchumi katika kulifikia vizuri eneo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa bluu ni shughuli za kiuchumi zinazohusisha endelezaji na utumiaji wa rasilimali ya bahari ambayo Tanzania kwa maana ya Tanzania Bara na Zanzibar tunayo. Kwenye eneo hilo Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la *IFAD* - Mfuko wa Kimataifa wa Uwezeshaji kwenye maeneo ya Kilimo, tumepata pesa takribani dola milioni kama 20 kwa ajili ya kununua meli nne, ambazo zitaenda mbili Zanzibar na mbili Tanzania Bara kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa bluu na meli hizi zitasaidia kwa *TAFICO* na *ZAFIKO* lakini zitafanya katika eneo la kilimo kwenye utafiti baharini kwenye eneo la elimu, kwenye teknolojia na maeneo mengine. Kwa hiyo diplomasia hii ya uchumi itaendelea kukua kwenye eneo la uchumi wa buluu kwa kuendelea kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga.

Na. 117

**_GPSA_ kuchelewesha ununuzi wa magari Serikalini**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya *GPSA* kuchelewesha ununuzi wa magari ya Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa ununuzi wa magari Serikalini umekuwa ukisababishwa na mambo yafuatayo: -

(i) Mabadiliko ya aina za magari yanayotumiwa na Serikali ambapo upatikanaji wa aina mpya huweza kuchukua muda mrefu zaidi kutegemea na idadi ya mahitaji ya magari kwa wakati huo;

(ii) Athari za kiuchumi zinazoathiri mnyororo wa uzalishaji na usafirishaji kwa mfano lilipokuja suala la UVIKO-19, iliyopelekea viwanda vinavyozalisha vipuri vya magari kufungwa na kupelekea changamoto ya uhaba wa vifaa vya TEHAMA ambavyo kwa sehemu kubwa ya magari ya kisasa hutumia teknolojia hiyo; na

(iii) Changamoto za usafirishaji wa magari, ikiwemo uhaba wa wasafirishaji na ukosefu wa makasha ya kusafirishia mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mnyororo wa ununuzi wa magari duniani umeanza kuimarika na magari yote yanafika kwa

wakati na kukabidhiwa kwa taasisi zilizoagiza. Aidha, hali ya upatikanaji wa magari kwa wakati imerejea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu licha ya ucheleweshaji wa ununuzi wa magari na kufikishwa kwa wakati, *GPSA* imekuwa ikinunua magari kwa gharama kubwa kuliko bei ambayo iko sokoni. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kushusha gharama ambazo soko la kawaida linauza magari hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nini mpango wa Serikali wa kununua ama kuagiza magari Japan moja kwa moja, badala ya kupitia kwa Wakala ambaye ni Toyota Tanzania? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kwenye bei za magari ukilinganisha na soko kuna mambo mawili, matatu ambayo yanajitokeza. Moja ni aina za magari ambapo sisi wote hapa tunajua magari ya aina ile ile yakiwa yanatokea Japan au yakiwa yanatokea South Afrika au yakiwa yanatokea maeneo mengine wanaotengeneza magari bei zao hutofautiana, lakini msisitizo na ambacho tumekifanya hata kwenye sheria ya manunuzi kwa sasa hivi tumeweka ukomo wa bei za bidhaa zozote ambazo Serikali inafanya zizingatie bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo lile alilolisema Mbunge Serikali imezingatia na halitakuwa kwenye magari tu, tumeweka hata kwenye bidhaa zingine. Kwamba kuanzia mfumo

wenyewe wa manunuzi Afisa Masuuli akitaka kulipia bei ambayo iko juu kuliko bei ya soko tunayoijua atakuwa anakiuka sheria. Kwa hiyo hilo litazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kuhusu kuagiza magari moja kwa moja kuna baadhi ya mazingira ambayo zikiwepo *specification* za baadhi ya bidhaa, sheria imeruhusu Afisa Manunuzi kununua moja kwa moja kutoka kwa muuzaji, lakini huwa inatokea katika baadhi ya maeneo wale wanunuzi wenyewe huwa hawapendi taasisi nunuzi ziende moja kwa moja kiwandani kwa sababu wanakuwa na *connection* na wale wanaofanya nao biashara. Kwa hiyo, wanakuwa na matawi yao, wanakuwa na mawakala maeneo mengine huwa wanatamani usiende moja kwa moja, wanatamani utumie kwa mawakala wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge, mtazamo wa Serikali ni kuendelea kupunguza masuala ya matumizi ya magari. Mtakumbuka kwenye Bajeti ya Serikali tunaendelea na utaratibu wa badala ya Serikali kuwa inamiliki magari, tunataka watumishi wenye sifa za kuwa na magari, wakopeshwe yale magari yawe yao ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kuyaendesha magari, kuyapatia *service* pamoja na vitu vingine vinavyotakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Malembeka. *(Makofi)*

Na. 118

**Kudhibiti Kampuni Binafsi za Ulinzi nchini**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, Kuna mpango gani kudhibiti Kampuni Binafsi za Ulinzi ili kuhakikisha haziendi kinyume na maadili ya kazi zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeweka utaratibu kwa mujibu wa Waraka Na. 3/2009 wa Usimamizi wa Makampuni Binafsi ya Ulinzi na Polisi Wasaidizi na Kuhakiki, Kusimamia, Kufanya Ukaguzi pamoja na Vikao na Wamiliki wa Makampuni ya Ulinzi. Pia Sheria Na. 2/2015 ya Leseni za Umiliki wa Silaha imeainisha utaratibu wa ukaguzi pamoja na matumizi ya silaha kwenye maghala ya kuhifadhia silaha, mafunzo ya umahiri kwa kutumia silaha na utunzaji wa silaha. Utaratibu huu husimamiwa na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na kwa kuratibiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Makampuni Binafsi ya Ulinzi na Polisi Wasaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shughuli za makampuni binafsi ya ulinzi hufanyika kila mwaka na wakati wowote pindi pakitokea ukiukwaji wa utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pia nampongeza Waziri kwa kazi nzuri anayoendelea nayo. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa Serikali yetu inatambua Askari wetu wastaafu wapo makini katika masuala ya ujuzi, uzoefu, maadili na uwezo wa kutumia silaha mbalimbali katika suala zima la ulinzi wa nchi, rais, na mali zao.

Je, Serikali haini ni muhimu sasa kwa makampuni hayo kumilikiwa na askari wastaafu badala ya kuwa mtu yeyote ananzisha Makampuni ya Ulinzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Serikali inatoa tamko gani juu ya raia wake ambao wanatembea hadharani na

mapanga, mashoka, sime, rungu kwa kielelezo kwamba wanatimiza utamaduni? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri sana. Nikianza na swali la kwanza, suala la kufungua makampuni binafsi ni suala la kibiashara, hivyo mtu yeyote ana haki ya kufanya biashara ikiwemo askari wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunadhani vilevile kulingana na Sera ya Jeshi la Polisi la kushirikisha wananchi kwenye ulinzi kupitia ulinzi shirikishi ni vizuri wananchi wakatumia fursa hiyo kuweza kuanzisha makampuni wakiwemo askari wastaafu. Hivi sasa wapo Askari ambao ni wastaafu wana makampuni hayo na yanafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na ubebaji wa silaha, hususan silaha za jadi; kubeba silaha za moto hadharani ndiyo kosa kisheria, lakini silaha nyingine inategemea unaitumiaje? Kwa mfano, sisi kule kwetu kuna watu wanaitwa Wakwezi, wale ambao kazi yao ni kuchuma nazi. Sasa kama ameweka kisu chake kwa ajili ya kupanda mnazi kuangusha madafu, lile siyo kosa, lakini akitoka pale akawa na dhamira ya kwenda kutumia kisu kile kufanya uhalifu, hilo ndiyo kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya hali ya ulimwengu unavyokwenda, bado Waheshimiwa Wabunge wana nafasi ya kuangalia sheria hiyo kwa siku zijazo kuishauri Serikali kama kuna haja ya kuangalia na kuongeza matumizi ya silaha nyingine za jadi iwe kama sehemu ya silaha ambazo zitakuwa ni makosa kutembea nazo hadharani, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Stella Simon.

Na. 119

**Maji safi na salama katika shule za msingi na sekondari**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka maji safi na salama katika shule za msingi na sekondari nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza inapatikana katika maeneo yote ikiwemo katika taasisi za umma za shule na vituo vya afya. Katika kutimiza hilo, Wizara inaandaa mpango maalum wa kuboresha huduma ya maji katika taasisi za umma ikiwemo shule zisizo na huduma hiyo ambapo maandalizi hayo yanatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na utekelezaji wake kufanyika katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2024/2025 hadi 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa shule nyingi zinashindwa kumudu gharama za ulipaji maji, Serikali ina mpango gani wa kuziongezea bajeti ya fedha ili ziweze kumudu gharama hizi za ulipaji maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa wa kutengeneza mifumo ya uvunaji maji ya mvua katika kila shule ili kurahisisha huduma na kupunguza gharama za uendeshaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na gharama za ulipaji maji, shule nyingi zinashindwa kuongezewe fedha. Naamini Wizara husika imesikia na ushauri utakuwa umepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uvunaji wa maji ya mvua katika shule zetu, ni moja ya elimu ambayo tumekuwa tukiitoa sisi kama Wizara kwa sababu tayari tumeanza uvunaji wa maji maeneo mbalimbali kupitia mabwawa. Katika shule pia, nalo niseme ushauri umepokelewa na tutaendelea kutoa msisitizo huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kata ya Mulbadaw hasa Kijiji cha Gidamambura ina changamoto kubwa ya maji na wananchi wanafuata maji zaidi kilomita 15: Je, Serikali iko tayari kuchimba kisima cha dharura ili wananchi waachane na adha hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, naomba niiagize *RUWASA* Mkoani kwako, watakwenda kuona, kufanya utafiti wa kama inahitajika kuchimba kisima au kuona njia gani itumike ili eneo lile liweze kupata huduma ya maji. Ikihitajika kuchimba kisima Mheshimiwa Mbunge, tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza; mwaka 2020 wadau kwa kushirikiana na Wizara ya Afya walifanya tathmini ya upatikanaji wa maji kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya kwa maana ya zahanati na vituo vya afya; na ikaonekana ya kwamba asilimia 53 ya zahanati na vituo vya afya havijaunganishwa na maji ya bomba, kwa hiyo, hakuna maji safi na salama: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaunganisha maji safi na salama katika vituo vyetu vya kutolea huduma kwa maana ya zahanati na vituo vya afya? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 53 ya vituo vya afya havina huduma ya maji safi na salama. Tunapopitisha miradi yetu katika maeneo mbalimbali, maeneo haya yenye vituo vya afya pamoja hata na shule, tumekuwa tukisisitiza watalamu wetu kuhakikisha wanaingiza huduma ya maji safi na salama. Kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba jinsi muda unavyozidi kwenda na tunavyoendelea

kupata fedha za kutekeleza hii miradi, tutahakikisha maeneo haya ya huduma ya afya na yenyewe pia tuendelee kutoa kipaumbele kuhakikisha yanapata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Serikali imekuwa na nia njema ya kuendelea kutatua changamoto ya maji hasa kwenye maeneo yetu na imeweza kununua magari ya kuchimba visima na kuyagawa kwenye mikoa yetu, lakini changamoto ni gharama kubwa ambayo inajitokeza pale taasisi za Serikali inapotaka kuyatumia magari hayo: Je, ni upi mwongozo wa Serikali unaoelekeza matumizi ya magari haya, gharama ziwe chini kuliko wachimbaji binafsi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kubwa za uchimbaji wa visima ni kutokana na ubora wa kazi unaofanywa na watalamu wetu. Unaweza ukachimbiwa na mtu binafsi kwa gharama ndogo, lakini baada ya muda ukaanza kulalamika unapata maji yaliyo chini ya ubora. Kwa hiyo, sisi gharama zetu zinaonekana kubwa, lakini ubora wa maji, kwa sababu huenda sisi tukaenda chini mita 200 ndiyo maana tukaku-*charge* shilingi milioni 20. Mtu binafsi ataenda tu mita 70, halafu atakwambia shilingi milioni tano, wewe ukaona ni rahisi. Kwa hiyo, ubora wa maji unakwenda kutofautiana na hapo ndipo gharama inapokuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba Mheshimiwa Rais anahitaji kuona kwamba, magari haya yanaendelea kutumika na watu wengi, tutaendelea kuona kadri tuwezavyo gharama ziwe rafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Noah Lemburis.

Na.120

**Hitaji la maji Kata za Jimbo la Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini maji yatasambazwa Kata ya Mlangarine, Vitongoji vya Longipa, Mbuni, Olkereyan, Olmaroroi na Shule ya Msingi Muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mkakati wa kuhakikisha maeneo ya Kata ya Mlangarine na vitongoji vyake vya Longipa, Mbuni, Olkereyan, Olmaroroi na Shule ya Msingi Muungano katika Jimbo la Arumeru Magharibi yanapata huduma ya maji safi. Katika kutekeleza hilo, kuanzia mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea kusogeza mtandao karibu na makazi ambapo hadi sasa bomba lenye urefu wa kilometa 55.7 zimelazwa katika Kata ya Mlangarine inayojumuisha maeneo hayo kati ya kilometa 116.8 zinazohitajika. Kupitia ulazaji huo, baadhi ya maeneo ya Vitongoji vya Longiva, Mbuni na Olkereyan yanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kuongeza mtandao wa bomba zenye urefu wa kilometa 12 ili kuendelea kusogeza huduma ya maji kwa wananchi wa Kata ya Mlangarine na vitongoji vyake ambapo hawajafikiwa na huduma. Ulazaji wa bomba hizo unatarajiwa kuanza mwezi

Desemba, 2023 na kukamilika mwezi Februari, 2024. Aidha, katika mkakati huo tutaendelea kutekeleza kwa kila mwaka ili kuhakikisha huduma inawafikia wananchi wa kata nzima na vitongoji vyake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa eneo hilo limekuwa na watu wengi sana kwa maana ya Vitongoji vya Longiva, Mbuni, Olkereyan, Olmaroroi; je, Serikali haioni ni vizuri ikapeleka maji kwa asilimia hiyo 47.3 iliyobaki badala ya kupeleka kilometa 12 peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Shule ya Muungano ina watoto wengi na hakuna maji; je, Serikali haini ni muhimu kuchukua hatua ya dharura kuwapelekea watoto maji ili kuwaepusha na magonjwa ya mlipuko hasa ikiwepo *UTI? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lemburis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tupeleke asilimia 47 na siyo hiyo tuliyoitaja, tutafanya hivyo. Hiyo ndiyo dhamira ya Wizara. Kadiri tutakavyopata fedha tutahakikisha tunatoa kipaumbele na tukitambua kabisa eneo hili lina changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Shule hii ya Muungano, naomba kupitia Bunge lako tukufu nimwagize *Regional Manager* wa *RUWASA,* Arusha ahakikishe anafika katika shule hii na kuona uwezekano wa kuwachimbia kisima waweze kupata huduma ya maji safi na salama ili watoto waweze kuendelea na masomo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kutatua changamoto ya maji na hata kununua magari kwa ajili ya ajili kuchimba visima hasa kwa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya, lakini mpaka sasa magari yale hayajaanza kufanya kazi maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijue mpango mkakati wa Serikali wa kuhakikisha sasa yale magari yanaanza kuchimba visima hasa kwenye maeneo ambayo hayana maji safi na salama Wilayani kwangu Rorya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafari, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Jafari amekuwa akifuatilia sana suala hili. Suala la magari kutumika, tayari magari yapo kazini, labda gari halijafika tu kwenye Jimbo lake kwa sababu kila Mkoa una gari moja. Kwa hiyo, napenda tu kumtoa hofu, tutahakikisha gari linafika katika Jimbo lake la Rorya na kuhakikisha maeneo yote ambayo yanahitaji huduma ya visima ambayo yanapitiwa mbali na mtandao wa mabomba, basi yanaweza kufanyiwa huduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo, jiandae Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Kata za Mbuguni, Makiba, Kikwe na Shambarai Burka ambako bomba kubwa la mradi wa shilingi bilioni 520 umepita? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kata alizozitaja ni kweli zimeshapitiwa na mradi wa bomba kubwa la mradi mkubwa ule wa Arusha. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wakati wowote ule utaanza kuona sasa matoleo yanawatokea na kuwafikia wananchi wako wa hizi kata zote ulizozitaja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Kata ya Lipwili ina changamoto kubwa sana ya maji kwa muda mrefu, ni lini sasa Serikali itatatua changamoto hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge tunafahamu ina changamoto, lakini tutachukua jitihada za makusudi kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha tutahakikisha tunakuja kuleta huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Simwanza.

Na. 121

**Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha kupooza umeme Wilayani Urambo ili kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na kazi ya Ujenzi wa Kituo cha Kupooza Umeme cha Urambo kinachogharimu jumla ya shilingi bilioni 16, ambapo kwa sasa ufungaji mitambo ikiwemo transfoma kubwa yenye uwezo wa *MVA* 35 unaendelea. Kazi ya ujenzi wa Kituo cha Kupooza Umeme cha Urambo imefikia asilimia 70 na kituo kinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa kituo hiki kutawezesha kuimarisha hali ya upatikanaji umeme katika Wilaya ya Urambo na maeneo mengine ya jirani, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shida kubwa ya umeme tuliyonayo Urambo, ni lini sasa Serikali itakamilisha utekelezaji wa *line* ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Urambo ili kuwezesha Kituo cha Kupoozea Umeme kuanza kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *line* ya kusafirishia umeme kutoka Tabora hadi Urambo unaenda sambamba na ujenzi wa kituo hiki cha kupoozea umeme. Ujenzi wa *line* hii utakuwa umekamilika ifikapo Juni, 2024 na hadi sasa umefikia asilimia 18, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kuna Mradi wa Kituo cha Kupoozea Umeme kinajengwa Ibadakuli hadi Bariadi. Wananchi walihaidiwa kulipwa fidia shilingi milioni 2.3, mpaka sasa wananchi hawajalipwa; je, ni lini Serikali italipa fidia hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Fidia ya eneo hilo tupo tunakamilisha tathmini, na ikikamilika basi tutaanza kulipa kabla ya mwaka huu kwisha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ningependa kumuuliza Naibu Waziri; suala la usambazaji umeme katika Manispaa ya Ilemela, kuna mitaa 29 haina umeme au umefikia nusu lakini kati yake ni nane haina kabisa. Isanzu, Kilabela, Igogo, Bujingwa, Kiswindi na Butindo. Ni lini watapewa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Angeline Mabula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshasaini mikataba mitatu ya ujazilizi. Mjazilizi wa Pili A, Mjazilizi wa Pili B na Mjazilizi wa Pili C. Katika mikataba hii baadhi ya mitaa ya Ilemela itapata umeme. Pia

tunategemea kusaini mkataba wa ujazilizi wa mitaa 15 ambapo, Jimbo la Ilemela pia litapata umeme katika mitaa hiyo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tayari tumeshasaini mikataba ambayo italeta umeme kwenye mitaa hiyo na mikataba yote inayofuata pia mingine tunatafuta wakandarasi ili kuendelea kuleta umeme katika mitaa hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni dhahiri *TANESCO* inaonekana kuelemewa na kazi za kuzalisha umeme, kusafirisha umeme, kusambaza umeme, *REA*, kukatikakatika kwa umeme.

Je, Serikali inaona kigugumizi gani ku-*restructure TANESCO* kama vile ilivyokuwa Kenya kufanya suala la *generation* mbali, usafirishaji mbali na usambazaji wa umeme mbali, ili kuleta ufanisi na tija katika shirika hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Tarimba Abbas kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshafanya mkakati wa miaka 10 ya *TANESCO* ambapo tunaenda kuboresha huduma zote za usafirishaji, usambazaji na uzalishaji wa umeme. Kwa hiyo, tunategemea makadirio yetu ni kwamba, tukifika 2030 tutakuwa tumeongeza uzalishaji wa umeme kufikia megawati 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mikakati imeanza na tunavyoelekea tutakamilisha na tutaboresha huduma zote kwenye maeneo yote matatu ili kuhakikisha tunaendelea kutoa umeme wa uhakika kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Serikali mna mpango mzuri na sasa hivi tunawapongeza mnakwenda vizuri. Kuna mpango wa kuanzisha Vinu vya Nyuklia. Kinu kimoja kinatoa umeme *megawatt* 600. *Fastrack* hii kitu umeme utapatikana kwa uhakika Tanzania, sawa.

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

Na. 122

**Umeme wa migodi kuacha vijiji Lulindi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza: -

Je, ni kwa nini vitongoji vinavyopitiwa na mradi wa kuweka umeme migodini vinaachwa bila umeme – Lulindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kupeleka umeme katika migodi umelenga kusambaza umeme kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi kupitia migodi na maeneo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* umeandaa mpango wa kusambaza umeme katika vitongoji ambapo vitongoji vyote vya Jimbo la Lulindi vitapatiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2023/2024, jumla ya vitongoji 58 vitapatiwa umeme kupitia mradi wa kusambaza umeme wa vitongoji 15 kila Jimbo na vitongoji 43 kupitia Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili C, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri lakini kama alivyosema kwamba, lengo ni kupeleka shughuli za kiuchumi, sasa kwa watu gani? Kwa sababu hapo panapopita umeme huu, hawa watu walioko katika eneo hilo hawaguswi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) Mkandarasi wa *REA* hafuati wigo *(scope)*ya kazi yake badala ya kupeleka umeme kilomita tatu, yeye anapeleka kilomita moja tu. Pia amekuwa akifanya kazi hii ya kusuasua. Nini, tamko la Serikali kuhusu Mkandarasi huyu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Mchungahela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na eneo ambalo limepitiwa na *line* bila wananchi wa eneo husika bila kupata umeme. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari pale kuna mradi unaendelea wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili na zikikamilika kilomita tatu basi wananchi wa hilo eneo husika watapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Mkandarasi huyu anayesuasua. Tayari Serikali tumechukua hatua kwa kukaa na huyu Mkandarasi na kujitahidi kumuongezea nguvu lakini nitoe maelekezo kwa Mkandarasi Namisi ambaye anahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma amekuwa akisua sua kwa muda mrefu. Napenda nimwambie kwamba hatutasita kusitisha mkataba pale ambapo mkataba wake utaisha ili kuwapa watu, wakandarasi ambao wanaweza kutekeleza miradi hii kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimsihi aendelee kutekaleza miradi hii kwa kadri ambavyo tumekubaliana na ifikapo

Tarehe 30 Mwezi wa 12 awe amemaliza maeneo yote haya, la sivyo tutasitisha mkataba wake na kutafuta wakandarasi ambao wanastahili, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Licha ya Serikali kufanya kazi kubwa ya usambazaji wa umeme katika maeneo yenye migodi ikiwepo Mkoa wa Shinyanga. Kumekuwepo na tatizo kubwa la uhaba wa vitendea kazi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu katika Mkoa wetu hasa nguzo za zege, kiasi ambacho Mkoa wetu umekuwa na tatizo la kukatika sana kwa umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka miundombinu ya kuboresha usambazaji wa umeme katika Mkoa mzima wa Shinyanga? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Mayenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tuna mradi mahsusi ambao unatekelezwa na Wakala wetu wa Nishati Vijijini *(REA)* kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye migodi na maeneo ya kiuchumi. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mradi huu kadri unavyoendelea tutahakikisha wakandarasi wanaopewa kazi, wanapata vifaa pamoja na miundombinu inayohitajika kwa wakati ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuwanufaisha wananchi wanaojishughulisha shughuli zao kwenye maeneo ya migodi na maeneo mengine mabayo yanachagiza shughuli za kimaendeleo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji na vitongoji lakini kumekuwa na uhaba na mgao mkubwa sana wa umeme hasa kwa Mkoa wa Iringa. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, angalau wananchi wanapata umeme kama inavyotakiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hiki kifupi ambapo tumekuwa tukipitia mgao wa umeme, tayari kama Serikali tumechukua hatua za haraka.

Moja, mashine mbili ambazo zilikuwa zimesimama Tegeta pamoja na *Ubungo One* tayari tumeshaziingiza katika uzalishaji. Vilevile Mradi wetu wa Rusumo unaozalisha megawati 90, tayari tumeshaingiza megawati 27 na vilevile megawati zingine 27 zipo katika majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mradi wetu wa Julius Nyerere mpaka kufikia juzi mradi umefikia 94.1% na tayari kwa mashine moja tumeshaanza majaribio ya kuzungusha tabaini na tunategemea mpaka ikifika Februari tutaanza uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuhaklikishie Mheshimiwa Mbunge zile upungufu wa megawati 421 tumeweza kupunguza sasa hivi tunaelekea chini ya megawati 200. Kwa hiyo, tunapoelekea hali ya upatikanaji wa umeme itaendelea kuimarika. Niwatoe shaka tunajithidi ili kuhakikisha ndani ya miezi hii miwili mpaka mitatu tunaondoa tatizo la upatikanaji wa umeme, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ni kweli umeme unaanza kuimarika. Ahsanteni sana *TANESCO,* mnafanya kazi nzuri Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hassan Kungu.

Na. 123

**Mpango madhubuti wa kukabiliana na wanyamapori wakali**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka mpango wa kukabiliana na wanyama wakali wanaosababisha vifo na hasara ya mazao kwa Wananchi wa Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Tunduru. Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tabia za wanyamapori na mbinu za kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu, ambapo vijiji 83 vyenye jumla ya wananchi 50,284 wa Wilaya ya Tunduru wamepatiwa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumefanya doria za udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu, kujenga vituo vya askari kwenye makazi ya wananchi ili kuwasogeza askari karibu na maeneo yenye changamoto. Vilevile kwa Wilaya ya Tunduru tumejenga Kituo cha Askari cha kudumu katika Kijiji cha Chingulungulu na Kituo cha Askari cha muda katika kijiji cha Mbesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumejenga vizimba vya kuzuia mamba wasidhuru wananchi wanapotumia maji ya mito na maziwa. Pia tumeanzisha Mfumo wa Kielektroniki ambao umeandaliwa ili kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji na Utunzaji wa Taarifa za Matukio ya Wanyamapori wakali na waharibifu, vilevile tumeweka namba maalum za simu kwenye vituo vya kanda za kiutendaji za taasisi za uhifadhi kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori bila malipo na kuandaa Mpango Kazi wa Kuongoa shoroba za Wanyamapori Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha usalama wa Wananchi wa Wilaya ya Tunduru pamoja na mali zao dhidi ya tembo, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za udhibiti ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari mawili, pikipiki tatu, ndege zisizo na rubani tano. Aidha, mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa vijijini yamepangwa kutolewa mwanzoni mwa Mwaka 2024 kwa ajili ya kuongeza nguvu katika udhibiti wa tembo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wilaya ya Tunduru ina ukubwa wa *square meters* za mraba 18,778 (eneo lake ni kubwa kuliko Mkoa mzima wa Mtwara) lakini tunao askari wa wanyamapori watano tu na jiografia yake siyo nzuri. Je, ni lini Serikali itaongeza idadi ya askari wa wanyamapori ili kuweza kuwasaidia wakulima wale kwa urahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio upya ya kifuta jasho kwa wakulima kutokana na malipo ya sasa mkulima akiliwa ekari moja analipwa shilingi 100,000 haiendani na thamani halisi ya mazao. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuongeza hiki kifuta jasho? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hassan Kungu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi. Serikali imejielekeza kwenye kuhakikisha ifikapo mwanzoni mwa mwaka kesho tunaendesha mafunzo ya Askari wa Vijijini. Mafunzo haya tunatarajia tutafundisha takribani askari 166. Tukiweza kuyakamilisha haya tutakuwa na uwezo wa kupeleka askari wawili kwenye kila Kijiji cha Wilaya hii. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hali itakuwa imeimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya pili, tayari Serikali iko katika hatua za mwisho za kufanya mapitio ya kanuni za kifuta jasho na kifuta machozi. Ni imani yangu kwamba tutakapokamilisha zoezi hili, tutatangaza ili hatua za kufidia ziweze kufanyika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dkt. Chaya, ajiandae Mheshimiwa Aida.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki, tuna kilimo cha korosho kwa mfumo wa *block farming* lakini tembo wanawasumbua sana Wakulima wa Korosho. Je, nini Mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanapambana na hawa tembo ili Kilimo cha Korosho kiwe na tija hapo Manyoni? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, katika Wilaya ya Manyoni kuna Kilimo cha Korosho kinachoendelea. Kilimo hiki kimeanzishwa kwenye eneo la Ushoroba. Kwa hiyo, tunapambana sasa na changamoto ya wanyama ambao wamekuwa wakitumia maeneo haya kutoka kwenye hifadhi zetu na kwenda kuvamia maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imeweka mkakati wa kuondoa shoroba hizi. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali itajielekeza kwenda kuondoa shoroba hizi ili tuondokane na changamoto tuliyo nayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida, ajiandae Kuchauka.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bunge la Bajeti lililopita Wizara ya Maliaslili na Utalii waliji-*commit* ndani ya Bunge kwamba, watakwenda kupitia zile kanuni kwa kuwa hazina uhalisia, kwa maana ya kwamba heka moja ndani ya mita 500 tembo wakila mazao yao wanalipwa shilingi 25,000 wakati heka moja inaweza ikatoa gunia 25 na gunia moja tu ni shilingi 75,000. Ni, lini mtakamilisha hilo zoezi na muwalipe wananchi badala ya kuwatia umasikini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Aida swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu yaliyopita, Serikali inakamilisha mapitio ya kanuni hizi. Naomba wawe na subira tuzikamilishe vizuri, namini tutapata ufumbuzi wa tatizo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Pamoja na kwamba Serikali inasema kwamba inaandaa mikakati mbalimbali ya kukabiliana na wanyamapori lakini Wilaya ya Liwale kwa asilimia kubwa imezungukwa na Pori la *Selous* pamoja na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini, Mikakati ya Dharura ya Serikali kuokoa maisha ya wananchi yanayotokana na wanyamapori? Kwa sababu mpaka sasa hivi watu wameshatoka mashambani na njaa zimeshaanza kuingia vijijini kutokana na wanyamapori na Serikali wanasema kwamba mnaandaa mipango mpaka mwakani. Sasa mipango gani ya dharura ya kuokoa maisha ya wananchi ambao wanaathirika na tembo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kuchauka swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Liwale ni miongoni mwa maeneo ambayo tuna changamoto ya wanyama wakali na waharibifu. Kwa kulitambua hili Serikali imeongeza doria katika eneo hili ili kupambana na wanayamapori hawa. Serikali imeongeza idadi ya Askari wa Vijiji wa Wanayamapori. Vilevile tumekuwa na jitihada mbalimbali za kuhakikisha tunakuwa na mifumo ya kuweka kora kwenye makundi viongozi ya tembo, ili tembo wale wanapotoka kwenye hifadhi iwe ni rahisi kuwafuatilia na kuweza kuwaswaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kuchauka atakumbuka tulipokuwa Tunduru Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo tunakuja na zoezi la pamoja ambalo litaenda kusaidia kupambana na changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya mkakati huo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani na Serikali tunaenda kulimaliza tatizo hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea muda wetu umekwisha. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

Na. 124

**Ugonjwa *sickle cell* nchini**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, ni Watanzania wangapi wenye tatizo la *sickle cell* na ni Mikoa mingapi imeathiriwa sana na ugonjwa huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA), jumla ya wagonjwa 86,990 wa *sickle cell* walihudumiwa kwa mwaka 2022. Aidha, takribani watoto 11,000 kwa mwaka huzaliwa nchini wakiwa na ugonjwa wa Selimundu unaohusisha kurithi vinasaba toka kwa wazazi. Hivyo basi, takribani watu 200,000 nchini wana ugonjwa wa *sickle cell*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa iliyoathiriwa zaidi na ugonjwa wa *sickle cell* ni Mwanza, Tabora, Kigoma, Mara, Dar es Salaam na Pwani. Tafiti pia zinaonyesha, sehemu zenye maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa wingi ndizo ambazo pia zina wagonjwa wengi wa *sickle cell.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninashukuru majibu ya Serikali; nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, nini mkakati wa Serikali wa kutoa uelewa katika ile mikoa ambayo imebainishwa kwamba ina wagonjwa wengi wa *sickle cell? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swaLi langu la pili; ni nini mkakati wa Serikali wa kuwaelimisha watarajiwa wa kuoana ambao wana maambukizi ili kusudi waweze kuchukua hatua? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza; kwanza nimpongeze kwa sababu, kwa kweli amekuwa na mchango mkubwa sio tu kwenye kuuliza maswali, lakini kwenye kuja mwenyewe Wizarani kuhamasisha baadhi ya mambo mbalimbali anayofikiri yanahusu jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kujibu swali lake la kwanza. Kwanza tuna kampeni ambayo inafanyika na *American Society of Nephrology* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu chetu cha Muhimbili ambacho wanaenda sehemu mbalimbali wanafanya utafiti na kila mwaka wanagundua watoto 10,000 wenye tatizo hilo, lakini pia tunatumia siku za kuadhimisha haya magonjwa na kuhamasisha kwa njia mbalimbali, lakini sasa tunaamua kwamba, twende kila hospitali, kila mtoto anayezaliwa tuhakikishe kwamba, anapimwa tatizo hili, ili kuweza kuwatambua mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni hili la kusema kwamba, tunafanyaje watu ambao wanataka kuoana watambue afya zao. Kwa kweli, hilo linafanyika kwenye kampeni zetu. Wakati

wote tunawahamasisha wachumba waweze kupima, ili kujua hali zao kama wana hizo *trait* za *sickle cell* kabla hawajaamua kupata watoto.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutokuwepo kwa huduma za vipimo za uginjwa huu katika maeneo mengi hapa nchini, idadi ya wagonjwa ni kubwa sana na Tanzania ni ya tano duniani na hapa Afrika sisi ni watatu kwa kuwa na wagonjwa wengi wa selimundu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuja na Sera ya Afya ya Selimundu, ili hili kundi ambalo linakumbwa na huu ugonjwa waweze kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali zuri la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, yote aliyoyasema ni kweli kwamba, sisi duniani ni watano, lakini pia kwa Afrika ni watatu kama ambavyo anasema, lakini nimhakikishie kwa *investment* ambayo Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na ameiingiza kwenye afya kwa maana ya trilioni 6.7 na mliona akigawa vifaa mbalimbali, tatizo hilo la kwamba, hakuna vifaa sio tatizo tena. Suala ni sisi kujipanga katika kila hospitali na katika kila kiliniki, watoto wanaozaliwa kuwa *screened* na kutambuliwa mapema. Ndiyo maana unaona kila mwaka sasa tuna uwezo wa kutambua watoto 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kwa sera tulizonazo zime-*accommodate* hilo tatizo. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuja na sera nyingine, sera

tuliyonayo ya afya ambayo muda si mrefu inaenda kurekebishwa kwa ajili ya ku-*accommodate* mambo mengine likiwepo hilo eneo la *sickle cell,* kwa hiyo, hatuna sababu ya kuwa na pekee ya *sickle cell.*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ndulane.

Na. 125

**Kuhamisha Mifugo Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhamisha mifugo kutoka Wilaya ya Kilwa kwenda katika maeneo mengine nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya mifugo iliyopo Wilayani Kilwa ni takriban ng'ombe 121,176, mbuzi 25,883, kondoo 6,587 na punda 218. Kufuatia uwepo wa mifugo hiyo, Serikali imepanga kuendelea kuboresha mazingira ya ufugaji kwenye Mkoa wa Lindi, ikiwemo Wilaya ya Kilwa kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kuanzisha mashamba darasa ya malisho kwa lengo la kutoa elimu kwa wafugaji ili waweze kuzalisha malisho kwa ajili ya mifugo yao;

(b) Kuendelea na ujenzi wa majosho;

(c) Kutoa dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo ili kudhibiti magonjwa ya mifugo; na

(d) Kuwezesha Serikali za Vijiji kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ili kuondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ni fursa kwa wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kuongeza na kukuza uchumi. Hivyo, Serikali itaendelea kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo na kuboresha kosafu za mifugo iliyopo, ili ufugaji uwe wa tija na unazingatia uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ndani ya miaka miwili iliyopita katika Wilaya yetu ya Kilwa, tumepoteza watu takribani 10 hivi ambao wameuawa na jamii ya wafugaji kutokana na mapigano yanayoendelea. Wiki iliyopita tu, tumepoteza wananchi wawili, mmoja anaitwa Zuberi Abdallah Mpili na mwingine anaitwa Shaibu Said Mwangu katika Kijiji cha Liomanga, katika Kata ya Namayuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mifugo ilitoka kwenye Bonde la Ihefu, mingine ilitoka Pori la Burigi, Chato, lakini pia hata ile iliyokuwa Ngorongoro ilihamishiwa Handeni. Sasa kuna tatizo gani kwa Wilaya ya Kilwa na Mkoa wa Lindi kwa ujumla kuondolewa hii mifugo, ili ipungue ibaki ile ambayo inatosheleza kulingana na malisho yaliyopo na kiasi cha maji kilichopo, kuna shida gani? Naomba Serikali watupe sababu za msingi kwa nini hawataki kukubaliana na hoja hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tuliahidiwa wakati mifugo inatolewa Ihefu kuletwa Mkoani Lindi kwamba, miundombinu ya majosho pamoja na miundombinu mbalimbali ingeimarishwa, lakini mpaka leo hiyo shughuli haijafanyika. Sasa sijui Serikali inatuahidi nini katika jambo hili la kimkakati ili tunusuru na mapigano ambayo yanaendelea kule Kilwa, Liwale na Nachingwea? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni lazima tukubaliane kwamba, wale ni Watanzania wenzetu na wanapaswa kuishi mahali popote ambapo wanaruhusiwa kwa mujibu wa sheria na ilimradi wasivunje sheria. Sasa hapa changamoto kubwa ni kwamba, vijiji ambako wafugaji wetu wanapatikana ni vema wakapanga matumizi bora ya ardhi, ili ifahamike wapi wafugaji wanaishi, wapi wakulima wanaishi, ili kupunguza hii migogoro kwa sababu hawa ni Watanzania na Serikali inaruhusu kwa mujibu wa sheria Watanzania popote pale unaweza ukaishi, ilimradi usivunje sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika msingi huo, sisi Wizara tumekuja na mkakati; kwanza kuwaelimisha wafugaji wapunguze mifugo na kuingia kwenye ufugaji wa kisasa ili kupunguza hizi kelele, kwa sababu, utakuta mfugaji ana ng’ombe 1,000 lakini tija ya hao ng’ombe 1,000 ni sawasawa na ng’ombe 100 na ng’ombe 1,000 wanahitaji eneo kubwa zaidi kuliko ng’ombe 100. Kwa hiyo, tunazidi kutoa elimu kuhamasisha wafugaji wetu waondokane na ufugaji wa kizamani waanze kufuga kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi zaidi ni kwamba, tayari Wizara …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** … imeshapeleka wataalam kwa ajili ya kwenda kupanga matumizi bora ya ardhi, ili ifahamike wapi wanatakiwa kufuga na wapi wanatakiwa kulima. Wizara baada ya kupata huo mpango wa matumizi bora ya ardhi, tuko tayari kwenda kujenga majosho kwenye maeneo hayo ambayo watakuwa wamekubaliana, wapi wanafuga na wapi wanafanya kilimo, ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU,* marafiki 18 wa Spika wakiongozwa na Ndugu Joyce Mwakifwambwa, mkuu wa msafara ambaye pia ni Afisa Michezo Jiji, Mbeya na Ndugu Estuta Stima, Mkuu Msaidizi wa Msafara, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi wanne wa Shule ya Sekondari ya *Amana Muslim Welfare Trust,* Ilongero, Singida, wakiongozwa na Ndugu Abdallah Rahman Kundya, Mkurugenzi wa Shule, karibuni. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni kumi wa Mheshimiwa Khamis Chiro, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Walimu wa Sekondari ya Jimbo la Uzini, Wilaya ya Kati ya Mkoa wa Kusini Unguja, wakiongozwa na Asha Khalfan Selemani, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 61 wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, Wenyeviti na Makatibu wa UWT kutoka Kishapu, Mkoa wa Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 145 wa Mheshimiwa Husna Sekiboko, Viongozi wa UWT kutoka Mkoa wa Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu, mwanasaikolojia kutoka Zanzibar, karibu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, wawekezaji kutoka Korea Kusini, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Asya Mohammed, hawa ni rafiki zake kutoka Zanzibar, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ali Mlaghila Jumbe kutoka *RUWASA,* Mkoa wa Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, ndugu zake kutoka Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Lucy Sabu, Mkurugenzi wa Taasisi ya *Juniors and Child Care Foundation* kutoka Mkoa wa Simiyu, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Venant Daud, wapigakura wake kutoka Jimbo la Igalula, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete, Kada wa CCM kutoka Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara, karibu. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Ndugu Anna Jackson Sipembe na Ndugu Shoshe Suzan Katende, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho siku ya Alhamisi, tarehe 9 Novemba, utafanyika uzinduzi rasmi wa *Bunge Marathon* katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge. Uzinduzi huu utashirikisha Wabunge na wadau kutoka taasisi mbalimbali nchini ambazo zinatarajiwa kudhamini *marathon* hii. Mgeni rasmi katika uzinduzi huu atakuwa ni Mheshimiwa Dkt.

Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria uzinduzi huu muhimu ili kufanikisha *marathon* hii ya kwanza katika historia ya Bunge letu.

Mheshimiwa Agnes Hokororo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, anaomba kuwatangazia Wabunge wote na watumishi wa Bunge kuwa leo tarehe 8 Novemba, baada ya kuahirisha kikao cha Bunge jioni kutakuwa na hafla fupi ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hafla hiyo, itafanyika katika viwanja vya Bunge, wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa mafunzo ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu Mfumo wa Uanzishaji Tamko la Njia ya Mtandao iliyokuwa ifanyike leo siku ya Jumatano, tarehe 8 Novemba, imeahirishwa, badala yake wataalam kutoka Sekretarieti ya Maadili wa Viongozi wa Umma kwa kushirikiana na wataalam wetu wa TEHAMA watakuwepo chumba kilichopo jirani na Ofisi ya *Seargeant-At-Arms* kuanzia tarehe 8 hadi 10 Novemba, ili kutoa mafunzo ya ujazaji fomu hizo kwa makundi madogo madogo ya Waheshimiwa Wabunge kwa kadri ambavyo watajitokeza.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnahimizwa kuwatembelea wataalam hao kwa ajili ya kupata mafunzo hayo muhimu ya ujazaji fomu kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Rashid Shangazi, Katibu wa Wabunge wa CCM, anaomba kuwatangazia Wabunge wote wa CCM, kikao cha *Party Caucus* leo saa 7.00 mchana, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, mahali ni *White House,* CCM Makao Makuu.

Katibu.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku.

**NAIBU SPIKA:** Hoja ya Dharura.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 79, ili kuomba Shughuli za Bunge zisitishwe kujadili jambo mahususi ambalo limetokea jimboni kwangu na kwa ridhaa yako naomba unipe nafasi niweze kutoa maelezo, ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuniunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana jimboni kwangu kuna mwananchi ambaye ameuawa na tembo, lakini leo asubuhi, saa 1.00 asubuhi kuna mwananchi mwingine ameuawa na tembo. Jana ameuawa mwananchi ambaye anaitwa Telesfori Yusti Agusti, mwenye umri wa miaka 28 katika Kijiji cha Mangale, Kata ya Mangale. Leo asubuhi ameuawa mwananchi anaitwa Leah Likwaso Lekole, mwenye umri wa miaka 45 ambaye anatoka katika Kijiji cha Mangae, Kitongoji cha Mkangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka nazungumza hapa tumeshapoteza wananchi sasa hivi wanafika 40, lakini majeruhi ambao wametokana na tembo ni zaidi ya 20. Mara kadhaa kwenye michango yangu nimekuwa nikitoa mchango na kuiomba Serikali ichukue hatua za makusudi kunusuru jambo hili. Leo nimelazimika kusimama kwa Kanuni hii ya 79 kwa sababu, hali ni mbaya na wananchi wamepanga kuandamana kufunga Barabara ya Iringa *(Iringa Road)* ili wananchi waoneshe hisia zao na Serikali iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wamekufa wananchi wawili, jana na leo, wamefika jumla 40 Serikali haijachukua hatua zozote.

Tunataka wafe wananchi wangapi ndio Serikali iende ikachukue hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kufa mwananchi ni jambo la kawaida sana, kufa na tembo. Juzi juzi tumeona kupitia vyombo vya Habari, kuna mwananchi Iringa pale amefungwa miaka 22 kwa sababu ya kukutwa na nyama kidogo tu ya swala. Leo watu wanakufa wanafika 40, hakuna hatua za makusudi zilizochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja, Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, ili tujadili jambo hili la dharura na Serikali iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kaeni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mbunge ametoa hoja yake kwa mujibu wa Kanuni ya 79. Kwanza pole kwa matukio hayo na kwa Wabunge wote. Serikali iko hapa, mmesikia na hii kweli ni kero ya siku zote inajitokeza, basi naomba Serikali mjitahidi kutafuta njia ya kuepuka hivi vifo ambavyo siku zote vinaathiri wananchi wetu.

Mheshimiwa Mbunge, baadaye utaonana na Waziri wa Maliasili na upande wa Serikali watajipanga wasikilize vizuri hoja yako na kujaribu sasa kuondoa kero hiyo. Pole sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sendeka.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama chini ya Kanuni ya 76, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139 na Kanuni ya 36 (4).

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba nilipokuwa nachangia siku ya Jumamosi hoja ya *CAG,* nilitoa hoja mwishoni ya kuomba kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge. Wakati Mheshimiwa Hasunga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* alipokuwa akihitimisha alisema kwamba Kamati imekubaliana na hoja yangu sehemu (a) inayotaka Serikali iokoe fedha zote zilizokuwa zimetajwa na *CAG,* lakini akaacha hoja mbili ziamuliwe na Bunge kwa maana ya sehemu (b) na sehemu (c).

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu (b) ilikuwa inataka Mawaziri na Makatibu Wakuu na Maafisa wengine ambao walikuwa na dhamana waliotajwa na Ripoti ya *CAG* wajitafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu (c) ilitaka mambo mawili; Kamati Teule ikaangalie uwezekano wa mfumo mzuri utakaosaidia katika kufuatilia Maazimio ya Kamati, baada ya Ripoti ya *CAG,* lakini kuweka bayana majina ya watu na kiasi cha athari au dosari zilizoonekana ili Kamati hiyo ipendekeze kwa Bunge hatua madhubuti zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya hawa wanaokula bila kunawa mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu iliungwa mkono na Bunge, lakini Mheshimiwa Spika alisema hivi kwa sababu alikuwa hajapata nakala, naomba kunukuu Mheshimiwa Spika alisema; "Waheshimiwa Wabunge siko nayo hii hoja hapa mbele, siko nayo na yeye amewaambia kwamba amekabidhi. Kwa hiyo, pengine wanatazama utaratibu mzuri wa kuitumia, siko nayo hapa mbele, kwa hiyo, siwezi kusema kama imeungwa mkono ama kwa namna gani."

Mheshimiwa Naibu Spika, badaye baada ya hoja kuja kuwekwa Mezani, Mheshimiwa Spika kwa busara zake akaizungumza kidogo sehemu ile ya (c) ya kuundwa kwa Kamati Teule akasema; "Waheshimiwa Wabunge jambo lingine lililokuwa limezungumzwa hapa, nadhani nilishalieleza kwa sehemu, ni lile la uundaji wa Kamati Teule. Nimeshatoa maelezo kwamba tujaribu kwanza huu mfumo tuliouanzisha tuone unatupeleka sehemu gani."

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo nilisimama baadae baada ya kuona kwamba sehemu ambayo Mheshimiwa Spika ameielezea ni kwamba hoja yangu haijaamuliwa, lakini Mheshimiwa Spika akasema hivi wakati anahitimisha mwishoni wakati anafunga kikao, naomba kunukuu kwenye *Hansard;* "Waheshimiwa Wabunge pamoja na hayo alisimama hapa Mheshimiwa Ole-Sendeka akisema Mwongozo. Sasa kwa sababu kwa kawaida Miongozo hawezi kuibeba kutoka leo kwenda siku nyingine lakini nafikiri Miongozo hapa leo ilikuwa mingi sana, tukubaliane kwamba Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa sababu Mwongozo anataka kujua kama jambo hili linaruhusiwa ama haliruhusiwi, tutapata nafasi ya kujua alitaka kujua nini, halafu Bunge litajulishwa kwa ajili pia ya kutunza afya zetu kidogo. Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana." Halafu ndiyo Mkutano ukaelekea kwenda kuahirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, wakati huo ni Jumamosi, Siku ya Jumatatu viporo vilivyokuwa vimehama kutoka Jumamosi kuja Jumatatu, wenzangu walipata nafasi ya kujieleza hapa na wengine hoja nyingine ya Mheshimiwa Shangai ilipelekwa siku ya mwisho ya Bunge lakini ya kwangu ikawa kimya. Sasa, nilikuwa nasema kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni, hoja iliyoletwa ilitakiwa iamuliwe na Bunge na ilishaungwa mkono na Bunge na Mheshimiwa Spika hakuikataa hoja hii huko na Watanzania wanasubiri Mheshimiwa Spika kuona hatua ambazo Bunge hili litachukua kutokana na vitendo vya ufisadi wa matrilioni ya hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwongozo wako kwamba nitapata nafasi wapi ya kusimama sasa ili hoja hii ya kwangu iweze kuamuliwa na Bunge au ikataliwe kwa namna yoyote

ili niweze kutenda wajibu ambao uko mbele yangu. Nakuomba Mwongozo wako juu ya utaratibu wa kuhitimishwa kwa hoja yangu, kwa sehemu (b) na sehemu (c). Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendekea, kwanza unayo Kanuni hapo?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo.

**NAIBU SPIKA:** Soma Kanuni namba 78.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni namba 78 nadhani hiyo itakuwa inahusu mamlaka ya mwisho ya Spika.

**NAIBU SPIKA:** Wewe isome.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, inasema hivi; "Uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la Utaratibu, Mwongozo au Taarifa utakuwa ni wa mwisho."

Kifungu hiki hakihusiani na hoja niliyoileta, kwa sababu si Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Sasa wewe Mheshimiwa Ole-Sendeka, kaa chini kwanza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma nipe nyingine.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini, kaa chini.

Sasa wewe ndiyo refa, wewe ndiyo mchezaji, wewe ndiyo mfunga magoli, wewe ndiyo *linesmen*. Mheshimiwa Spika alishatoa maelekezo wakati wa hoja yako na maelekezo ya Spika ni *final*.

Pili, kwa vile mimi siwezi kurudia tena au ku-*question* maelekezo ya Spika ambaye ndiye mwenye Mamlaka katika Bunge hili na kama utakuwa na malalamiko zaidi, tumia Kanuni ya 5 ya kuandika barua kwa Katibu kueleza *grievance* ambazo unazo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge Majadiliano yanaendelea, tunaanza na Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Kiswaga ana dharura atakuwa wa pili na Mheshimiwa Kakoso atakuwa wa tatu.

Mheshimiwa Francis Mtinga, hayupo? Mheshimiwa Kiswaga, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi leo nipate kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Maandalizi ya Mpango wa Bajeti 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuunda Tume ya Mipango ambayo ilikuwa ni kilio cha Wabunge wengi, pia tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Profesa Kitila Mkumbo, mtu mahiri kabisa kuisimamia Wizara hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo ningependa kushauri eneo la mipango. Tumeangalia mpango umekuwa na vipaumbele vingi vizuri lakini kuna mambo ambayo tungependa kushauri kujazilizia kidogo. Kwa mfano, upande wa uwekezaji kwenye viwanda lakini ningependa kujielekeza zaidi upande wa viwanda vya madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania imefanya kazi kubwa sana ya kuwekeza katika miundombinu ya afya. Ukianza kwenye zahanati, ukienda kwenye vituo vya afya, ukienda kwenye hospitali za Wilaya, hospitali za Mikoa, hospitali za Rufaa lakini wamenunua vifaa kila eneo. Pia ukiangalia ongezeko hili la miundombinu limesababisha pia matumizi ya dawa nchini kuongezeka sana. Sasa ushauri wangu ninafikiri kwenye mpango wangeona uwezekano wa kuona ni namna gani tunaweza kujipanga kujenga viwanda nchini kwa ajili ya vifaatiba, kwa ajili ya dawa na vifaa tendanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kwa taarifa ambazo nimezipata pale Wizara ya Afya ni kwamba, tumetumia kiasi cha dola milioni 253.25 kwa ajili ya kununua madawa ambayo ni sawa sawa na bilioni 590. Kati ya fedha hili dola milioni 16.9 sawa sawa na shilingi 39,377,000,000, hizo peke yake ambazo ni sawa na asilimia 6.7 ndiyo manunuzi yaliyofanyika katika viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ukiangalia hali ya mtiririko wa dola nchi na uhaba wa dola hasa nchini na nchi zinazozunguka hapa, kama tungeweza kuwekeza kuwa na mpango wa kuwekeza viwanda vya madawa nchini na vifaatiba, tutaweza kupunguza matumizi ya dola. Hivyo, kwa sababu sasa tutakuwa tunanunua

nchini, kwa hiyo itakuwa ni rahisi sisi kupunguza hayo matumizi ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napenda kushauri, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo aone uwezekano wa kuweka mipango ya kuwa na viwanda vya dawa nchini. Hili jambo litaisaidia sana nchi lakini pia mkumbuke kwamba tuna malengo tukifika mwaka 2030, manunuzi ya nje na manunuzi ya ndani yafike asilimia 50. Kwa hiyo ni muhimu kuanza mikakati sasa ili kuweza kufikia hapo malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na pili ambalo ningependa kushauri hasa katika mapendekezo ya kusaidia ukuaji wa uchumi nchini, hasa katika ukusanyaji wa mapato, napenda kuishauri Serikali ione namna gani ya kutengeneza miundombinu wezeshi ambayo itapelekea ukuaji wa uchumi nchini. Miundombinu wezeshi iko mingi kwa mfano, kwenye upande wa mawasiliano, mawasiliano yamekuwa yakichangia kwa kiasi kikubwa hasa ukuaji wa biashara lakini na huduma nchini. Wanasema kwamba dunia sasa hivi inakwenda kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hii miundombinu wezeshi kwa maana ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, kwa maana ya minara vijijini na tuka-*blanket* nchi nzima, tutaweza kuchangamsha biashara kwa sababu wengi wanatumia mitandao kufanya biashara na huduma mbalimbali. Kwa hiyo, huo ni muundombinu mojawapo wezeshi ambao ninafikiri kwamba Serikali ione namna gani itaimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mingine wezeshi ni upande wa barabara. Hapa hasa nikiangalia Nyanda za Juu Kusini, tumesema kwamba tuna zile fedha ambazo Serikali ilikuwa imezikopa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ule wa *REGROW* na hizi fedha zimekaa muda mrefu, kwa hiyo, tuna ujenzi wa barabara ya *Ruaha National Park* ambayo itakwenda kuchochea ukuaji wa uchumi Nyanda za Juu Kusini na maeneo mengine ambayo yameorodheshwa katika ile miradi ya *REGROW*. Napenda kuona

Serikali inakwenda kumaliza hii miundombinu ili sasa tuchochee ukuaji wa uchumi Nyanda za Juu Kusini na kupata dola za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mwingine ambao ningependa kushauri ni kwamba, kwenye upande wa ujenzi wa mabwawa na huu ni muundombinu mwingine ambao ni wezeshi katika kukua kwa uchumi. Nchi yetu imeanza sasa hivi kupitia, maeneo mengi yameanza kupata ukame, katika ujenzi wa haya mabwawa, Serikali ingeweka kipaumbele katika yale maeneo ambayo tayari yameanza kuwa kame na tayari tumeanza kupata upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo mojawapo ambalo litakwenda kuwezesha kwenye kilimo sasa tuweze kuongeza tija, ninajua Serikali inaendelea lakini kama tukianza na yale maeneo ambayo tayari yameanza kuwa kame, itasaidia kwenda kasi zaidi. Miundombinu hii ya mabwawa siyo lazima iwe ya ajabu sana, kuna maeneo mengi ambayo tayari ni korongo, ukifunga hapa, ukifunga hapa tayari unaanza kukusanya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutolea mfano bwawa moja ambalo nimejenga kule kwangu, Mheshimiwa Aweso amejenga pale, amefunga tu tuta palikuwa pana korongo tayari maji yamejaa. Kwa hiyo, hatuna haja ya kufikiria teknolojia kubwa sana kutumia matrilioni, wakati tunaweza kuziba tu makorongo, yako mengi katika nchi hii na tukaweza kuanza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvunaji maji pia ni muhimu sana katika kutekeleza hiyo miundombinu wezeshi kwa sababu, maji yanapotea mengi sana hasa ukiangalia hata Dodoma, maeneo ya Bahi wakati wa mvua ni maji mengi sana yanapotea. Kwa, hiyo, kama tuna utaratibu wa kuziba haya makorongo, ni rahisi sana kuweza kutengeneza miundombinu na kuweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuangalie kwenye mipango yetu kama Taifa kuwa na programu ya upatikanaji wa maji toshelevu katika nchi. Tukiwa na programu ya Kitaifa ya kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kwa wingi ni rahisi sana kuvutia wawekezaji. Kwa mfano, tuna wawekezaji ambao wanataka kuja kuwekeza hapa Dodoma, wanasema wanataka kuja kujenga *five stars hotel* lakini wanasema kwa sababu ya upungufu wa maji, hatuwezi kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano kule Iringa, ninao wawekezaji ambao wanataka kuja kuwekeza kwenye viwanda vya parachichi lakini kwa sababu hatuna miundombinu ya majitaka, kwa mfano mtu anataka kujenga kiwanda cha parachichi, anataka kukamua mafuta kwenye parachichi unapata asilimia 10 peke yake ile asilimia 90 inakuwa ni *waste product*, kwa maana ni eneo la mabaki yanayopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukisema kwamba mwekezaji yeye mwenyewe atengeneze miundombinu ya majitaka, itakuwa ni gharama zaidi kwake. Kwa hiyo, tuangalie hii mifumo yetu kwenye maji, kuwa na programu ya maji ya kitaifa, yaani tuwe na mpango mkakati wa kitaifa, tukishamaliza sasa kwenye reli, tumemaliza sasa kwenye umeme, eneo lingine ambalo tunaweza kusisimua uchumi wa Taifa ni uwekezaji kwenye eneo la maji. Tuwe na programu kubwa za Kitaifa, tuwe na miradi mikubwa ya kimkakati na hii itakwenda kuchochea uchumi na uchumi wetu utakwenda kwa haraka. Kwa hiyo, mimi niliona ni muhimu sana haya maeneo tukayawekea mfumo ili kuanza kukuza uchumi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia kama ni eneo muhimu katika kutengeneza miundombinu wezeshi ya kuuza uchumi ni eneo la bandari. Tanzania imekuwa ikizalisha mazao hasa haya yanayoweza kuharibika haraka *(perishable foods)*. Ukiangalia matunda ukiangalia mboga lakini liko soko kubwa sana la bidhaa hizi Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata India sasa wameanza kutumia parachichi, lakini kwa sababu hatuna miundombinu mizuri hasa wanaita hizi *storage system*, kwamba katika eneo letu la Bandari ya Dar es Salaam ni muhimu sana sasa Serikali ikafikiria ni namna gani tunakwenda kupanua hii miundombinu ya kuifadhi mazao yetu yanayoharibika. Mboga mboga na mtunda katika Bandari kubwa kama ya Dar es Salaam ili tuweze kuyasafirisha kirahisi, hili ni eneo kubwa ambalo pia litakwenda kuchechemua uchumi wa Taifa na tukaweza kuitumia bandari yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona ni muhimu basi nichangie kwa haya machache ili tuweze kukuza uchumi pia kuweka mipango yetu ya muda mrefu. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji kwenye mpango huu wa Taifa ambao Watanzania wanausubiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu kwenye mazingira. Tanzania ni nchi ambayo inamiliki hekta 9,930,650. Hizo ni hekta ambazo zipo kwenye *National Parks*. Nchi yetu hatujatumia mazingira mazuri ambayo yanaweza yakaleta uchumi mzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi jirani ya Kenya wameitumia fursa vizuri, kwenye *National Parks* wanazozimiliki. Mwaka jana walivuna fedha za hewa ya ukaa *US dollar* bilioni moja ambazo zimeleta fedha nyingi kwa Taifa lao. Sisi misitu tuliyonayo tumeshindwa kuitumia vizuri na tungekuwa na pato ambalo ni zaidi ya *US dollar* bilioni tano ambazo tungezipata kama Taifa. Bahati mbaya sana Serikali haijawahi kuchukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na mwaka jana nililitela hili hapa na halikufanyiwa kazi, matokeo yake kila bajeti inayokuja tunajielekeza kwenye mambo

madogo madogo ambayo yanakuja kupandisha gharama za maisha kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tuitumie fursa tuliyonayo ambayo Mwenyezi Mungu ametupa ili iweze kuleta manufaa kwa Taifa letu. Hatuwezi kufanya hayo, lazima tufanye mabadiliko ya sheria. Huwezi kuvuna hewa ya ukaa kwenye Hifadhi ya Taifa bila kubadilisha sheria. Tujifunze kwenye Mataifa ambayo wenzetu wamenufaika nayo. Nchi ya Zambia wana kampuni nyingi sana ambazo sasa hivi wanavuna hewa ya ukaa. Mwaka jana niliwaambia, nchi ya Pakistani baada ya kupata *Tsunami* waliyatumia yale maeneo wakahamisha wananchi, wakaandaa mpango kazi wa kurejesha mazingira ambayo yameanza kuwannufaisha Pakistani, wanavuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, unapata mawazo na unafikiria mara mbili mbili, Pakistani ambao hawana misitu wanapata fedha sisi ambao tuna misitu mingi hatuitumii vizuri. Kenya wanatumia baadhi …

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kakoso, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Kakoso kwa sababu, katika miongoni mwa watu ambao wameleta mchango mkubwa sana katika eneo hili ni Mheshimiwa Kakoso. Serikali kutokana na mawazo hayo mazuri, mwaka jana mwezi Oktoba tulikuja na Kanuni na Mwongozo Mpya wa Biashara ya Hewa ya Ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mpaka hapa nilipokuwa, zaidi ya makampuni 33 yameshafanya *registration* ya biashara ya hewa ya ukaa; na kati ya makampuni 33, makampuni 11 tayari yameshapata *endorsement letter* kwa ajili ya kufanya biashara hiyo. Katika makampuni machache ambayo tathmini kutoka *Carbon*

*Monitoring Center* inaonesha kwamba zaidi ya dola za kimarekani bilioni tatu zitapatikana. Maana yake ni trilioni nyingi zaidi zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Kakoso, mchango wake ni mzuri. Nimhakikishie kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana na *endorsement letter* nyingine zimetoka siku tatu zilizopita katika Ofisi ya Makamu wa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, shilingi trilioni saba hizo juu ya fedha zako, hongera sana. Mheshimiwa Kakoso, endelea na mchango mzuri.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa ambayo nimeipata kutoka Serikalini, Watanzania ni miongoni mwa wabunifu, lakini mipango yetu huwa hatuiendelezi. Wakati sisi tunaendelea kwenye mifumo ya kuandaa mipango, wenzetu wanapata fedha hizo na zinawasaidia. Kenya wamewashirikisha kampuni ya ndege ya *Etihad*, ndiyo waliowapa *US Dollar* bilioni moja. Sisi tuna *Emirates* ambao tungewawahi tungepata fedha nyingi sana ambazo zingetusaidia, lakini matokeo yake Serikalini kila mwaka tutakuja na mipango hii hii ambayo huwa ahifanyiwi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya yafanyiwe kazi ili Serikali iepukane kuongeza gharama za kupandisha gharama za mafuta ambazo zinakuja kumfanya mwananchi wetu ashindwe kuendana na mazingira halisi. Ninao mfano, kwenye eneo la jimbo langu ndiyo pekee ambapo wanavuna fedha za hewa ya ukaa. Mwaka huu kwa kutumia hekta 216,944 ambazo zipo chini ya Serikali za Vijiji, tumevuna na tunatarajia mwaka huu kupata Shilingi bilioni 11, fedha ambazo zinaenda kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vijiji vyetu wanaweza hata kuweka mipango ya kutengeneza mazingira ya kwao. Tunao msitu wa Tongwe Mashariki, tuna msitu wa Tongwe Magharibi, Serikali baada ya kuona tumefanya jitihada, sasa hivi wameanza vurugu za

kuwanyanganya misitu, naomba hili mkaliangalie. Halmashauri yangu inauwezo wa kupokea shilingi bilioni 30 kwa miezi sita na shilingi bilioni 30 nyingine kwa miezi sita. Tunaweza tusiitegemee Serikali Kuu kwa kiwango kikubwa sana. Naomba mkatatue migogoro mmalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia sana ni miradi ya barabara. Tunathamini kwamba Serikali imewekeza miradi mikubwa ya barabara na kwenye sekta ya ujenzi. Kwa bahati mbaya sana kwenye sekta ya ujenzi tumejenga barabara kilometa 14,641 ambazo ni za kiwango cha lami. Tuna kilometa 63,314 za changarawe. Mfuko wa barabara unahitaji shilingi trilioni mbili kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Barabara mpya ina mahitaji yasiyopungua shilingi trilioni mbili. Jumla ya kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi pekee kuna mahitaji yasiyopungua shilingi trilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ije na mkakati wa kuhakikisha tunatengeneza mifumo ambayo uwekezaji uliowekezwa na Serikali unakuwa endelevu. Barabara nyingi muda wake ulishaisha. Kwa sababu hiyo, mtaangalia. Mfuko wa Barabara unapata shilingi bilioni 850 kwa mwaka. Fedha zinazoenda kwenye matengenezo ni shilingi bilioni 600, sasa barabara tulizonazo hazitaweza kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Fedha, na Mheshimiwa Profesa Kitila, ambaye unashughulikia mipango, mwangalie hili. Mipango tuliyonayo ya kujenga barabara mpya zina uhitaji wa fedha nyingi, lazima tuje na mipango ya kutafuta fedha ambazo zitakuwa *ringfenced* hasa kwenye Mfuko wa Barabara wa *TANROADS* ambao fedha zake ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ninayoyazungumza kwa mwaka huu ambao tuna majanga ya mvua nyingi, barabara nyingi zitakatika na hata ile miradi tuliyonayo itashindwa kufanyiwa kazi. Eneo hili ni muhimu liende likafanyiwe kazi na Serikali ielekeze

mipango yake kwenye eneo hili ili tuweze kupata fedha ambazo zitasaidia miradi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo haya, kupata fedha ni lazima tuwe na eneo ambalo tutatengeneza mfumo wa *ringfencing*, fedha ambazo tutaziongezea nguvu ili barabara ziweze kujengeka, na mifano ipo. Barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa iliisha, barabara ya kutoka Mkoa wa Singida kwenda Tabora imeisha, barabara ya kutoka Tabora kwenda Mwanza muda wake ni kama ulishaisha na barabara ya kutoka Mbeya kwenda Kyela zimeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maeneo mengi kwenye nchi yetu barabara zimeharibika. Bila kufanya mkakati wa dharura, barabara zote nchini zitatoweka na uwekezaji uliopo utakwisha. Tunaishukuru Serikali imewekeza mradi mkubwa wa ujenzi wa reli. Reli haiwezi kwenda bila kuwa na barabara. Mifano ipo kwenye jimbo langu. Tumejenga bandari kubwa kwenye eneo la Karema. Bandari ile sasa hivi haifanyi kazi kwa sababu hatuna Barabara. Naomba haya wayafanyie kazi ili Serikali iweze kupata mifumo ambayo itawasaidia wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Waheshimiwa Mawaziri mpo hapa, *to get good government, you must have good men and women,* Mheshimiwa Kitila umesema juzi. Mpo vizuri na *you are capable*. Shilingi trilioni saba hizi alizozisema Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, ajira zitapatikana, mvua za kutosha, *food security* itakuwepo na nchi itakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtaturu, ajiandae Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami asubuhi ya leo niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ambao unakuwa umebakiza mwaka mmoja kufikisha miaka mitano ya Mpango wa Maendeleo ambao tuponao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kunijalia uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia Mpango huu wa Maendeleo. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hasssan kwa kuwa ameamua ku-*champion* maendeleo ya nchi yetu. Tumeona katika muda wa uongozi wake amefanya mambo makubwa sana. Hata leo tulivyokuwa tunasomewa mpango huu, tumeona namna ambavyo mwaka uliopita tumetekeleza baadhi ya mambo mengi na ambayo leo yanaonekana kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Tanzania yenye neema inawezekana, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, nasi kama Wabunge tunaendelea kumuunga mkono na Watanzania wanamuunga mkono. Hongera sana Mheshimiwa Rais. Wanasema wenyewe, kaza mwendo mambo mazuri yanakuja mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mipango, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa wasilisho lake, yeye pamoja na wataalamu wote. Kwa hakika nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kurudisha Tume ya Mipango. Tumeona mambo mazuri yaliyowekwa hapa, chombo hiki kilikuwa ni muhimu sana. Mheshimiwa Rais, kuonesha ana dhamira, basi amekirudisha kiweze kusaidia nchi yetu. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ndugu yangu Dkt. Mwigulu Nchemba, kwa namna ambavyo amewasilisha Mpango wa Bajeti ya mwaka unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwahi kusema lolote baada ya kuchaguliwa Mheshimiwa Spika kwenye Bunge la Dunia. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Spika wetu kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge ya Dunia. Kwa hakika ameiheshimisha Tanzania na tunampongeza sana na tunaendelea kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ninukuu maneno machache ya Hayati Mwalimu Nyerere. Wakati tunapata

Uhuru mwaka 1961, Mheshimiwa Baba wa Taifa alisema kwamba, ili tuweze kupata maendeleo tunahitaji mambo makuu manne; tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika watu tunao na kwenye sensa ya mwaka jana 2022 tumefikia milioni 61 kutoka milioni 44 tuliyokuwanayo. Ardhi tunayo mita za mraba 900,000 ambazo ni nyingi sana, ambapo nyingine ndani ni ardhi ya kilimo. Tatu tunao uongozi bora. Uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Chama Cha Mapinduzi, uongozi mzuri kabisa. Tunayo pia siasa safi ya CCM ambayo inaongoza na kutoa miongozo yote hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo manne ndiyo yanatupatia nguvu ya kusimama leo na kusema Tanzania ambayo leo tunajivunia imetokana na mipango mizuri kupitia nguzo hizi nne. Niseme wazi, kulingana na Mpango wa Taifa, umeeleza vizuri kwamba tutachochea uchumi shindani na shirikishi. Maana yake ni kwamba tunaenda kushirikisha watu. Watu ndio ambao wamebeba jambo hili, lakini watu hawa hawawezi kufanya peke yao, lazima wawe na rasilimali. Rasilimali mojawapo ni ardhi, ambayo kimsingi mimi nitajikita sana kwenye eneo la kilimo, kilimo ambacho kimebeba zaidi ya asilimia 80 ya watu wanaofanya shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka jana, 2022 nilichangia. Kwa sababu bado naamini, kilimo kikifanyiwa mapinduzi makubwa, kilimo kikiwekezwa vizuri, kilimo kikizingatiwa tukapata pembejeo, tukapata teknolojia, tukaweka mtaji, Maafisa Ugani wakawa ni wale waliyoandaliwa vizuri. Kilimo ndiyo kimebeba watu wengi, pia kilimo ndiyo kinategemewa kuleta malighafi kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote yaliyokuwa yanasemwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba tukifanya vizuri kwenye uzalishaji, tutaongeza uwezo wa Taifa katika kuchakata mazao kwenye viwanda, tutaweza kuuza nje na tutaweza kuleta

dola ambayo imekuwa inapungua katika nchi yetu. Hapa ukisikiliza hata maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba mauzo ya nje yalipungua kwa sababu mbalimbali. Yalipungua kwa sababu ya ukame, tabia ya nchi na mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwekeza vizuri katika sehemu ya uzalishaji wa mazao na kuongeza pembejeo za kilimo, kuongeza zana za kilimo za kisasa, na kama anavyosema matrekta na kadhalika. Mwaka jana, 2022 tuliletewa mpango wakuweza kupima udongo wetu katika maeneo mbalimbali. Ninaamini jambo hilo likifanywa vizuri, tukawa na uhakika pale tunapoenda kulima tutapata mazao kwa sababu tumejua aina ya udongo, tunataka kuongeza mbolea kiasi gani? Tukiongeza mazao ninaamini kabisa tutaweza kufanya vizuri na tutaongeza uzalishaji na mwisho wa siku tutakuwa na usalama wa chakula, lakini tutauza nje chakula na kuongeza malighafi kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kilimo cha kutegemea mvua. Kilimo hiki kimekuwa cha kubahatisha. Tulisikia kwenye Ripoti ya *CAG*, kuna baadhi ya Mkurugenzi wa halmashauri mmoja aliitwa akaja kueleza kwamba mwaka huu tulipunguza mapato kwa sababu hakukuwa na mvua. Maana yake ni kwamba hata mapato yanaathirika kwa sababu hatuna kilimo cha uhakika. Kwa hiyo, naomba sana *scheme* za umwagiliaji ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri, zitengewe fedha, zitengenezwe katika maeneo mbalimbali na tuwasaidie wakulima wetu waingie kwenye kilimo cha umwagiliaji waweze kuondokona na kilimo cha msimu, waweze kulima mara mbili au mara tatu kwa mwaka ili tuongeze uzalishaji wa kutosha, kwa sababu ardhi ninayosema tunayo ya kutosha na itaweza kutusaidia katika kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye wingi wa watu, asilimia zaidi ya 67 ni nguvu kazi ya vijana ambao wanaweza kwenda kazini. Tumeitumia vipi hii nguvu kazi? Ukiangalia katika nchi yetu, kwenye ikama ya watumishi katika nchi, hatufiki 700,000. Maana yake ni kwamba kuna kundi kubwa lipo nje ya mfumo rasmi

wa ajira, maana yake lazima Serikali iangalie nguvu kazi hii ambayo ipo iweze kutumika vizuri kwa ajili ya kuongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tukiuza nje, itatusaidia ku-*attract* dola kuja nchini. Itatusaidia katika manunuzi ya malighafi na vipuli mbalimbali kutoka nje, itatusaidia kuongeza uchumi wetu na kwa hakika itasaidia kuongeza uwezo wa kuzalisha katika nchi yetu na vipuli vitakuwa vinapatikana kwa haraka ili kuondokana na changamoto ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *populatio*n tuliyonayo ya Watanzania kuwa na uchumi wao, utakuwa kupitia shughuli za kilimo na kiuchumi watakuwa ni soko pia. Hao hao Watanzania ambao tunao, tukizalisha vizuri, tukaweza kutoa pamba kuwa nguo, itasaidia kuuzwa katika nchi yetu, tutageuka kuwa soko. Kwa sababu *population* pia ni uchumi. Tumeitumiaje *population* hii tuliyonayo ya watu zaidi ya milioni 61? Maana yake tukiwa na uwezo wa viwanda vyetu vikazalisha hapa hapa tutakuwa na uwezo wa kuuza nguo katika nchi yetu na itasaidia kuongeza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mwingine, madawa yakitengenezwa katika nchi yetu, maana yake tutakuwa tunanunua na fedha, tutanunua kwa shilingi na mwisho wa siku tutaweza kuuza nje na tutapata dola ambayo imekuwa ina changamoto. Kama haitoshi, tukiweza kukuza uchumi, tutaweza kuwa tumepambana na maadui watatu toka uhuru ambao ni ujinga, maradhi pamoja na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye upande wa miradi ya maendeleo, miundombinu au miradi ya kielelezo, tuna kazi nzuri tumeiona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, tutaenda kuongeza uwezo wa kujenga *SGR* ambayo inaendelea. Tutaenda kuongeza kuhakikisha vipande ambavyo vimebakia vinaenda kuongezwa, lakini kwenye hili tunaenda ku-*connect* kazi kubwa iliyofanywa juzi. Mheshimiwa Rais, kuruhusu ku-*sign* mkataba na *DP World* kwa ajili ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Itasaidia sana kuongeza kasi

ya mzigo ambayo itaongeza fedha. Fedha zile zikiongezeka, zitaenda kufanya kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba tunaenda kuleta jibu. Shilingi trilioni 47 ambayo imetajwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, itapatikana kupitia mapato haya ambayo tutaenda kuanza kufanya kazi na wawekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, ambayo tumeenda kuwekeza juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye taarifa yao kwamba tunaweza kuongeza kujenga kile kipande cha treni cha kutoka pale Tabora - Kigoma, Isaka – Rusumo, Rusumo - Kigali ambayo ni kilometa 495. Zaidi itatoka Uvinza – Msongati - Itega mpaka Burundi. Tukijenga reli hii, italeta matokeo makubwa sana. Itaenda kuleta jibu la kusafirisha mzigo ambao ulikuwa hatuufikii, utasaidia sana kuongeza uchumi, maana yake tutaendelea kuongeza fedha za kigeni kwa sababu tutapeleka mzigo mpaka nje ya nchi. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba mradi wa kielelzo huu utakuwa na majibu makubwa. Tunaomba sana jambo hili lifanyike vizuri ili tuweze kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, pamoja na yote tuliyoongea pamoja na barabara za kuunganisha mikoa na mikoa, naomba sana Serikali itafute fedha za kukamilisha miradi hii. Unaweza ukawa na mpango mzuri lakini huna fedha za kutekeleza, itakuwa ni kazi bure. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mipango katika miaka minne hii, tunaenda wa tano kumaliza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano; kama hatuna fedha, hatuna vyanzo vya kutosha, haitatusaidia chochote, tutabakia na mpango kwenye makaratasi. Naomba sana jambo hili tulifanye ikiwemo kwenda kuongeza uwezo wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika. *LNG* ya Lindi inalenga kuzalisha tani zaidi ya milioni tano. Ninaamini kabisa gesi hii ikitolewa kule ikaletwa katika matumizi ya wananchi, wengine wameenda zaidi wamesema hata magari yaanze kutumia gesi hii. Tutakuwa na uchumi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeendelea kuona kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais, alipokuwa Zambia juzi, amesema wanaweza kujenga hata bomba la gesi kupeleka kuuza Zambia. Ni kama ambavyo tulikuwa tumewapelekea bomba la mafuta. Ninaamini kabisa, tukifanya hivyo, uchumi wetu utakua, utaenda kufidia maeneo ambayo yamekuwa na changamoto ya mapato katika nchi yetu. Ninaamini kabisa mipango yetu hii ni mizuri tukiisimamia na kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni tathmini. Baada ya kuwa tumefanya Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja, turudi mezani na wataalam, tujitathmini; je, tulivyopanga mwaka jana, tumefika katika asilimia gani? Nini vilikuwa ni vikwazo? Nini ilikuwa changamoto? Kama Taifa tujitathmini na tupange vizuri wakati unaokuja. Siyo kila mwaka ukifika tunaandaa, halafu mwisho taarifa zinabaki kwenye makabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, narudia tena kuunga mkono. Naomba niwatakie kila la heri Mawaziri katika kutekeleza Mpango huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri.

Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Shukrani Elisha.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja iliyo mezani. kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuunda Wizara hii mahususi Ofisi ya Rais, inayosimamia masuala mazima ya Mipango na Uwekezaji pamoja na kuunda Tume ya Mipango na hali kadhalika nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii, pamoja na Lawrence Mafuru, naye kwa kuteuliwa na wote hawa wawili ni majembe na hakika wanatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tunapojadili Mpango wa Maendeleo ya Taifa, naamini ni muhimu sana kwa Serikali kuhakikisha ya kwamba Maendeleo haya ya Taifa yanatawanywa katika maeneo yote ya nchi yetu. Nasema hivi, kwa sababu ni kwa kufanya hivyo itapelekea Serikali kuweka mipango thabiti ambayo itatafuta nyenzo na njia mbalimbali za kuinua mikoa ambayo ipo kwenye hali ya umasikini ili nayo iweze kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kuchangia katika Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo hata Mheshimiwa Rais, ameshalisemea mara nyingi nakumbuka katika ziara yake ya kwanza alivyokuja Mkoa wa Kagera, alisema Mkoa wa Kagera kwa jiografia yake na kwa mambo mbalimbali iliyonayo haipaswi kuwa kati ya Mikoa ambayo inaongoza kwa umasikini nchini. Hivyo, alielekeza ifanyike tathmini mbalimbali na kuona namna ya kuhuisha kwenye Mipango ya Serikali ili mkoa huu pamoja na mikoa mingine inayofanana na hivi, iweze kuinuka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, haijaeleza wazi ni kwa namna gani ambavyo Serikali imejipanga kuweka mikakati thabiti ya kuinua uchumi wa Mikoa ambayo ina hali ya umasikini na haijaweka mipango thabiti ya kuona namna gani ambavyo itatawanya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka tu nitaendelea kujielekeza katika huu Mkoa wa Kagera na kwa upekee Mkoa wa Kagera unapakana nchi tatu za Afrika Mashariki kwa maana ya Rwanda, Burundi na Uganda. Mkoa huu wa Kagera ndio ambao tuna asilimia kubwa zaidi ya Ziwa Victoria. Mkoa wa Kagera tuna ranchi tano, Mkoa wa Kagera tuna ardhi yenye rutaba pamoja na mvua misimu miwili lakini bado inashangaza kwamba ni Mkoa ambao unaongoza kwa umasikini nchini. Tunaweza tukajiuliza ni kwanini ipo hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka tu, jambo la kwanza, tumeshindwa kuona namna ambavyo tutatumia maeneo yetu ya kimkakati ili yaweze kufungua uchumi wa Taifa letu. Mkoa wa Kagera unaweza ukawa na unapaswa uwe *international hub*, ya kuunganisha biashara ya Ukanda wa Afrika Mashariki kwa maana ya biashara kati ya Tanzania na Uganda, biashara kati ya Tanzania na Rwanda, biashara kati ya Tanzania na Burundi, ili kufanya hivyo tuhaitaji tuwe tuna *International Airport* jambo ambalo hatuna na haieleweki ni lini mpango huo utatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hatuna soko kuu la biashara za mazao ya kilimo, mifugo wala uvuvi. Jambo la tatu, hakuna mkakati thabiti wa kuona namna gani ambavyo zile *ranch* tano zitaweza kuwekewa mikakati ili kuchangia maendeleo. Jambo la nne, hatuna viwanda vya kutosha vya Samaki. Jambo la tano, fedha za misaada pamoja na miradi ya maendeleo kutoka kwa wadau wa maendeleo na Mashirika ya Kimataifa hayatawanywi ipasavyo katika nchi yetu. Unakuta ni maeneo machache ambayo ndio hayo hayo wadau wote wanakwenda ili hali Serikali inapaswa iweke jitihada makusudi kabisa ya kuhakikisha kwamba fursa zinatawanywa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la sita, japokuwa Mkoa wa Kagera ni mkoa wa sita kwa wingi wa watu bado Hospitali yetu ya Mkoa ni sawa sawa na Hospitali ya Wilaya. Hadi kufikia kwamba kwa hivi karibuni ni hadi miezi 18 iliyopita tu ndio tulipata vifaatiba kwa ajili ya watoto njiti kupitia jitihada zangu na kwa kushirikia na Shirika la *Dorice Mollel Foundation* ambalo leo hii takribani watoto 780, wameweza kuokolewa maisha yao. Hiyo inaonesha dhahiri kabisa Mkoa wa Kagera katika sekta ya afya bado tupo nyuma. Mkoa wa Kagera, ndio Mkoa ambao mara nyingi unapata kadhia mbalimbali inapotokea milipuko ya magonjwa lakini bado uwekezaji kwenye sekta ya afya kwa Mkoa wetu haujaridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine kwa haraka haraka hatuna Chuo Kikuu, wakati tungekuwa na Chuo Kikuu tungeweza kupata wanafunzi kutoka nchi ya Rwanda, tungeweza kupata

wanafunzi kutoka nchi ya Burundi, tungeweza kupata wanafunzi kutoka nchi ya Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Serikali ilipoandaa *SAGCOT*, *Southern Agricultural Growth Corridor* ya Tanzania, ilikuwa na lengo ya kuona namna gani ambavyo uwekezaji utafanyika, ili kuimairisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Dhamira ya Serikali ilikuwa ni baada ya miaka kadhaa Taasisi kama *SAGCOT* ianzishwe kwenye maeneo mengine ya nchi. Kwa zaidi ya miaka 10, bado hakuna mpango wowote ambao unaelekeza au unaonesha dira kwamba itaanzishwa *SAGCOT* nyingine wapi kwa mfano Mikoa ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili linaendelea kuchangia kupeleka maendeleo katika sehemu moja ya nchi, huku sehemu nyingine za nchi zikibaki nyuma. Hadi leo kuna Mkoa wa Kagera ni Mkoa ambao unaongoza kwa idadi halisi ya watoto wenye utapiamlo. Ukija Mkoa wa Kagera hutakuta mradi wowote wa maendeleo ambao unalenga kuusaidia Mkoa wa Kagera kupambana na mpango wa udumavu. Hali kadhalika inaonesha ni namna gani ambavyo tunashindwa kuhuisha malengo yetu ya maendeleo na maeneo yenye uhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwa upekee kabisa nimshukuru sana, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuleta Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Mahajat Fatma Mwasa, kama tunavyopenda kumwita sisi Kagera, pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa, Toba Nguvila, kwa sababu hawa wawili wamekuja na maono na nia ya dhati kabisa kuhakikisha ya kwamba wanaendeleza Mkoa wa Kagera, ili tutoke pale tulipo na tuende pale ambapo tunastahili kuwa ili nasi kama Mkoa tuchangie maendeleo ya Taifa lakini pia tuchangie katika pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, noamba nihitimishe kwa kumuomba sana Mheshimiwa Waziri Prof. Kitila Mkumbo, utakapohitimisha hoja hii utueleze bayana ni namna gani ambavyo utahakikisha ya

kwamba Mpango wa Maendeleo wa Taifa unakuwa ni Mpango wa Maendeleo ya Taifa, kwa vitendo sivyo ilivyo hivi sasa, kwamba huu ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa maeneo baadhi ya Taifa letu. Huku ukiacha maeneo mengine nyuma kama ilivyo Mkoa wa Kagera pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Prof. Kitila Mkumbo tutendee haki Mkoa wa Kagera pamoja na Mikoa Mingine ambayo ina changamoto kama ya Mkoa wetu wa Kagera na kwa kufanya hivyo ndivyo kwa nadharia ya dhati kabisa tutaweza kusema kwamba sasa tuna Mpango wa Maendeleo wa Taifa kinyume na ilivyo hivi sasa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mpina, ajiandae Prof. Shukrani.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na niweze kuchangia katika haya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri na Waziri wa Mipango kwa ile kauli mbiu yake, kwamba hii mipango inayoanza sasa hivi na itakayokuja baadaye itakuwa na lengo la kuhakikisha, kwamba kuna ukuaji wa uchumi jumuishi lakini kutakuwa na kupunguza umasikini kuzalisha ajira nyinyi kutengeneza matajiri. Vilevile, kuongeza mauzo ya nje yaliyoongezwa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hii ndio kweli dhamira yetu, basi inatubidi tubadilike mno, kwa sababu haya yote mengi tunayoyafanya ni kinyume chake, kwa sababu hizi *item* zote nilizozitaja tunafanya kinyume chake badala ya *facilitate* tunarudisha nyuma. Sasa kama kweli tuna dhamira hiyo basi inatubidi tubadilike sana kifikra tubadilike sana kimtazamo na kuweka mikakati madhubuti itakayotuwezesha kufika hapa. Vinginevyo tutaendelea kuwa na kauli nzuri bila matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya ninajua, kwa mfano hivi sasa katika ulinzi wa ajira na ulinzi wa viwanda hapa nchini hakuna. Viwanda vyetu havina ulinzi, ajira hazina ulinzi. Ndio maana ajira nyingi wanapewa wageni makampuni mengi ya kigeni ndio yanapewa kazi na makampuni ya ndani yananyimwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano leo *TANESCO* na *REA* wanaagiza vifaa vya umeme kutoka nje ya nchi licha ya baadhi ya viwanda vipo hapa vinavyotengeneza vifaa hivyo vya umeme wanavyovihitaji, lakini vinaagizwa nje ya nchi makampuni yanayojenga miradi ya *REA* yanaagiza vifaa kutoka nje ya nchi na bila hata sababu zozote za msingi. Hata hivyo, tuna kiwanda kikubwa pale kwa mfano *Esther by Science African Limited* cha uzalishakji mkubwa wa chanjo lakini bado chanjo nchi hii nyingi kwa sehemu kubwa zinaunuliwa nje ya nchi. Viwanda vya viwatilifu navyo tunanunua nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafanyika unasema unalinda ajira, unailindaje lakini leo hii bado tunatengeneza na kutumia TEHAMA ya kutoka nje ya nchi licha ya uwezo mkubwa tulionao Mfumo wa *ITS,* Mfumo wa *TANESCO* unaojengwa. Vijana tunao waliobobea vizuri tuna Mkongo wa Taifa leo unaenda ku-*hire* Mfumo wa TEHAMA kutoka nje ya nchi ili ufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa udhaifu huu hatuwezi kupiga hatua wala hatuwezi kufika malengo tunayotarajia. Upande wa kilimo upande wa kilimo mbegu kuchelewa lakini mbegu zenyewe pia ukikuta mbegu bora za kisasa za mahindi mfuko mmoja unauzwa shilingi 22,000/=, 24,000/= maana yake kilo moja inauzwa elfu 12,000/= kilo moja ya mahindi ya kawaida inauzwa 600? Hao wanaoratibu bei za mbegu wanazitoa wapi hizi bei? *TARI* mko wapi? *TOSCI* mko wapi? *ASA* mko wapi? Hizi bei zimeruhusiwaje wananchi mbegu siyo gharama pekee katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata upande wa mifugo upande wa mifugo sasa hivi unataka mabadiliko haya ufikie haya malengo. Wafugaji wanakamatwa ng'ombe, ng'ombe mmoja

anapigwa faini ya shilingi 100,000 isiyokuwemo kwenye sheria ng'ombe zinakamatwa kiholela tumeshafikisha malalamiko kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuna hatua inachukuliwa. Sasa unasema unatajirisha watu Serikali inashiriki kufirisi wananchi halafu inasema inaenda kutajirisha watu. Haya mambo tulishayalalamikia unayaleta hapa Waziri wa Maliasili, anajibu kwamba nendeni Mahakamani halafu unasema kwamba unaweza ukatajirisha wananchi wako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye suala la ufadhili wa miradi yetu, tunaifadhilije miradi yetu.? Lazima tujiulize kwa mfano *SGR* sababu ya leo *lot three* bado kuwa asilimia 12 ni nini? sababu ya *lot four*, kuwa asilimia tano mpaka sasa hivi ni nini? Miaka miwili mitatu ya mkataba wana asilimia tano. *lot six* yenyewe ni 0.29. Ufadhili wa miradi wa miradi ukoje? miradi *EPC+F* jana hapa tumezungumza miradi ya *EPC +F* leo miezi sita mkataba umesainiwa hakuna mjenzi miradi haijaanza kutekelezwa miezi sita, tatizo liko wapi? Tuliambiwa kwamba hawa wakandarasi wana hela. Sasa mliwekaje mkandarasi ambaye hana pesa na mkatuambia kwamba wao wana pesa watajenga mpaka kukamilisha miradi mpaka sasa hivi miradi haitekelezwi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mpina kwamba kwenye upande wa miradi ya *EPC+F, TANROADS* wali-*design* lakini kimkataba inabidi hawa *engineering, procurement* na *construction* nao wafanye *preliminary design* kabla ya ujenzi kuanza na hilo ndio zoezi linaloendelea hivi sasa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mpina, taarifa unaikubali?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na taarifa yake. Mheshimiwa Waziri atulize vizuri kichwa katika hili suala la *EPC+ F,* yeye amelikuta, suala kama unasema hawakufanya *design* walizipataje gharama za ujenzi? Kama hakufanya *design from the early beginning*. Umesema kwamba ufanya *engineering*, utafanya *construction,* utafanya *procurement* utafanya *financing* ulizipataje gharama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili dubwasha la *EPC+F* linatupeleka kubaya, kwanza ni suala ambalo liliingia kinyume hata na Sheria zetu za Manunuzi zilizopo hapa nchi. Mikataba inayoingia nchi tumekiri kwamba tumefanya upekuzi wa mikataba, tumefanya upekuzi wa wa mikataba yetu tunayoingia yenye thamani ya shilingi trilioni 91. Toka tuiombe Serikali kuleta mikataba hiyo hapa Bunge imeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali imeshindwa kuleta hiyo orodha ya hiyo mikataba? Tunapanga mipango pamoja ikifika kwenye mikataba hata kujua tu mikataba ya trilioni 91 hiyo ipo wapi? Nayo imekuwa tatizo. Pili, Serikali imeenda kuingia mikataba 43, kati ya mikataba hiyo kuna mikataba ya rasilimali na maliasili za nchi, ambayo nayo imeingiwa. Sheria yetu ya maliasili za nchi ile *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty* inataka lazima hiyo mkataba iletwe Bunge hiyo mikataba 43 iliingiwa haijaletwa Bunge. Sasa hivi mpaka tunapozungumza haijaletwa Bunge kwa nini Serikali inafanya siri kubwa katika hili jambo kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *NLG,* suala la *NLG* nalo tunaambiwa mikataba ipo hatua za mwisho lakini *PSA* zilikuwa zinatakiwa kufanyiwa marekebisho tumeambiwa hapa zimefanyiwa marekebisho kupitia mlango gani? Marekebisho hayo yamefanywa na nani? Ushirikishwaji wa wananchi katika kurekebisha zile *PSA* wameshirikishwa wapi *GN* iliyotangaza *PSA*. Mnafikiaje hatua ya kukamilisha majadiliano ya mikataba mikubwa ya *NLG* bila ya kulishirikisha Bunge kama inavyotaka Sheria ya *Natural Resources* na kama inavyotaka Sheria ya *VAT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Bandari wa *PTA* na *DP world*, mpaka sasa hivi Waziri ameongea kwenye *para* yake ya 35, ameshindwa kutueleza huyu *DP World* anaenda kuwekeza kiasi gani? Anaenda kuwekeza kwenye maeneo gani? Kuna shida gani? Kama tathmini imeshafanyika na mkataba umeshaingiwa kuna shida gani ya kutueleza kwamba huyo *DP World,* anaenda kuwekeza kiasi gani na tathmini imefanywa na nani ya kuthibitisha mahitaji ya uwekezaji tunaoutaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwanini hii mikataba imeshakwisha kuingiwa Bunge ndio hili, kwa nini haijaletwa Bungeni mpaka sasa hivi Mikataba ya *DP World*. Lingine ni Suala la huduma za nishati ya umeme, suala la huduma ya umeme *EWURA* ni jukumu lake la kufanya *compliance audit* ili kuthibitisha kwamba gharama wanazotozwa wananchi ni sawasawa kwenye umeme? Gharama wanazotiozwa kwenya mafuta ni sawasawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza mpango kama huu utauwezesha, wananchi wanakatiwa umeme, viwanda havizalishi, watu hawafanyi biashara. Ukataji wa umeme mara kwa mara usiyokuwa na majibu na majibu yanayopinzana kila leo na hakuna mamlaka iliyotoa majibu ya kisanyansi kwanini tukatie umeme? Bei za mafuta zinavyopanda kila siku zinapanda bei za mafuta mara unaambiwa Vita vya Ukraine, hakuna maelezo hakuna ukaguzi wa gati uliofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba ni jukumu la *EWURA* ku-*conduct compliance audit* ambayo ita-*reveal* kwamba je, kweli bei ya mafuta tunayotozwa sasa hivi na wauzaji wa mafuta ni sahihi. Je, ukataji wa umeme mara kwa mara unaozunguzwa sasa hivi ni sahihi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa Mpina hiyo. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha. Ajiandae Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuunda na kuirejesha tena Tume ya Mipango ili kuweza kupanga Mipango ya Maendeleo ya Nchi katika ngazi ya Taifa na Tume hii ikiwa ni Ofisini kwake mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu nikuwa uwepo wa Tume ya Mipango, kwanza, utaondoa *duplication of effort* jambo moja kufanywa na Wizara au Taasisi mbalimbali za Serikali na hivyo kuokoa fedha nyingi za miradi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, matarajio yetu ya kuwepo Tume ya Mipango ni kwamba mtapanga maendeleo ya nchi kwa kuangalia *geographical* na *ecological advantage* ya eneo husika kama amabvyo Wabunge wenzangu wamesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba Mpango utakapo kuja mwezi wa tatu maana sasa hivi ni mapendekezo. Nakuomba sana rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila, uzungumze bayana jinsi ambavyo umetumia matokeo ya Sensa ya mwaka jana katika kupanga mipango. Yaani tusifanye kazi kubwa ya Sensa ambayo tuliiona kwamba ni *digital* Sensa ya maana. Inapokuja kwenye kupanga Mpango wa Taifa haizungumzwi mahali popote kwamba imetumika vipi. Kwa hiyo, hilo lije bayana katika maelezo yako unakuwa unapanga Mpango wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja zangu siku ya leo kwanza niongelee kitu kinaitwa Dridi ya Taifa ya Maji. Jambo hili Mheshimiwa Prof. Kitila, mwenyewe ni muasisi alipokuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Maji. Kwa nini tuzungumzie Gridi ya Taifa ya Maji?

Kwanza, itumie vyanzo vya kuaminika vya maji. Kwa nini jambo hili liendelee kuwa nadhari ya kwamba Tanzania ina Ziwa Tanganyika kama Ziwa la pili lenye kina kirefu Duniani lakini wakati wote hatuliingizi katika Mpango wa Kuchota Maji katika chanzo

hicho ambacho tunajua hakiwezi kukauka huwezi ukakausha Ziwa ambalo ni kina kirefu cha pili duniani. Kwa nini hatuendi huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunapokuwa tunaangalia miradi mikuwa ya maji, bado tunaona Wizara ya Maji inajihusisha na matumizi ya majumbani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunaangalia miradi mikuBwa ya maji, bado tunaona Wizara ya Maji inajihusisha na matumizi ya majumbani zaidi. Ningependa Waziri wa Mji, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Mifugo, Waziri wa Mifugo asiende kutafuta malambo kwa ajili ya mifugo halafu, Waziri wa Kilimo asiende kutafuta *scheme* peke yake, hawa watu wakae pamoja ili tuweze ku-*consolidate efforts*. Tunapoongelea mradi mkubwa wa maji, uangalie mambo yote hayo. Tunywe majumbani, tupate *scheme* za umwagiliaji na mifugo. Tutatue jambo moja linalohusu maji kuliko ambapo sasa hivi *efforts* ni kila Wizara kujaribu kutatua hoja yake binafsi. Tukifanya hivyo kwa *consolidated efforts* kutoka Tume ya Mipango tutaokoa gharama nyingi na tutakuta tunapata tija katika miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hoja yangu katika habari ya matumizi ya maji ipo hivi, mwaka jana Ziwa Victoria lilikuwa linafurika zaidi ya mita mbili juu, lakini wakazi kandokando ya Ziwa Victoria hawajapewa mwongozo, bado wanasubiri *scheme* ya kutoka Wizara ya Mheshimiwa Bashe eti waweze kulima kilimo cha umwagiliaji. *Why should that happen?* Yaani kwa nini, hawa wakazi wanaozunguka maeneo ya vyanzo vikubwa vya maji wasipewe mwongozo wa namna ya kutumia maji bila kuathiri mazingira ili waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili ni jambo ambalo tunapaswa kulipanga vyema kama Taifa ili *private sector* iingie, wasisubiri Serikali kila wakati kujenga *scheme* wakati chanzo cha maji kipo hapo, anahitaji *water pump* lakini na kuangalia namna ambayo hawatafanya *siltation* kubwa katika ziwa. Wapewe

mwongozo ili watu wafanye kilimo cha umwagiliaji bila kusubiri Serikali kuwajengea *scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni mapendekezo ya mpango, yamechukua miradi ya siku nyingi ambayo mingi ya hiyo miradi pia haijaanza na mfano wa hapa ni Liganga na Mchuchuma. Vita ya Urusi na Ukraine ilisababisha mahitaji ya nishati Ulaya kuwa makubwa na; hivyo lile pendekezo la kutotumia makaa ya mawe duniani wakati fulani ukifika liweze kurejeshwa na makaa ya mawe ya hapa nchini yaweze kupata soko Ulaya. Sasa Mchuchuma tuna tani 536 milioni za makaa ya mawe, ambayo yameendelea kuwa ni *laughing stock* yaani yameendelea kuwepo hapo kila mwaka mpango huu unafaulishwa kutoka mwaka huu kutoka mwaka huu, tunaendelea kusoma Liganga na Mchuchuma na Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukajikuta kwamba tuliendelea kuisema Liganga na Mchuchuma lakini ikaja kuwa ni *lost opportunity,* kwa maana ya kwamba, *resource* ilikuwepo hapo lakini tulichelewa kuchukua maamuzi. Napenda kuamini kwamba, vikwazo vinavyoongelewa katika mradi huu vipo katika utashi wa kimaamuzi wa Serikali kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mwezi Machi Mpango utakapokuwa unasemwa, Serikali ije na jibu la ni lini mkakati huu wa kuanza Liganga na Mchuchuma unaanza sio habari ya kuendelea kuifaulisha kutoka mwaka hadi mwaka, iseme tarehe ya kuanza mradi; hiyo itatupa amani. Tunaelewa fidia imeshafanywa lakini katika mpango tuje na *when, deadline* ya kuanza kuchukua hii *resource*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kuongelea ambayo pia ni *opportunity* nyingine, ni *opportunity* ambayo Tanzania sasa ipo katika ukingo wa kupata manufaa ya uchimbaji madini au kupoteza *opportunity*. Hii ni kwa sababu, tunapenda kusimuliana habari za uchimbaji wa *nickel* pamoja na uchimbaji wa *graphite* kama *materials* za kutengeneza *battery*. Sasa

ni kweli kwamba Makamu wa Rais wa Marekani alipokuja alituahidi kiwanda, naomba hapa tuwe *very strategical*. Kwa nini? Makampuni ya madini siku zote yana *offtake agreements, offtake agreements* ni kwamba nachimba ili nikuuzie kwa sababu yawezekana wewe ndiye uliye-*finance* mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukajikuta pamoja na kwamba wanachimba hapa bado *offtake agreements* zikalazimisha madini haya yaende kwa aliye-*finance* mradi, *so it should be a strategic thinking* hapa, kwamba, tunapotarajia kuwa na kiwanda cha *battery* hapa lazima twende tukaongee tena na kuwashawishi wenye kuchimba kwamba, bwana sehemu ya *raw materials* hii; tunapotaka kuanzisha kiwanda hapa itabaki hapa na sio kila kitu kitapelekwa kwa hawa ambao tayari wana mikataba nao.

Kwa hiyo, hapa sio habari ya kuandika, tufuatilie ahadi ya Makamu wa Rais wa Marekani kutujengea Kiwanda cha *Battery* lakini *we have to be strategical* kuona kwamba hawa wanaochimba bado wasiwe na *concession* za kupeleka kwa *offtakers* tuwe na *raw materials* ili tuweze kufanya hivyo. La sivyo tutaendelea kuchimba madini kama *raw materials* za viwanda vya Asia pamoja na Europe na tukadhani kwamba tunapata faida kumbe tunapoteza *opportunity* ya kuajiri watu wetu katika mnyororo mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba Mpango utakapokuja uendelee kutamka wazi wazi, tulianza mwaka jana kwamba lazima Benki Kuu inunue dhahabu na tukasema mwaka jana inanunua tani sita. Mpango unapokuja mwezi Machi useme wazi wazi kwamba mwakani tunanunua tani ngapi ili tuendelee kuwa na *vault* yetu ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Francis Mtinga, wajiandae Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo katika mpango ambao utaiongoza nchi yetu katika malengo ya nchi ya asali na maziwa ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vijana hawa japo ni watu wazima, lakini kwenye siasa bado hawa ni vijana, ambao wamekuja na mpango mzuri kabisa wa kuisaidia nchi yetu kusogea mbele na kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu ambaye anapambana usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanakuwa na maisha mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nijikite kwenye rasilimali ambazo tunazo, ambazo Mwenyezi Mungu ametusaidia tunazo mpaka sasa, lakini nahisi kama hatujazitumia vizuri katika kubadilisha maisha ya Watanzania. Rasilimali mojawapo kubwa ni gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia Mpango uliopita na nataka nichangie tena na nitaendelea kupiga kelele mpaka siku nitakapoona mabomba ya gesi yanaanza kutandikwa kutoka Dar es Salaam kuelekea katikati ya nchi na hatimaye kwenda mpaka magharibi, mashariki na kusini mwa nchi. Gesi tayari tunayo nyingi, *reserve* ya gesi ni kubwa na bado inaendelea kugunduliwa na tayari tumeshaitoa huko kwenye *source* tumeifikisha mpaka Dar es Salaam. Gesi hii inaweza kusaidi kupunguza matumizi mengi sana ya mafuta ambayo yapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile gesi hii inaweza kulinda mazingira. Sasa sijaona kwenye Mpango kauli yenye nguvu ikionesha kwamba tuna nia ya kusambaza gesi hii kwa Watanzania, kutoa bomba Dar es Salaam kulifikisha mpaka Mwanza ambapo litapita huku pote ili wananchi waweze kuitumia hii gesi kwenye majumba yao kama tunavyotumia maji, lakini vile vile tuweze

kutumia kwenye magari jambo ambalo litaokoa fedha nyingi sana za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo moja ya gesi ni Sh.1,500 na inakwenda klilometa nyingi kuliko lita moja ambayo ni Sh.3,500 kwa hapa ya *petrol* au ya *diesel*. Kilometa za lita moja ni chache ukilinganisha na kilometa za kilo moja ya gesi ambayo ni Sh.1,500. Kwa hiyo, kwanza fedha za wananchi utakuwa umeziokoa kiasi cha kutosha, lakini sijaona kwenye Mpango u-*seriousness* katika kuhakikisha tunalisambaza hili bomba ili tutumie hii gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu yangu Mheshimiwa Kitila, Mheshimiwa Waziri, alipokuwa hapa kwenye hiki kiti alikuwa anatoa kweli kweli mambo ya *material* mipango mikubwa mpaka mama akamwona akaamua ampe mwenyewe kisu ashikilie; hebu alitazame hili litaokoa sana maisha ya Watanzania. Gesi tayari tunayo hebu aweke kwenye mipango ya kutosha kuhakikisha tunaisambaza hii gesi inakuja huku ili tuitumie kwenye magari, majumba, tuokoe mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia mtu anachangia hapa kupata hela za ukaa. Sasa hii itaokoa miti haitakatwa, wananchi watatumia gesi, miti itaongezeka tutapata fedha kwenye ukaa. Nimwombe sana Waziri anapokuja ku-*wind up,* akae na timu yake waangalie jinsi gani wanaingiza hili suala la kusambaza bomba la gesi kutoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza ili wananchi waweze kutumia. Nimekaa muda mrefu hapo kwa uchungu ili angalau ushike kalamu, nashukuru sasa hivi umeishika ili uweze ku-*note* hilo jambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la maji. Maji ni muhimu sana kwa kila kitu na amesema msemaji aliyepita hapa. Mheshimiwa Waziri alipokuwa Katibu Mkuu wa Maji alikuwa na mpango wa kuleta maji Dodoma kutoka Ziwa Victoria; na alikuwa ayapitishie njia ya Sibiti ambayo ingepita kwenye Jimbo langu la Mkalama ingeingia Singida tena kwa *gravity* kutoka pale Kisana, Singida mpaka Dodoma maji yanakuja kwa *gravite*. Hebu naomba,

wakati huo alikuwa Katibu Mkuu leo ndiyo Waziri wa Mipango; aweke hili jambo kwenye Mpango, maji yatoke Ziwa Victoria yaje mpaka Dodoma huko kote njiani wananchi watapata maji, mifugo itapata maji, tutamwagilia mabonde na ni *source* ambayo haitakaa iishe mpaka dunia hii itaondoka, lakini hiyo *source* ya Ziwa Victoria haitaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimwombe sana, ule mpango wake wakati alipokuwa Katibu Mkuu aende akafungue mafaili aingize sasa kwenye Mpango wa Taifa ili tupate maji kutoka Mwanza kupitia Singida kuja Dodoma na nchi yetu iweze kupona kwa kiasi kikubwa kwa *source* ya uhakika; na tutaokoa fedha nyingi za visima na kadhalika. Yote yanaisha kwa suala hili moja tu na maji kule yalishakuwa tayari ni kiasi tu cha kuyasogeza. Nimwombe sana aliingize hili kwenye Mpango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Mipango ni profesa, mipango yote hii inataka elimu nzuri kwa vijana wetu wa Tanzania. Elimu ikiwa hovyo hii mipango haitafanyika. Katika suala la elimu nasikitika sana, tuna *TCU* inashughulikia suala la elimu ya juu *degree, PhD* na kuendelea, lakini tuna *NACTE* kwenye vyuo vya kati, hapa palikuwa na vurugu. *NACTE* inashughulikia vyuo vya kati, lakini hivyo vyuo vya kati sasa vinatoa *degree*, unakuta chuo cha kati kama cha *CBE* kinatoa *degree* wakati msimamizi wa *degree* ni *TCU*, sasa hapa mbona kuna vurugu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama chuo ni cha kati tunataka tupate mafundi na nini, visimamiwe na hiyo *NACTE* na iishie kwenye *level* yake. Vyuo vyote vya *degree* visimamiwe na *TCU;* huu mvurugano huu umesababisha, halafu kitu kingine kibaya sana, wameviachia vyuo kwamba zile ada wazitumie kwenye mipango yao ya kupanua vyuo na vitu vingine. Matokeo yake vyuo vime-*concetrate* kuhakikisha vinaanzisha kila aina ya program ili vipate wanafunzi wengi. Leo Chuo cha Ardhi kinafundisha uhasibu, *CBE* kinafundisha *Human Resource* sasa hii…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, karibu.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa anayechangia sasa, kimsingi anachokisema ni sahihi kabisa. Kuna vyuo kama *Mbeya University of Science and Technology* wakati huo kilikuwa kinaitwa *Mbeya Tech,* kilikuwa kinatoa vijana wenye maarifa na ujuzi, leo hii baada ya kupanda hadhi kuwa chuo kikuu vijana wenye ujuzi na maarifa hawapo na tukumbuke elimu ya chuo kikuu inamuandaa kijana kuwa na maarifa na sio ujuzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taarifa hiyo.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea. Leo *Sokoine University* chuo nilikosoma mimi eti wanafundisha ualimu! Sasa haya mambo yanakuwaje? Mheshimiwa Waziri kwa kuwa yeye ni Profesa wa Chuo Kikuu kwenye Mipango yake hivi vitu visimamiwe inavyotakiwa. Kila kimoja kisimamiwe kwa utaratibu wake ili mambo yaende vizuri. Hii habari ya kuwaachia vyuo ili eti wakusanye ada wazitumie ndiyo inakotupeka. Leo unaenda kwenye vyuo, wanafunzi wamesimama hakuna hata darasa, leo hakuna cha *supplementary* wala hakuna cha ku-*disco*, wanajua huyu akifanyiwa *disqualification,* anapoteza ada, matokeo yake tunapata vijana wa hovyo, yaani kama mwalimu ni mkali mkali…

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis kuna Taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpe Taarifa mzungumzaji kwamba, hayo masuala wakati mwingine inabidi tuyachunguze zaidi kwa nini inafikia hivyo. Mfano, kwa hawa wanafunzi tunaohitaji wa vyuo vya

ufundi wasipoweza kupata Walimu maalum wanaohusika na masuala ya ufundi kupitia vyuo hivyo vikuu vya ufundi kunakuwa na changamoto kubwa ya kuwa na Walimu wa kuwafundisha watu wa aina hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Taarifa hiyo.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaelewa vizuri ila nalipokea kwa sababu yule ni mama yangu. Leo hii Mwalimu akiwa mkali anasababisha watoto wana-*disco* au wanapata *supplementary,* chuo kinamwalia macho mawili kwamba wewe unataka kutupotezea wanafunzi kwa sababu wanaitaka hiyo ada. Niombe Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango hivi vyuo hela itoke Hazina kule, ada zote zikusanywe kama zamani ili kila chuo kifanye kazi kwa *discipline*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatuharibia tunapata vijana ambao wanakuwa wana uwezo mdogo kwa sababu ya kukusanya ada. Hii imesababisha hata polisi wameachiwa eti zile hela wanazokusanya ndiyo zijenge vituo. Matokeo yake kila Polisi ana *POS,* makosa yanalazimishwa, wananchi wanaumia. Hii yote ni kwa sababu mtu anaangalia tu amepewa *target* akusanye ngapi? Hii yote kwa sababu ya kuachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda *LATRA,* faini ya *LATRA* mtu amekosa kidogo, kwa sababu tu ile hela wanaitumia wao faini ina-*double* mwaka mzima yaani kila faini inaongezeka kila mwezi, matokeo yake mamlaka ni nzuri, tunazitaka zisaidie wananchi, zinawaumiza kwa sababu tozo hizi zinaachiwa zitumike huko. Naomba mipango itumike, hela zote zikusanywe Hazina watu, wapewe fedha kwa ajili ya matumizi ili wache kuumiza wananchi na matokeo yake tunapata vitu ambavyo havina *quality*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimalizie kwa kusema, mipango yote hii elimu na kila kitu bila miundombinu haiendi vizuri. Pale Singida ndugu yangu Waziri wa Fedha hatujaunganishwa na Simiyu ambapo inatoka pamba, tunatumia vumbi, bado kule Itigi

hatujaunganishwa na sisi ndiyo mkoa wa katikati. Naomba wamalizie hizi barabara muhimu kama hii ya Singida kwenda kule Simiyu, pamba inatoka huko; ili na sisi tuweze kufaidi uchumi wa hii nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kengele imelia ila hizi taarifa ndugu zangu nasubiri na nyinyi mchangie maana mnatukatia *floor* halafu matokeo yake muda hautoshi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, wajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Bonna.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie. Kwanza niwapongeze Mawaziri wawili, nawaamini sana wote wanafanya kazi nzuri na wasaidizi wao, ila nilikuwa najiuliza kati ya Mheshimiwa Kitila na Mheshimiwa Mwigulu mkubwa ni nani? Nani anamwelekeza mwingine, nikajua kumbe Mheshimiwa Kitila hana fedha, lakini ana mamlaka ya kumwelekeza Mheshimiwa Mwigulu afanye kazi za mipango. Tunaamini sana kwa kazi waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametupa utulivu wa nchi na tunaendelea vizuri. Nianze kwa kuangalia vyanzo vya mapato tulivyonavyo tuvilinde au tutafute vipya? Mgogoro wa nchi zote za Afrika hasa nchi changa tatizo lake lipo kulinda mapato ya nchi zao na Tanzania ni mojawapo. Nimemwona hapo Mheshimiwa Ole-Sendeka anateseka, Mheshimiwa Mpina anateseka. Mambo yote tunayoyaona ni ulinzi mbaya wa vyanzo vya mapato na mapato yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukilinda fedha tulizonazo zinaweza kutupeleka mbali zaidi, kwa hiyo mipango tunayopanga iende kwenye mifumo, mifumo ambayo tutahakikisha kwamba fedha zetu tunazozikusanya zinalindwa vizuri. Tatizo lipo hapo, tatizo lipo kwenye kula hela; tatizo lipo kwenye ubadhirifu. Tukilinda vyanzo vyetu na mapato yetu fedha yetu itafanya kazi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba mipango yetu ijielekeze kwenye mifumo, kuna kitu kinaitwa *POS*,

ugonjwa wa kuficha hela za Watanzania. Kwa hiyo tuangalie *POS* inafanyaje, tuirekebishe, tufanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia miundombinu ya shule za msingi, sijui Wabunge wenzangu wanakaaje. Majengo ya shule za msingi madarasa yamechoka mno, vyumba vya madarasa vimechoka sana lakini nyumba za Walimu wapo porini hawana mahali pa kupanga; hakuna nyumba za Walimu. Leo katika maeneo yetu mengi madawati hayapo, lakini tunazungumza hapa vyanzo vya mapato na wakati mwingine fedha zetu zinapotea wakati watoto wetu wanakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Kitila waliangalie. Nilikuwa napiga hesabu, kupata madawati ya watoto ni shilingi bilioni 150, tunashindwa nini kupata shilingi bilioni 150 watoto wote wakae kwenye madawati bora yaliyotengenezwa, wakasoma vizuri. Kwenye Jimbo langu juzi Mwalimu mmoja amesimamishwa hana madawati, akaenda kukodi viti, akasema viti havikaliwi. Shida sana. Wanamtoa madaraka kwa kukosa madawati, atafanyaje Mwalimu. Tumekuja na kauli nzuri hapa tunasema kwamba wananchi wasichangie, lakini wananchi hao sasa miundombinu yetu sasa imechoka; na tukiwaambia kuchangia hawachangii. Niombe sana kwenye upande wa miundombinu ya shule za msingi tuangalie mno kwa sababu hali ni mbaya sana kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza maswali mengi sana, nchi yetu ina bei elekezi ya pamba; lakini nchi yetu haina bei elekezi ya dawa za mwanadamu; dawa za wanadamu zimekuwa na bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda hospitali kuna dawa nyingine za wanadamu ni laki sita, laki nane, laki tatu. Sasa niwaombe mipango mingine inayokuja ya Waziri wa Afya na mipango mingine muipange kwamba, huko tunakokwenda kuwe na bei elekezi za madawa ya binadamu. Tunakuwaje na bei elekezi ya pamba, tusiwe na bei elekezi ya dawa za binadamu wakati

ndiyo afya yenyewe tunaitunza? Hali ni mbaya sana kwenye madawa, bei ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda India na laki sita, unatibiwa kila kitu. Ukienda Tanzania hiyo ni ya dawa mbili tu. Kwa hiyo, tuombe huko tunakokwenda mipango yetu ielekee kwenye kupunguza bei za dawa za wanadamu itatusaidia sana kuweka hii hali iwe sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa kwenye maeneo mbalimbali, nije kwenye Mkoa wangu wa Mara, Mkoa wa Mara mpaka tunajiuliza hivi tulipata laana gani sasa au kutoa Rais ndiyo ilikuwa shida. Kwa sababu huko nyuma tulikuwa na bandari inafanya kazi, imekufa, huko nyuma tulikuwa na uwanja wa ndege mzuri, haupo sasa ni shida. Huko nyuma kulikuwa na mpango wa reli ya kutoka Moshi – Arusha kuja Musoma, mipango imeishia katikati, haipo! Huko nyuma tulikuwa na mpango wa kuweka maji katika maeneo yetu, tumeahidiwa maji, mimi mwenyewe nimeahidiwa ingawaja nina imani kwamba nitapata lakini bado na huu ni mwaka wa saba sasa! Tumezungukwa na Ziwa, leo tunaambiwa kwamba maji yanatoka Ziwa Victoria kuja Dodoma!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnatupa kazi ngumu sana Wabunge wa Mkoa wa Mara, ngumu sana, ngumu sana. Yaani sisi tuna maji kilometa 40, kilometa 20 maji hayapo, yanaletwa kilometa 3,000! Mnatupa kazi ngumu sana. Kwa hiyo, mnavyopanga mipango hiyo muangalie kwamba ni kipi bora, kuwasaidia walioko hapo karibu na baadae kwenda mbali, mnatupa kazi ngumu mno. Tunasema nini kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba hilo nalo ni jambo la kuangalia. Maeneo mengi Mkoa wa Mara tunatoa uchumi mkubwa sana. Tunachangia sana Pato la Serikali. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ambayo ni hifadhi bora Afrika na Duniani ndiyo asilimia 80 iko Mkoa wa Mara. Madini ya Barrick ipo Mkoa wa Mara, tuna Maziwa, tuna kila kitu lakini mipango yetu ya ndani ni mibovu sana.

Mkao umechoka, viwanda vyote vya Maziwa vimekufa! Viwanda vya pamba vimekufa! Tunafanyaje sasa, tunajiuliza ni kosa au ni nini? Mkoa wa Baba wa Taifa ndiyo umefikia hatua hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yenu mnayoipanga, muangalie. Kwenye maji mtupe maji na kwenye viwanda mtusaidie kupata viwanda. Tusaidieni kufufua viwanda vilivyoko Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, nafikiri hilo nalo ni jambo mnatakiwa kuliangalia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu ajira. Bodi ya Mikopo ya Tanzania inatoa mikopo shilingi bilioni Sita mpaka shillingi bilioni 730 mwaka huu. Kwa mwaka inazalisha watoto wanaotoka kwenye vyuo wanaomaliza kati ya 100,000 mpaka 150,000. Wanamaliza, wanaenda wapi? Miaka nenda rudi wanaenda wapi. Vijana wengi wanaotoka maeneo hayo wamejiunga na bodaboda na bajaji. Sasa sikiliza gharama za bajaji, gharama za bodaboda acha kulipa leseni shilingi 150,000, mimi najiuliza shilingi 150,000 bodaboda analipa leseni, si mmpunguzie? Mwekeeni hata shilingi 50,000. Bodaboda analipa bima shilingi 140,000 mpaka shilingi 354,000 waliokopa benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda wanalipa *LATRA* shilingi 22,000, *TRA* shilingi 120,000, *TARURA* 180,000 kwa nini? Maskini watoto wale waliosoma wengi wamekwenda kujiunga kwenye bodaboda na bajaji. Badala ya kuwapunguzia hizo gharama waishi, tunawaongezea gharama. Mheshimiwa Profesa Kitila Waziri wa Mipango, hilo nalo uliangalie tuweke vizuri ili tusije tukawaumiza hao watoto wetu kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwamba, mipango yetu yote ni mizuri na nchi yetu siyo kwamba tunafanya vibaya sana, mipango yetu ni mizuri sana. Tatizo letu liko kwenye ulaji. Kama tunaweza kuweka mifumo mizuri ya kuziba mianya ya ulaji, Taifa letu litaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiombe sasa na niwaombe Waheshimiwa Wabunge, huko tunakokwenda kwenye miaka ijayo na bahati nzuri hii ni miaka ya lala salama, tukubaliane kwenye mambo mengi, maeneo ambayo yana walaji, sekta ambazo kama Wizara ina walaji wengi, Waziri wake na watu wake wote tufyekelee mbali. Tumeshachoka sasa mambo ya ulaji hapa, huko tunakokwenda mbele tupange mipango, Waziri yoyote asiyedhibiti ulaji kwenye Wizara yake tuondoke naye. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Khadija Aboud, ujiandae Mheshimiwa Bonnah Kamoli, ujiandae Mheshimiwa Mafuwe. (Makofi)

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mipango mizuri ya kuona Tanzania inapaa ndani ya nchi lakini inapaa Kimataifa kwa mipango madhubuti ya kuwainua wananchi kiuchumi na kuleta maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili waliotuletea Mpango huu na vipaumbele vyenye mwelekeo na tija kwa wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia najielekeza kwenye upande wa mazingira. Ukataji wa miti bado unaendelea kwa kasi lakini hauendi sambamba na upandaji wa miti, kwa maana miti inachukua muda kukua, lakini miti mizima tayari inakatwa. Ushauri wangu ni kwamba, kwenye mpango huu waweke fungu au bajeti maalum kwa ajili ya nishati mbadala kwa matumizi ya wananchi, ambapo nishati hizo mbadala zitakuwa na bei nafuu na zinapatikana kwa urahisi ili mwananchi yoyote aweze kumudu

kutumia nishati hiyo mbadala ili kunusuru ukataji wa miti yetu katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye Ukurasa wa 73 wa Mpango huu, ambapo wameelezea uimarishaji na jinsi ya kuifanya bidhaa ya Lugha ya Kiswahili. Wameweka katika mpango kwamba wataanzisha vituo 30 vya kufundishia katika Balozi zetu mbalimbali. Ni jambo zuri na jema, pamoja na kuanzisha madarasa katika nchi mbalimbali za Kiafrika. Hoja yangu iko hapa kwamba pamoja na kuwekeza nje, kusomesha lakini na ndani tuwekeze fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo zaidi kwenye taaluma ya Kiswahili, kwa fani ya ualimu, ukalimani na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili. Kuwajengea uwezo zaidi wa kuongeza lugha mbalimbali waweze kuzimudu zaidi. Kwa hiyo, na hapa ndani ya nchi tunataka tuwekeze zaidi ili tuwe na Waswahili wabobezi wanaoweze kufanyakazi hii duniani badala ya kuwa na lugha moja tu ambayo badala yake huko tunakopeleka mafunzo wakalikamata hili soko la ajira kwa maana ya kwamba wao watakuwa na lugha nyingi zaidi kwa hivyo wanaweza kwenda nchi nyingine zaidi na hawawezi wakabakia katika nchi zinazojifunza Kiingereza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo ninaposisitiza kwamba tuwajengee uwezo zaidi Waswahili wetu na wataalam wetu wa ndani ili waweze kukidhi vigezo, kusomesha, kufundisha na kuwa wakalimani kwa lugha mbalimbali na nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea najielekeza kwenye upande wa kilimo. Tumeona mipango mzuri na tunaipongeza Serikali kwa uongeza bajeti kwenye Wizara ya Kilimo kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kilimo, kwenye mbegu na viuatilifu. Nashauri Kiwanda cha Kibaha kitumike kwa ajili ya kutengeneza viuatilifu ambavyo tutavitumia hapa nchini. Kile kiwanda kina uwekezaji mkubwa na kina uwezo mkubwa. Tufanye mipango ya kuweza kuwekeza pale kuzalisha viwatilifu ambavyo tutavitumia hapa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hii ya kilimo, nashauri pamoja na mambo yote ya umwagiliaji, lakini nashauri tuongeze uwekezaji kwenye viwanda vya mbolea ambavyo vitamilikuwa na wawekezaji wa ndani, kwa sababu mbolea ni siraha kubwa kwenye kilimo. Kwa mfano, sasa hivi asilimia 25 ya mbolea, Urusi peke yake tunaagizia asilimia 25 ya mbolea Tanzania, haya hiyo ni nchi moja tu. Kwa hiyo, mbolea inahitajika sana ndani ya nchi na tuweze kuwa na mbolea yetu hapa nchini yatakapotokea majanga, maafa na mambo yote duniani tuwe na utoshelevu wa mbolea yetu ndani ya nchi, ambapo viwanda hivyo tunaweza kuvidhibiti na kuvipangia sisi wenyewe namna ya usambazaji bora wa mbolea ili wananchi na wakulima wetu, mbolea hii iweze kuwafikia kwa bei nafuu na kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nasisitiza tuwe na viwanda vyetu vya mbolea. Baada ya kuupima udongo wetu tutaweza kufahamu ni aina gani ya mbolea tunahitaji katika ardhi yetu za Tanzania. Nasisitiza kuongeza uajiri wa Afisa Ugani wa kilimo na uvuvi. Kwa sababu wakulima na wavuvi wanahitaji utaalam wa kupewa ili wawekeze kwenye hizi sekta bila kupata hasara. Wanaingia kwenye kilimo na uvuvi lakini bila kuelekezwa na kuwa wataalam, wanapata Maafisa Ugani wa kutosha na wanawafikia kwa wakati, wanaweza wakapata hasara. Tunataka tuendelee kuhamasisha kilimo na uvuvi ziwe ni sekta mbili ambazo zinatoa ajira kubwa kwa vijana wetu na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, Shirika la *TAFICO*; Shirika la *TAFICO*, tumelifufua. Ni jambo zuri na ni jema na tutaingiza fedha nyingi sana pale na hasa tukianzisha huu uvuvi wa Bahari Kuu. Shirika hili linahitaji uwekezaji mkubwa, kuna mambo tumeambiwa hapa kwenye mpango kwamba kutanunuliwa magari ya barafu lakini bado kunahitajika fedha. Zitafutwe fedha ili hili shirika lifanye kazi. Kila bajeti tunaweka fedha lakini halifanyi kazi, ni vema tukaamua kuwekeza fedha za kutosha tukamalizana na hili la *TAFICO* na likaanza kufanya kazi likaingiza faida kuliko kufanya kidogo kidogo, mitambo na majengo yanaharibika baadae tukarudia kurekebisha. Lifanye kazi ili tupate fedha za kigeni kwa upande wa uvuvi pamoja

na kuimarisha uvuvi mdogo mdogo pamoja na uvuvi mwingine ambao ni wa viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, nakwenda kwenye Sekta ya Uwekezaji. Kwenye Sekta ya Uwekezaji wa Viwanda tuhamasishe zaidi uwekezaji kwenye viwanda vya maziwa ya unga. Tunapoteza fedha nyingi za ndani ya nchi kuagiza maziwa ya unga kuletwa Tanzania wakati tuna maziwa mengi. Kutokana na ng'ombe wetu walio wengi tutasaidia wakulima wetu wa upande wa ufugaji ili kupata fursa ya kuuza maziwa yao katika viwanda ambavyo vitatengeneza maziwa ya unga badala ya kutumia fedha zetu za kigeni kuagiza maziwa ya unga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye mpango kuna kufufua kiwanda cha sukari. Hili ni jambo jema, nashauri kiwanda hiki kifufuliwe kwa haraka ili wanafunzi waanze kusoma ili tupate ajira kwa vijana wetu. Kwa sababu sasa hivi tunaagiza wataalam wa sukari kutoka nje ya nchi na tunawalipa fedha nyingi za kigeni, tunao uwezo wa kuanzisha chuo chetu cha sukari na tukapata vijana wataalam wa kuendesha hivi viwanda vyetu vya sukari, ambavyo sasa hivi viwanda vingi vya sukari vinaanzishwa lakini pia na vingine ambavyo vinatanuliwa ili viweze kuzalisha zaidi sukari lakini wana uhaba wa wataalam wa sukari.

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, ajiandae Mheshimiwa Saasisha Mafuwe, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika huu mpango wa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na kipekee kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba anailetea nchi yetu ya Tanzania maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 3(24) Ukurasa wa Sita, Mpango umeongelea kwamba katika Mpango huu pamoja na athari za majanga ambazo zinatokea katika nchi yetu nazo zimeingizwa katika mpango. Majanga ambayo yameongelewa ni vita, magonjwa ya mlipuko pamoja na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiongea hili jambo kwa muda wa miaka mitano mfululuzo sasa, kuhusiana na Mkoa wa Dar es Salaam, kuna Bonde ambalo linaitwa Bonde la Mto Msimbazi ambalo limepita Wilaya tatu. Limepita Wilaya ya Ilala, Wilaya ya Ubongo, pia liko Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimwombe Waziri wa Mipango, ana mipango gani na Mkoa wa Dar es Salaam? Tukizingatia Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo Mkoa ambao unalipatia Taifa kipato au una uchumi mkubwa, asilimia 80 ya uchumi wa Tanzania unatokea Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa juzi kama siku nne mvua imekuwa ikinyesha mfululizo katika Mkoa wa Dar es Salaam, hivi ninavyokuambia pamoja na Jimbo lako na Majimbo mengine na asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ambao tuko hapa katika Bunge hili wengi wanaishi Dar es Salaam na wengi wanaishi Jimbo la Segerea, ni jambo la kushangaza, kila mwaka Mkoa wa Dar es Salaam lazima upate mafuriko na viongozi wapo na mipango inapangwa. Nilikuwa nataka nimwombe au nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Mipango ana mpango gani na Mkoa wa Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Bonde la Mto Msimbazi na tumeongea hapa mwaka jana kwamba, mwezi wa Tatu Bonde la

Mto Msimbazi litaanza kujengwa kwa kuwekewa kingo. Pia, tukawaambia na wananchi wetu kwamba, hawana sababu ya kuhama kwa sababu sasa wanaenda kutengenezewa kingo za Bonde la Mto Msimbazi pamoja na kulifanyia *beautification* ili maji yasiweze kuwaingilia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi hakuna kitu chochote ambacho mimi kama Mbunge ambako Bonde hilo limepita ambacho kimefanyika. Hivi juzi mvua ilivyonyesha, kwa sababu ya miundombinu chakavu ambayo ipo kwenye Mkoa wa Dar es Salaam, maji yamejaa mpaka kwenye nyumba za wananchi. Kabla ya haya maji hayajatokea au mvua hazijatokea, watu wetu wa hali ya hewa walishatoa tahadhari kwamba kuna mvua kubwa inakuja lakini hakuna kilichofanyika. Mpaka sasa hivi ninavyokuambia kuna mafuriko makubwa sana katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nijue haya mafuriko ya Mkoa wa Dar es Salaam yataendelea kila mwaka na ndiyo itakuwa hivi hivi? Basi tuwatangazie wananchi kwamba kila itakapofika msimu wa mvua watatakiwa wahame kwenye makazi yao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata vitendea kazi hakuna. Mfano, mabasi ya mwendokasi katika siku hizi zote ambazo mvua inanyesha kulikuwa hakuna Mabasi ya Mwendokasi Dar es Salaam. Mabasi ya mwendokasi yaliyokuwa yanafanya kazi pengine ni mawili au matatu. Kwa hiyo, hii yote inaleta athari za kiuchumi katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Kwa sababu mvua itakaponyesha hakuna bodaboda anayefanya kazi, hakuna mamantilie anayefanya kazi, hakuna mtu yeyote na hata wanaokwenda kazini wanachukua masaa matatu kufika ofisini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mazingira na wewe uko hapa, hili ni jambo ambalo

tunaliongelea kila siku, kila mwaka, Mkoa wa Dar es Salaam lazima upate mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba wanaanza kujenga miradi ya *DMDP*. *DMDP* mpaka sasa hivi ninavyokwambia bado haijaanza na sijui inaanza lini. Mifereji mingi ambayo inapita katika Majimbo haya matatu inatakiwa kujengwa na kwa sababu ni chakavu ndiyo maana mvua ikinyesha kidogo maji yanaingia kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunasema kwamba watu ndiyo wameufuata mto, sasa hivi maji ndiyo yanawafuata wananchi! Kwa sababu maji yameacha njia yake ya asili yamekwenda kwa wananchi kwa sababu ya miundombinu chakavu. Mheshimiwa Waziri wa Mipango tunaomba sana hili Bonde la Mto Msimbazi, wakati wa kuhitimisha tunaomba sana utuambie hili linajengwa au halijengwi ili tuwaambie wananchi wetu waweze kujua kwamba hili Bonde linajengwa au halijengwi ili waweze kuhama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam, mtu yeyote anayekuja Tanzania ni lazima ashuke Dar es Salaam. Mtu yeyote anayeondoka kwenda nchi za nje lazima aondokee Dar es Salaam, na ni Jimbo la Segerea, lakini Mkoa wa Dar es Salaam hatuna mashamba, chakula chote ambacho kinalimwa Mikoa tofauti tofauti kinakuja Dar es Salaam, lakini ukifika Dar es Salaam yenyewe miundombinu ni mibovu ni afadhali hata katika Mikoa mingine. Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunaomba sana mje na mpango ambao utaiweka miundombinu mizuri katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu inawezekana na sisi tuwe na barabara nzuri lakini pia tuachane na mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea, Mheshimiwa Waziri wa Mipango ameongelea kuhusiana na uchumi wa nchi yetu pamoja na uchumi wa wananchi wetu. Katika Jimbo langu la Segerea, Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni, kuna wananchi 1,800 ambao tayari wamefanyiwa tathmini mwezi

wa sita. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha baadaye tulienda naye tukafanya mkutano, wakaambiwa kwamba wanalipwa mwezi wa tisa. Mpaka sasa hivi wale wananchi bado hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, nakuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, uwalipe hawa wananchi kwa sababu tulishawaambia kwamba wanalipwa mwezi wa Tisa, na sasa hivi ni mwezi wa 11. Baada ya haya wananchi kuambiwa wanalipwa, tayari wameshabomoa nyumba zao, wengine wameshaondoka, nyumba ambazo zilikuwa zinapangishwa wapangaji wameondoka, lakini pia familia za hao watu tayari wametoa watoto wao wamepeleka sehemu nyingine. Pale pamekuwa ni sehemu ambayo watu walihama muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na mambo yote ambayo yameendelea kwa uhakiki na viwanja ambavyo mmeenda kuangalia, naomba hawa wananchi sasa walipwe, imekuwa muda mrefu, karibu miezi sita imekwisha wanasubiri hayo malipo. Tunaomba sana Serikali iweze kuangalia hawa wananchi waweze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kuongelea ni kuhusiana na Vituo vya Afya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea vifaa vya vituo vya afya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa. Nakuongezea sekunde 10.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Tayari!

**MWENYEKITI:** Nakuongeza sekunde 10.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuweza kutuletea Vituo vya Afya, pamoja na vifaa. Tunashukuru, lakini tungependa tuongezewe kwa sababu jimbo langu lina wananchi wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa tunakwenda kwa Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/2025. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anafanya kwa Taifa letu. Sasa hivi Hai ni mpya, ya kilimo na viwanda, miradi mingi kwenye upande wa elimu, afya, kila mahali ndani ya Jimbo la Hai, magari yananguruma kuonesha kwamba shughuli zinaendelea. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Mipango na kumpa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kuwa Waziri wake. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona hili. Nimesoma taarifa hii, na sijui nilikuwa na matarajio makubwa sana, nimeona sivyo kama ambavyo nilikuwa nafikiri kwamba pengine uwepo wa Wizara hii maalum tungekuja na vitu vingine vipya maalum. Kwa kutambua umahiri wa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, bahati nzuri alikuwa jirani yangu hapa, mambo makubwa ya nchi hii ambayo tulikuwa tunajadili, nimeyatafuta humu, nimesoma mara mbili, mara tatu sijayaona. Naomba nishauri tu, pengine muundo wa namna ya kufanya jambo hili likawa zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yangu ni kuona sasa tunakuwa na mipango ya nchi yetu ambayo inataekelezeka kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu, mipango ambayo itajibu matarajio ya wananchi. Naomba nisome na uniruhusu ninukuu

ukurasa wa 13, unasema; "ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinua kiwango cha maisha cha watu wetu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mrefu na muda mfupi ijayo itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unatengeneza utajiri na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezewa thamani nje ya nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona sentensi hii nikalazimika kusoma kutafuta majawabu yake kwamba tunapataje ajira? Tunaongezaje thamani? Nikaona ni yale yale tuliyosema mwaka jana 2022. Sasa naomba nishauri, ili tuweze kuwa na mipango ya nchi yetu, kama ambavyo amesema kule nyuma, mwishoni kwenye hitimisho lake, amesema kwamba mpango huu ni wa Taifa, siyo mpango wa Serikali. Ningetegemea sasa atupe dira ya kuwa na mpango wa miaka 100, kuwa na mpango wa miaka 50, lakini tuanze na huu mmoja mmoja angalau mwelekeo wa kufanana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kazi ya viongozi wetu, wanatengeneza falsafa, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametengeneza falsafa yake na akatutengenezea mpango kwamba ni *Building Better Tomorrow*.

Mimi nilikuwa nashauri, hivi vitu vinavyotengenezwa na Wizara ya Serikali, kuwe na *intellectual committee*. Tafuta watu wenye *exposure* kubwa, wenye uwezo mkubwa, tengeneza timu ambayo haipo kwenye mfumo huu wa kawaida wa watumishi wetu ambao kila kitu watakuitikia. Chagua watu ambao wapo kwenye mataifa mbalimbali, Watanzania wenzetu wako kwenye vyama mbalimbali, tusiangalie chama, hata kama wako vyama vingine vya upinzani, walete pamoja iwe ni *intellectual committee*. Kazi yake ni kukushauri na kutengeneza mipango ya muda mrefu na muda mfupi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nina mashaka kwamba hivi vitu ambavyo tunavifanya vinaweza vikawa

vya mtu mmoja. Leo kuna kitu hiki kinaitwa *Building Better Tomorrow*. Ukisema *Building Better Tomorrow,* sura inayokuja hapa ni ya Mheshimiwa Bashe. Sasa tunatamani tutoke huko, kitu hiki kiende kiwe ni cha sura ya Taifa ili hata kama yeye hayupo, akija mtu mwingine, anaboresha na kuendeleza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna *vision* kwenye madini 2030, ikitajwa unaona kabisa Mheshimiwa Mavunde huyu hapa. Sasa ikishakuwa wametengeneza vitu vya namna hii, vipelekwe kwenye ile *intellectual team* waangalie *pros* na *cons* zake, waangalie namna gani jambo hili linaweza likaendelea mbele ya safari. Lengo ni ku-*ringfence* hayo mawazo mazuri yawe endelevu. Kesho Mheshimiwa Mavunde, akitoka kwenye Wizara ya Madini, akija mwingine, anakuja na jambo lake. Sasa ni kwa namna gani tu-*refence* mawazo yetu yawe endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, jambo hili kama tusipolitazama vizuri; bahati nzuri nchi yetu tunapata viongozi wenye hekima kubwa sana. Hebu tazama Mheshimiwa Rais, alipoingia, akaja na jambo, "Kazi Iendelee." *What if* angeamua kusema *Building New Tanzanian*, na akachukua mawazo ya wale jamaa kwamba, aah, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni maendeleo ya vitu, siyo ya watu. Ujenzi wa daraja la Busisi, ni maendeleo ya vitu, akaacha vile vitu tungekuwa na hali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojaribu kusema hapa ni kwamba, pamoja na bahati nzuri tuliyonayo na viongozi wetu wenye busara kubwa, lakini Wizara yako ifikirie namna ya kuwa na mipango ambayo imezuiliwa imekuwa, *ringfenced* kama *interests* za nchi hii, yeyote atakayekuja atekeleze. Leo tuna Waziri wa Fedha, anaitwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, akitoka pale akija kaka yangu Mheshimiwa Masache hapa, aendeleze yale; hata akija Mheshimiwa Mpina kwenye Wizara ya Fedha, aendeleze hayo hayo atake, asitake. Kwa hiyo, hicho ndicho ambacho ningetamani sana Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo utusaidie. Hivi vitu tunavyovifanya, kiongozi kazi yake ni ku-*drive* falsafa yake.

Ikishakuwa *driven* na kiongozi huyu, akabidhi kwenye hiyo *intellectual team*, itengeneze mfumo wa kuvizuia hivi vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani kuona, amezungumza hapa Mheshimiwa Profesa Manya, tunaenda kwenye Liganga na Nchuchuma, Serikali imeshalipa fidia. Hebu tufikirie mambo magumu, Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*, kipo pale, hivi kwa nini tusifikiri kwanza kutengeneza chuma pale? Tayari wametengeneza *foam machine,* tuboreshe ili tuzalishe bidhaa zetu ndani kama ambavyo kwenye hotuba yako umesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mkoa wa Kilimanjaro, *strategically* ni wa kibiashara pamoja na kwamba tuna ardhi ndogo. Pale uwanja wa Kilimanjaro *(KIA)* kulikuwa na reli inaingiza mizigo kule ndani, sasa hivi ile reli imekufa. Naomba Serikali ione namna ya kurejesha ile reli, mizigo iwe inaenda pale. Pale kuna *cold room* nzuri. Mwalimu Nyerere alikuwa na *vision* nzuri sana kuhakikisha uwanja ule unakuwa wa kimkakati wa kilimo. Sasa hivi Serikali imepeleka fedha, tunajenga *common use facility* pale, kuna *cold room*. Naomba ile reli ifunguliwe ili mizigo yetu iweze kusafiri kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uanzishaji wa Soko la kwa Sadala, hili nilikuwa nikisema sana ni la kimkakati, ifike mahali Serikali ikubali. Tumeshatenga eneo, bahati nzuri watu wa ushirika wametukubalia, tumetenga eneo, tumechora michoro mizuri. Sasa siyo kila mwaka niwe nahubiri hapa Soko la Kwasadala, Soko la Kwasadala, kila Mbunge anajua hilo Soko la Kwasadala, lakini halijengwi. Naomba mtusaidie tuweze kujenga soko lile. Ni sambamba na eneo lile, kuna wafugaji wengi wako pale. Tuanzishe machinjio ya kisasa. Hivi vitu viwili tukienda navyo vitatusaidia sana kuinua uchumi wa eneo letu la pale kaskazini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo kwa sababu kengele imepiga hoja yangu imeisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimia Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie kwenye hoja iliyoko Mezani. Nitangulie kwanza kumpa pongezi sana Mheshimiwa Profesa Kitila kwa kuaminiwa na kupewa Wizara nyeti ya Mipango na Uwekezaji. Vile vile nimpongeze kwa hotuba yake aliyotoletea Mezani, ambayo kwa kweli imesheheni mambo ya uhakika kwamba inaweza ikatuvusha. Nampongeza pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa hotuba yake ya Mwongozo na Ukomo wa Bajeti ambapo hivi viwili vinakwenda pamoja; Mpango na Bajeti, viko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango tulioletewa Mezani Profesa anasema ni mpango utakaokuwa na tija ya uzalishaji katika kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini. Kwa maana nyingine ni mpango ambao unakwenda kuchochea kasi ya ukuaji uchumi ambao utakuwa jumuishi, pia utakwenda kupunguza umaskini na kutengeneza ajira nyingi. Kwa hiyo, mwisho wa siku tunakwenda kutengeneza matajiri. Nakupongeza sana Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili huu mpango uzae matunda, na uwe ni mpango kweli kweli wa maendeleo, tunahitaji Barabara, kwa maana ya miundombinu, tunahitaji nishati ya uhakika kwa maana ya mafuta na umeme. Katika hili naipongeza sana Serikali, imefanya kazi nzuri sana katika kutatua tatizo la umeme. Bwawa la Nyerere liko mbioni kukamilika na tuna uhakika mwakani tutaanza kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna tatizo. Mafuta imekuwa ni shida kubwa sana, yanapanda bei kila mwaka. Kwa hiyo, iko haja kubwa sana sasa hivi ya ku-*shift focus* kwenda kwenye *gas (LNG)*.

Tunajua kwamba Serikali ipo kwenye mipango hiyo, tunaipongeza, lakini tunaomba iharakishe ili mikataba isainiwe, miradi ile ianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Barabara pia Serikali imefanya vizuri sana. Mtandao wa barabara nchini umekaa vizuri, lakini mpango huu uangalie kwa undani, kuna ushauri umetolewa na Kamati ya Bajeti; hizi barabara zina kasoro nyingi sana ambazo zimeainishwa kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti. Tunashauri yale maoni yafuatiliwe na kuhakikisha kwamba zile kasoro ambako zipo, ziondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ya barabara iliyofanyika, tunasema kwamba maendeleo na mipango hii itekelezwe kwa kuangalia *geographical area* na *geographical features* za maeneo yetu hapa nchini. Eneo letu kule Arumeru Mashariki, eneo kubwa ni mlima na siyo kule Arumeru tu, kule Upareni, Usambaani wananchi wako milimani. Huku tunapokwenda, mipango yetu ya maendeleo iangalie ni namna gani hizi barabara zinazokwenda mlimani zitatengenezwa ziwe tabaka gumu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Mkumbo utakapokuja kuhitimisha uweke bayana kwamba barabara za milimani zinakwenda kutengenezwaje ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanafikiwa na wanapata huduma muhimu za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba aliyotoa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tarehe 13 Novemba, 2020 alisema kwamba "Dira itakayomwongoza katika kuteleleza majukumu yake ni pamoja na Ilani, Mpango na Ahadi." Sisi kule Meru, tulimweleza kwamba kuna barabara ya King'ori, ambayo inagusa wananchi wengi sana, na ni barabara ya kimkakati. Alituelewa na kutoa ahadi ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Leo ni mwaka 2023 tunakwenda kumalizia miaka mitano baada ya mwaka mmoja na nusu, barabara ile haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Profesa Kitila utakapokuja kuhitimisha utekelezaji wa mpango huu, utuhakikishie kwamba ile barabara nayo inaingia kwenye mpango ili tupate majibu ya kuwaeleza wananchi wetu mwaka 2025. Hii ni pamoja na kuangalia ujenzi wa barabara za kwenda milimani nchi nzima kwamba ziwe za tabaka gumu, kama siyo lami, ambapo itafanya zile barabara zipitike na matengenezo ya mara kwa mara yasiwepo ambayo yataisumbua sana *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo, katika hotuba ya Rais, alisema kwamba tunakwenda kuweka utaratibu wa kuanza kuvuna maji ya mvua ili yatumike kwa ajili ya umwagiliaji. Pale Kingori Malula, kila msimu wa mvua yanatokea mafuriko mpaka yanaua. Wakati wa kuja kuhitimisha Mheshimiwa Prof. Kitila, tafadhali sana uje na mpango wa kujenga bwawa eneo lile, maji ya mvua yavunwe, yatumike kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Arusha, zamani tulikuwa na Kiwanda cha Pareto, na Kisimiri Juu walikuwa wanalima Pareto nyingi sana. Kiwanda kile kilifungwa na Kilimo cha Pareto kikasimama, badala yake kule Kisimiri Juu sasa hivi ndiko wanakolima bangi. Tunashauri Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, kwenye mpango wako; Kusini, Iringa nadhani wanajenga Kiwanda cha Pareto kwa ajili ya kutengeneza viuatilifu. Nashauri kwamba kilimo cha Pareto kifufuliwe kule Kisimiri Juu ili wananchi waachane na kilimo cha bangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, muda wetu umebaki mdogo. Kwa hiyo, jioni tutakuwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Suma Fyandomo na Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linarejea.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na shughuli zetu naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kuna fomu kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zitapitishwa Bungeni ili kila Mheshimwa Mbunge aweze kujaza eneo moja lenye changamoto katika jimbo lake kwa ajili ya kujenga kituo kimoja cha afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Waheshimiwa Wabunge, mnasisitizwa kutoa ushirikiano kujaza fomu hizo leo ili ziweze kurejeshwa Wizarani na kuanza kufanyiwa kazi kwa uharaka. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mapendekezo ya Mwongozo na Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yotu tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mpango huu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, kumpongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia mpango huu kwa kusema reli ya kisasa, reli ya kisasa ambayo ni *SGR*. *SGR* hasa hapa naongelea kuwa napongeza Serikali kwa sababu imefanya kazi nzuri sana lakini kipande hiki cha kutokea Dar es Salaam mpaka Morogoro chenye 300km naomba na ninashauri kuwa kimefikia 98.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kiweze kukamilika kwa wakati. Kikikamilika kwa wakati tutaweza kupata mapato, tutaweza kuinua uchumi wa nchi yetu na kupata ajira hasa kwa vijana ambao mpaka sasa hivi hawana ajira ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongeza hapo hata kipande cha kuanzia Mororgoro mpaka Makutupora chenye 422km na chenyewe kifanyiwe kazi na chenyewe kiwezekumalika kwa uharaka iwezekanavyo kusudi tuweze kupata pato la Kitaifa na kuinua uchumi pamoja na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia hapo ni barabara. Naomba niongelee kuhusu barabara, kuna barabara nyingi kwa kweli ambazo zimechukua muda mrefu hazijakamilika zimeingia kwenye mipango iliyopita kwa hiyo, nashauri hata kwenye mpango huu ambao unakuja wa 2024/2025 naomba nashauri kuwa barabara hizi ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikishauri kuwa barabara kwa mfano ambayo huwa tunaongelea sana ambayo ni ya Kidatu mpaka Namtumbo inaendelea vizuri lakini nashauri kwa sababu sehemu kubwa bado haijatekelezeka kwa hiyo, iweze kuwekwa kwenye mpango na iweze kutengewa fedha kusudi iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Bigwa – Kisaki imechukua nayo muda mrefu, barabara ya Ubena - Mvuha imechukua muda mrefu vipande ambavyo tunaongelea mara kwa mara humu Bungeni kipande cha Kilosa – Mikumi, kipande cha Tuliani – Mziha naomba na vyenyewe viweze kukamilika kwa mpango huu mbao tunakwenda nao wa 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bwawa la Mwalimu Nyerere napongeza Serikali kwa sababu bwawa hili likikamilika tutaweza kupata umeme wa kutosha ambao utazalishwa *kilowatt* 2115 ambao utakuwa ni umeme wa kutosha sana ambao

tutaweza kuutumia hapa nchini na tutaweza kuuza kwenye nchi za nje na utaweza kupunguza bei za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri sana kuwa wakati uliopangwa kuwa bwawa hili litakamilika mwanzoni mwa mwaka ujao 2024 bwawa hili liweze kukamilika kusudi tuweze kuongeza kipato kwa kuuza umeme ndani ya nchi na nje ya nchi na tuweze kuongeza ajira kwa vijana na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa upande wa utalii, utalii unakuza uchumi kwenye nchi yetu unachangia uchumi kwenye nchi yetu. Utalii mpaka sasa hivi ambao unasemeka sana ni utalii wa Kaskazini sasa hivi na mimi nashauri kuwa kila mahali kuwa mahali pengi kuna utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nashauri kwenye mpango huu tuweze kutangaza utalii wa Kanda ya Kusini, utalii wa Kanda ya Mashariki, tuna Milima ya Udzungwa, tuna Milima ya Uluguru, tuna na mambo mengine Mikumu, tuna mambo mengine mengi mpaka ukanda wote wa mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na utalii wa Kanda ya Ziwa pia uweze kutangazwa kusudi tuweze kupata watalii wengi ambao wataongeza kipato cha nchi yetu na kukuza uchumi wa nchi yetu pia na vijana waongoza watalii wataweza kupata kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa nchi yetu, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi nilikuwa nashauri tena kuwa kwenye mpango huu licha ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutenga fedha kwenye kilimo naomba tena na nashauri tena kilimo cha umwagiliaji kiweze kuzidi kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mpaka sasa hivi ni 2.8% tu ndiyo inayomwagiliwa kufuatana na eneo lote ambalo linaweza likamwagiliwa. Nikisema kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha kisasa,

kilimo cha kisasa kinaendana pamoja na mbolea, kinaendana pamoja na mbegu bora na kinaendana pamoja na viatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye mpango huu taasisi ambazo zinahusika zikiwepo *ASA*, *TOSCI*, naomba ziweze kuangaliwa kwenye mpango huu kusudi tuweze kuwa na kilimo ambacho tutazalisha mazao mengi, tutapunguza umaskini na tutaweza kutoa ajira na kukuza kipato cha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku ya mbolea. Ruzuku ya mbolea naipongeza Serikali ambayo kutokana na ruzuku ya mbolea watu wengi wameanza kutumia mbolea kwa sababu ni ruzuku kwa hiyo, bei imepungua watu wengi wameanza kutumia hiyo mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu nilikuwa nashauri kuwa kutokana na matumizi ya mbolea hii iweze kupatikana kwa wakati na kwa wingi ili wananchi waweze kuitumia mara wanapohitaji mbolea hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye ongezeko la uwekezaji nilikuwa naomba na ninashauri Mheshimiwa Waziri tuwawekee mazingira mazuri hawa watu wa uwekezaji kwenye viwanda, nikija kwenye viwanda unakuta kuwa viwanda vingi vilivyokuwepo zamani kama vya nguo, viatu kwa mfano Mopuwoko ya Morogoro viwanda vilikufa kwa hiyo nilikuwa nashauri kuwa mazingira mazuri yaweze kuwepo kusudi wawekezaji waweze kuja na kuwekeza na tuweze kupata mambo yetu kwa mfano pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba tunaweza kupata viwanda vya pamba kusudi tukaweza kupata nguo ambazo tunatengeneza hapa nchini badala ya kununua mambo ya nje. Nashauri kuwa kwenye mpango huu uweze kuangaliwa kuwa mpango uwe mzuri ambao utaweza kuwawezesha hawa wawekezaji kupata muda wa kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye ujenzi wa bandari. Ujenzi wa bandari ya uvuvi, nashukuru Serikali ujenzi wa bandari kule

Kilwa – Lindi umeanza na unaendelea vizuri ila nashauri ukamilike kwa wakati kama ulivyopangwa kusudi tuweze kutumia hiyo bandari kwa meli ambazo ni kubwa ambazo zinaweza zikatinga pale na tukaweza kuajiri vijana na wanawake pamoja tukaweze kupata na uchumi na kuinua pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ununuzi wa meli kusudi tuweze kupata meli za kuweza kuvua kwenye maji ya bahari kuu. Uchumi wa bluu, kwa upande huu bado hatujakita sana. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali iweze kununua hizo meli ambao huu mpango ulikuwepo kwa muda mrefu wa kununua meli nne, mbili bara na mbili Zanzibar kusudi ziweze kununuliwa kwenye mpango huu ziweze kuonekana kusudi tuweze kuvua Samaki kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa upande wa *BBT* kwa kweli hapa nampongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, Waziri Bashe, Waziri Ulega kwa upande wa *BBT* ambayo imesaidia sana. Mpaka sasa hivi vijana na wanawake 800 kwa Wizara ya Kilimo na 200 kwa Wizara ya Mifugo pamoja na Uvuvi wameweza kuingia kwenye mpango huu wa *BBT*, *BBT* inasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kuwa kadri tunavyokwenda fedha ziweze kutengwa kusudi vijana wengi huu mradi uweze kupanuka kusudi vijana wengi waweze kwenye mradi huu wa *BBT*. Kwa upande wa masoko ya ndani nashauri kuwa mazao tunazalisha naomba tuhamasishe Wananchi waweze kutumia mazao tunayoyazalisha hasa ya usindikaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale tunayoweza kuuza nje tuweze kuuza yale ambayo yamethaminishia tayari yamepewa thamani sio kuuza yale ambayo hayajapewa thamani. Jambo jingine kwa upande wa masoko, nilikuwa nashauri kwa mfano tuna-*import* mafuta ya kula lakini tuna ardhi, tuna wananchi, tuna watu ambao wanaweza wakalima alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nashauri kuwa kwa upande wa ngano pia tuna ardhi, tuna watu hivi mambo tuna-*import* kutoka nchi za nje nashauri kuwa mzao ambayo tunaweza kuzalisha hapa nchini tuweze kuyazalisha tuweke mpango mahususi ambao unaweza kuzalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia wakandarasi. Nashauri, naomba wakandarasi wanaofanya kazi zao wakamaliza kwa wakati waweze kulipwa hela zao waache kutangatanga wanapata shida na wengine wanapoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasema ahsante sana naunga mkono mpango, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt Christine Ishengoma nilimtaja Mheshimiwa Athuman Maige. Mheshimiwa Fyandomo na Mheshimiwa Aloyce Kamamba ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie mpango huu wa mapendekezo ya mpango wa Serikali kwa ajili ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu unalenga kuleta maendeleo ya usawa nchini kote na mpango huu utatumia misingi maalum ya kukuza uchumi nchini, kuendeleza sekta binafsi, kuendeleza utawala bora, umoja na amani wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mpango umerejea. Umefanya marejeo ya mpango wa mwaka 2022/2023 na wamepitia mipango ya sekta mbalimbali zilizopita katika mpango uliopita kuwa inaendelea vizuri, miradi ya sekta ya mfano kama vile nishati, ujenzi, elimu, afya na maji inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi katika mpango ya mwaka jana bado inaendelea lakini ipo pia katika mpango huu wa sasa. Huu ni mfumo mzuri wa mipango kuwiana na kuendelezana. Mradi kama wa *SGR*, mradi wa *LNG* na mradi wa umeme wa Bwawa la

Mwalimu Nyerere kule Rufiji miradi hii yote imekusudiwa kuendelea katika mpango huu, mradi wa *BBT* kwa ajili ya kilimo na umwagiliaji utaendelezwa pia katika mpango huu. Hii ni sifa kuwa kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango unaonyesha maoteo ya kukua kwa bajeti mpaka kufikia trilioni 47.4 na makusanyo ya ndani ya mapato kuwa 72% ya bajeti haya ni mafanikio makubwa sana na naipongeza sana Serikali, hongera sana Serikali na hasa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango jambo hili ni zuri sana kukua kwa Bajeti na kukua kwa makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuangalia ile miradi ambayo ilikuwa katika mipango iliyopita lakini haikutekelezwa kwa wakati na kwa mpango husika lkini sasa Wananchi wamepoteza imani na matumaini kwa miradi yao iliyokuwa imepangwa katika mipango iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ipo barabara ya Tabora – Mwambali Shimuwa, Shitage, Ushetu mpaka Shinyanga. Barabara hii ni muhimu sana imeunganisha mikoa miwili hii na inakuza uchumi kati ya mikoa miwili lakini sasa ni miaka mitano ilipofanyiwa usanifu yakinifu lakini haijajengwa mpaka leo hii wala haukuna hata dalili ya kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kasoro kuwa na Wananchi ambao walikuwa wameshangilia usanifu wa barabara hiyo sasa wamekata tamaa. Ipo mipango uko nyuma ilibeba miradi ambayo haikutekelezwa na hakuna maelezo kwa mfano mradi wa Mchuchuma na Liganga Wananchi walitegemea kutengeneza hela nyingi kwa kuwa namradi huu muhimu sana wa chuma na makaa ya mawe lakini sasa mradi huu haujatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo hayatoki Serikalini kutuambia wananchi na kuwaambia Bunge lako nini kinakwamisha mradi huo. Nimeona safari hii kwenye bajeti kwenye mpango huu kuna malipo ya fidia lakini fidia hiyo hatuelewi ni ya nini na wananchi walikuwa

wameka muda mrefu wakingojea mradi huo. Ni vyema Serikali ikatekeleza miradi ambayo imo katika mpango ambayo inaipanga yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa bandari ya Kasanga ambayo tangu imekamilika hakuna hata meli moja iliyotua bandarini hapo. Naambiwa ililenga mizigo ya DRC Congo lakini upande wa DRC Congo bandari zake zote hazina vifaa vya kupakulia mizigokutoka kwenye makasha yaAni makontena. Sasa nashangaa mradi huu wa Kasanga kwanini ulifanya haraka haraka na matokeo yake yamekuwa haya tumepoteza au tunalenga nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi fulani sitaki kuitaja, kwa mfano, sisi tulisaidia kushawishi upande wa pili ili wajenge reli na mizigo iweze kufika ili tufanye kazi ya bandari yetu, sasa Bandari hii ya Kasanga imekuwa *white elephant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la Serikali kutokamilisha miradi ya kila mpango. Nimetoa mfano wa barabara ile ya Tabora - Mambali miaka mitano sasa haijakamilika na wala haijajengwa na ni barabara muhimu sana kwa Mikoa yote miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Upuge, jengo la *x-ray machine* pamoja na *ultra-sound machine* halipo na lilikuwa la mradi wa mpango wa mwaka 2017/2018, hela hazikutosha na mashine hizo zipo ndani ya makasha yake, hatari ya kuharabika ni kubwa kuliko kufanya kazi tena baada ya kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu kwa upande umemalizia na kuendeleza miradi inayoendelea nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; mpango huu ulenge kuleta maendeleo na ustawi wa jamii kwa kuweka fedha za kutosha kusaidia vijana na watu wenye mahitaji maalum. Kwa mfano, ule Mfuko wa Vijana ulioko Ofisi ya Waziri Mkuu uboreshwe lakini pia Baraza la Uwezeshaji la Taifa, mpango wake nao uwezeshwe, lakini

mpango wa halmashauri kutoa mikopo kwa vijana, akina mama na watu wenye ulemavu nao uboreshwe ili uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa kuna matatizo haurejeshwi baada ya kukopeshwa ingawa hauna riba, lakini umekuwa na uzembe na tuhuma nyingi kwamba inawezekana watu wanakopeshana wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo mpango huu wa kukopesha 4-4-2 hauna tija sana ingawa una manufaa sana kwa wananchi na wanautegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta fedha nyingi, lakini pia kwa kuona mbali na kuanzisha Wizara ya Mipango na Uwekezaji, jambo ambalo litaleta mabadiliko makubwa katika upangaji wa mipango ya miaka inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu, nimepokea fedha nyingi sana na hata leo nimetumiwa ujumbe hapa zaidi ya shilingi bilioni 2.6 zimefika jimboni kwangu itakayogharamia miradi mingine mingi, lakini tumepokea Miradi ya Afya, Elimu, Maji, Umeme wa *REA*, Kilimo na Barabara. Kama nilivyosema hata leo hii ela zimeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, liko suala ambalo Watanzania au Serikali hailioni kuwan ni muhimu sana, nalo ni kitu kinachoitwa usalama wa mitandaoni au *cybercrime*. Hili ni tatizo kubwa sana duniani kote, lakini katika Mpango huu sioni kama Serikali imejiandaa kupambana na jambo hili la *cybercrime*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko miradi ambayo sikuiona vizuri sana hasa *TAFICO*, ambayo tunajenga Bandari kule Kilwa na kununua meli nyingine. Mipango hii inaweza kuleta uchumi mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Athuman Maige. Nilimtaja Mheshimiwa Suma Fyandomo, Mheshimiwa Aloyce Kamamba na Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kipekee nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kunipa afya njema na kunitia nguvu na moyo wakati nikichangia ama wakati wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akitafuta fedha nyingi na amezipeleka kwenye halmashauri nyingi, kila Mheshimiwa Mbunge anafurahia kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amir Jeshi Mkuu kwa namna ambavyo anapeleka fedha nyingi kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita kwenye mafanikio ya mipango yetu ya maendeleo yamejengwa katika nguzo kumi. Kwenye hizo nguzo kumi mimi najikita kwenye nguzo namba nne na namba sita ambazo zipo kwenye ukurasa namba 24; kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa namna ambavyo aliwasilisha hapa, aliwasilisha vizuri sana na kwenye Mpango huu natamani kushauri namna ya kuzinyanyua sekta binafsi ambazo hizo ni pamoja na *suppliers*, ni pamoja na wakandarasi na wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kushauri kwa upana wake eneo hilo. Wazabuni wengi, -*suppliers* walio wengi lakini na Wakandarasi, wapo ambao wanadai fedha zao kwa miaka mingi. Wanadai fedha zao kwa miaka mingi kiasi kwamba sasa hivi wapo wengine waliokosa mwelekeo. Kuna Wakandarasi, *Suppliers* na

wazabuni wengine wakifanya kazi wanalipwa fedha kwa wakati, lakini wapo ambao wanadai fedha kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natamani sana kuishauri Serikali, ingefaa kuweka mpango wa namna gani wafanye ili waweze kumaliza madeni yote nchi nzima. Huo mpango endapo watawatangazia Watanzania kipindi cha Bunge la Bajeti litakalokwenda kuanza mwezi Machi maana najua kabisa Mpango huu ni wa mwaka 2024/2025. Naomba sana wawatangazie Watanzania mpango wao, haya madeni yatakuja kukoma lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya kama nilivyosema yaliyo mengi ni ya miaka mingi. Sasa hivi ni Awamu ya Sita, Awamu hii ya Sita ni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama ambaye ana hekima, busara na upendo mkubwa sana kwa wananchi wake wa Tanzania. Naamini Mheshimiwa Rais wetu na Mama yetu atakwenda kubariki jambo hili ili angalau Watanzania wale ambao wanadai Serikali kwa miaka mingi wapate mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na *suppliers*, wazabuni pamoja na wakandarasi, wapo baadhi ya watumishi ambao wametumikia Taifa hili kwa uhuru kwa haki na kwa upendo mkubwa, wanadai mafao yao na hawajalipwa mpaka sasa hivi. Naomba sana wawaangalie hawa wastaafu ambao wamelitumikia Taifa lao, lakini sasa hivi wanapata machungu kwa sababu hawana fedha. Juzi nilikuwa naangalia taarifa ya habari, wazee wanalia machozi, wamestaafu miaka ya nyuma lakini hawajapewa mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu ana huruma na upendo. Naamini sana kupitia taarifa hizi, naomba sana Mheshimiwa Rais Mama yetu awaangalie sana hawa wastaafu kwa sababu kwenye taarifa ile ya habari wengine wanadai wapo wanashindwa kuendeleza majukumu yao na wengine wana madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa madeni, kwa sababu hata hawa wakandarasi wanakuwa wamekopa fedha za kufanyia kazi za ukandarasi. Kule wanaendelea kudaiwa riba, pia katika riba ile kwa sababu walishaweka dhamana ya nyumba zao, waliweka dhamana za mali zao ama viwanja vyao vilishachukuliwa *may be* vingine vimenadiwa, lakini sasa wanashindwa ni namna gani madeni yatalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MHE.CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niungane na anayechangia, kwamba madeni kwa wakandarasi ni makubwa sana na kwamba nawafahamu baadhi ya wakandarasi ambapo wamepata ugonjwa wa moyo kwa sababu ya kudaiwa kwenye mabenki, kwa hiyo naomba Serikali iweze kushughulikia hilo kwa haraka sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma, unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Kajege.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa. Amesema hao waliopata ugonjwa wa moyo, wengine vimeongezeka vitu vitatu, wengine wamepigwa *stroke* kwa maana wamepooza, mshtuko hawaelewi kwamba wataishi vipi, lakini kuna wenye visukari, ndio huo ugonjwa wa moyo, kwa hiyo hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuileta hii Wizara kwa sababu najua ana mpango mzuri sana na Watanzania wake. Hataki Watanzania wake wasumbuke, hataki wapate shida na ndio maana ameunda hii Wizara ya Mpango ili kuhakikisha Mheshimiwa Waziri anasimamia Mipango yote

inayokwenda kufanyika ndani ya Taifa hili ili mambo yaweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Fyandomo. Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Iddi Kassim ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja ambayo iko mbele yetu. Kwa kuanza kwa kweli nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan; Moja, kwa kuunda Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji lakini zaidi kwa kutuletea fedha nyingi kwenye maeneo ya elimu, afya, maji, umeme na kadhalika. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa ushauri; ipo miradi ya kimkakati, ukiwepo Mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, pale tumepeleka fedha nyingi, hebu mradi huu ukamilike, uanze kutumika na uanze kutuletea fedha sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni Reli ya *SGR* kipande cha Dar es Salaam - Morogoro, tunaambiwa kimekamilika kwa kiasi kikubwa. Kipande cha Morogoro - Dodoma, tunaambiwa kimekamilika kwa kiasi kikubwa. Serikali imeweka fedha nyingi pale, hebu eneo hili ambalo limekamilika lianze kutoa huduma na Serikali ianze kurudisha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo msongamano wa magari kutoka hapa Dodoma kwenda Morogoro na kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam. Sasa hivi ukipata usafiri kutoka maeneo haya kwenda Dar es Salaam, ni shida kweli hebu tuombe sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuweka njia mbili kwenda na njia mbili kurudi katika maeneo haya ili usafiri uweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma sasa ni Jiji, Dodoma inakua. Hatutegemei kwamba Dodoma imefikia Jiji itarudi kuwa Manispaa. Ukiangalia kwenye barabara tu unapotoka getini, msongamano ni mkubwa, hebu zianze kuwekwa barabara mbili kwenda na mbili kurudi ikiwa ni pamoja na maeneo mengine ambayo yamebanana sana katika Mji wetu wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara zingine ambazo ziko katika mipaka yetu. Tuombe mipaka yetu ifunguliwe. Nitoe mfano, katika Wilaya ya Kakonko ambako mimi natoka, iko barabara inatoka Kakonko kwenda Kata ya Gwarama lakini kwenda hadi Mpaka wa Mhange. Ule ni mpaka ambao unaunganisha Tanzania na Nchi ya Burundi na Burundi wamehamisha Makao Makuu kutoka Bujumbura kuja Kitega, barabara pekee ambayo inaweza kutuunganisha Tanzania na Burundi ni barabara hii ninayoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ichukue hatua kwa kujenga hiyo barabara ambayo; Moja, itatusaidia kufanya biashara miongoni mwa Tanzania na Burundi; Pili; itafanya bidhaa zetu za Tanzania ziweze kusafirishwa kutoka upande wetu wa Tanzania kwenda Burundi; na Tatu; itasaidia sana wananchi wa maeneo yetu kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo liende sambamba na kujenga ofisi za kukusanya mapato ya Serikali. Tuwe na ofisi katika mipaka yetu ili tuweze kukusanya fedha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia imefanya vizuri ni eneo la elimu. Eneo la elimu tumefanya vizuri. Moja, kwa kuandikisha wanafunzi wengi, lakini tumejenga madarasa na Serikali imejitahidi kuajiri Walimu. Ikumbukwe pia wakati ujenzi wa shule za sekondari za kata unafanyika, maeneo mengi ambako walikuwa wanatafuta eneo la katikati ya kata na hivi kutoka kijiji kimoja kwenda kwenye shule ilipo ni umbali mrefu. Kwa hiyo mvua ikinyesha mwanafunzi inamhusu, jua likiwaka mwanafunzi linamhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali ijenge mabweni kwa ajili ya kuwahudumia watoto hawa. Nina uhakika tukijenga mabweni watoto wataishi katika yale mabweni na itakuwa rahisi kwa Walimu kuweza kuwafuatilia hawa watoto, lakini itakuwa ni rahisi kwa wanafunzi hawa kupata chakula pamoja, lakini itakuwa ni rahisi sasa badala ya watoto kuishi kwenye nyumba ambazo hazifahamiki, watoto hawa watakuwa wanaishi sehemu ambayo tuna uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabweni haya yakijengwa nchi nzima, maana yake kutakuwa na uwezekano kuwachukua wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka Mkoa wa Kagera, unawapeleka hata Singida, unawachukua wa Singida unawapeleka Kigoma kwa sababu tuna uhakika wa mabweni katika maeneo hayo. Suala ambalo litakuwa la msingi ni kuwashawishi wazazi waweze kuchangia chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika Mheshimiwa Profesa Kitila ni Mwalimu mwenzangu, atakuwa ameandika historia kama atajenga mabweni kwa ajili ya watoto wa nchi hii katika sekondari zote hapa nchini, ambapo tutakuwa na uhakika kwamba watoto wetu watasoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni viwanda vya kimkakati. Tuna historia, vimekuwepo viwanda vingi vya kutosha. Kulikuwa na *Mwanzatex, Sunguratex, Mwatex* na kadhalika. Viwanda hivi vilikuwepo na vilikuwa vinatoa huduma, sasa viko wapi? Kwa hiyo niombe viwanda vilivyokuwepo vikarabatiwe vianze kutoa huduma kwa jamii yetu, lakini viwanda vingine vipya ambavyo vinakwenda kujibu changamoto za wananchi vijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Kitila anatoka Singida. Eneo lile ni wazalishaji wazuri sana wa asali, hebu tujenge Kiwanda cha Kuchakata Asali pale ili tuweze kufaidi matunda yanayotokana na asali.  Mkoa wa Kigoma ni wakulima wazuri wa chikichi, hebu tujenge kiwanda kikubwa kizuri ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchakata chikichi na kutoa mazao

mbalimbali. Yako maeneo mengine kama Mkoa wa Simiyu ambao ni wakulima wazuri wa pamba, hebu tujenge kiwanda kizuri kikubwa ambacho kitakuja kutoa huduma kwa wananchi wale kwa kutengeneza bidhaa ambazo zinatokana na zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili tutakuwa na uhakika kwamba, vijana wetu wataajiriwa katika viwanda. Vile vile, tutakuwa tumejibu suala la mazao yanayopatikana na kuweza kupata faida zinazotokana na mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeshika *microphone*, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kamamba. Nilimtaja Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Iddi Kassim, Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Daimu Mpakate wajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika hotuba iliyoko mbele yetu. Kabla sijajua nichangie nini, nimefikiria sana nini cha kuongea. Nimepitia Mipango, lakini pia nikapitia na *documents* ambazo zimepita za miaka iliyopita, kwa hiyo nikashindwa kujua nianzie wapi, kwa sababu vitu ni kama vilevile tumeshavisema. Naweza kuwa nimechukua hotuba za miaka sita tofauti niliyochangia huko nyuma nikajikuta nakuja na kitu kile kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumefika hapa? Ni kwa sababu vitu vingi tunavyokuwa tunavishauri pengine hatupewi *feedback* ya kati ya moja, mbili, tatu ambayo nilishauri je, mrejesho wake uko wapi? Kwa sababu tunajikuta tunarudia mambo yaleyale, kwa hiyo, nilikaa nikawaza hivi nishauri nini? Hasa nikiwa namshauri Profesa Msomi ambae wakati mwingine sisi tukiwa vijana tulikuwa tukimuona na tulikuwa tunatamani kuona hawa wasomi wanaweza kulisaidia nini Taifa. Kwa hiyo, nikajikuta sielewi nishauri nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaja kugundua kuwa changamoto ya hii nchi haijawahi kuwa mipango. Changamoto ya hii nchi haijawahi kuwa Wataalam. Mnaweza kuandika vizuri, mnaweza ku-*document* vizuri, mnaweza ku-*copy* na ku-*paste* vizuri mwaka hadi mwaka lakini matokeo hayapigi kelele. Matokeo yanaonekana kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, maandiko ambayo tumekuwa tukiandika ni dhahiri kwamba tumekuwa tukiyasema hapa na wakati mwingine hayatekelezeki. Pengine hatujagundua changamoto ni ipi. Nikasoma kuna Mwandishi mmoja wa Kitabu anaitwa James Clear ameandika kitabu kimoja kinaitwa *The Atomic Habits,* katika hicho Kitabu cha *The Atomic Habits* ameongea mambo mengi, pamoja na jambo jingine wamewahi kulisema Mbunge mmoja hapa akasema; "*You can't repeat the same things blindly and expect to become exceptional*". Hatuwezi kufanya mambo yaleyale, wakati ule ule, maneno yale yale na tukategemea tutapata mabadiliko. Pia, mimi nikagundua, pengine kuna kitu tunapaswa kukifanya tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikwenda kusoma sehemu nyingine akaeleza kwamba, akatoa mfano wa timu ya *cycling* ya waendesha baiskeli wa Uingereza anasema: *it took them one hundred years to realize the difference*. Yaani walikuwa wana-*train*, wanafanya kila kitu *lakini it was after one hundred years* kugundua wanakosea wapi. Kwa hiyo, mimi naanza kuwaza kwamba, pengine kuna kitu ambacho hakiko sawa ambacho tumekuwa tukikitumia kutafuta au ku-*bridge the gap.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kitu nilichokiwaza ni kwamba, *we need to change our mindset.* Lazima tubadilike namna ambavyo tunafanya mambo. Hatuwezi kufanya mambo kwa mazoea kwa kurudia yale yale na tukategemea matokeo tofauti, huo ni uwendawazimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho nilikiona, tunapaswa ku-*strengthen institution.* Leo tumekuja, wiki iliyopita

tulijadili hapa Bungeni kwa ku-*bust* tukiongelea changamoto nyingi ambazo zimejitokeza kwenye taasisi za umma, upotevu wa mapato, ufujaji wa fedha, tunaweza nini kutoka hapa? Tutaweza kuongea nini kwenye Mpango ambacho hakijakuwepo kwa miaka yote? Kwa hiyo, tunahitaji ku-*strengthen institution* ili tuweze ku-*move* kutoka tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizi *institution* ndipo nataka nione Mpango unaongelea nini katika kuhakikisha hizi taasisi zinakuwa imara, kusimamia mapato na kusimamia fedha za walipa kodi ili tuweze kupata matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma vitu vingi ambavyo vimekuwa vikichangiwa kwa miaka mingi, kwa sababu sielewi nieleze kitu gani kipya. Watu wengi wanaeleza mfano natolea changamoto ya *NIDA*. Nikawa nawaza pengine tueleze umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa, watu wakipata vitambulisho wataweza kuhusishwa kwenye mfumo wa fedha, kupata mikopo kwenye mabenki na kuunganishwa na bima. Leo tunakuja na Bima ya Taifa lakini watu hawana vitambulisho! Nikarudi kusoma, inaonekana katika Mwaka wa Fedha ni vitambulisho zaidi ya milioni 1.5 ambavyo vimezalishwa, lakini katika miaka 15 ya uanzishwaji wa *NIDA,* vitambulisho vilivyozalishwa ni milioni 12 *only,* licha ya kwamba kuna watu milioni 24 wenye namba ambao naona bado ni asilimia ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikarudi nikasema, hivi sisi tunashida gani? Changamoto yetu ni nini? Nikarudi pale pale. Baada ya kusoma, wanayo mitambo au mashine zenye uwezo wa kuzalisha vitambulisho 4,500 kwa saa, lakini kwa *statistics* zinavyoonyesha, ina maana kwa siku wanaweza kuwa wanazalisha vitambulisho 990 tu. Kwa hiyo, unaona shida siyo mipango, shida siyo nini, ni ku-*change the way we are thinking* na hapo ndipo tutapo-*move* tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaenda kwenye eneo lingine, tunaongelea kilimo. Kilimo ambacho leo kinaajiri kwa mujibu wa

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 unaajiri zaidi ya watu zaidi ya milioni 65 lakini hao hao watu milioni 65 wanachangia kwenye Pato la Taifa asilimia 28 tu. Kama huwezi uka-*transform economy* ambayo inagusa watu wengi huku kote itakuwa ni *mark time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakuwa mnakuja mnapanga mipango mizuri, upembuzi yakinifu, mchakato, tutakuwa na vitabu vizuri lakini hatutatoka hapa. Kabla hatujatoka hapa, nilitamani niwaulize swali. Kuna mtu hapa humu ndani hajui tumekwama wapi? Yaani ni kitu gani tukikifanya tunaweza ku-*move* tukaenda mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nani hajui kwamba watu wengi wanachepusha fedha za umma? Nani hajui? Kila mtu anajua lakini tumechukua hatua gani? Pia, hii sasa nitoe wito kwa Waheshimiwa Mawaziri, kila mmoja kwenye eneo lake, *just make the impact*. Kila mmoja akiona anasema huyu ni Waziri wa Kilimo. Mtu akiwaza kuwa Waziri wa Kilimo, awaze namna ambayo watu watapeleka majembe kwenye ma-*godown na s*asa tunakwenda kuwa na *mechanized ways of agriculture*. Japo sasa naacha kueleza changamoto nyingi ambazo ziko kwenye maeneo yao, lengo langu ni kuwaza namna ya ku-*change mindset* ili tuone tunaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea sasa kilimo lazima tuangalie tunawezaje ku-*include majority* katika kuzalisha uchumi. Mipango mingi tunayoipanga kama haigusi watu wengi hawawezi kutaka kushiriki kwenye *system* ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea hususani ujenzi wa barabara na hapa nataka nieleze changamoto nyingine. nitakueleza nini Mheshimiwa Profesa? Nitakueleza nini, hujui kwamba, hii nchi inalipa riba kubwa za wakandarasi kwa sababu ya kuchelewesha kuwalipa? Kuna miujiza gani itatokea kama hatulipi madeni kwa wakati tunakuwa tunalipa riba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu niliyejaribu kum-*quote* alisema, unahitaji *one percent of change*. Katika kila unachofanya kila siku onesha *a slight one percent* ya *change, a*nasema baada ya mwaka unaweza ku-*attain a certain level of change* na kubwa, hicho ndicho tunachokihitaji kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *good administration,* namna ya kusimamia mahusiano tunayoyafanya ya kibiashara. Hii nchi imeumia kwa kiwango kikubwa kutokana na mikataba mingi ambayo imewahi kuwekwa na wapiga *deal* wanaotoka tunaita *Multinational corporations,* wanakuja na *foreign direct investment.* Wameshajipanga namna ya kututengenezea au kuingia nao mikataba, kesho tunakuja ku-*default* tunalipa *billions and billions of monies,* hapo tunapaswa kushauri nini kipya ambacho sisi hatukijui humu ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokihitaji ni *mindset*. Tunachokihitaji ni kuamua, *where do we want to go after five years? Where do we want to go after ten years.* Hiyo kama haitoshi na hiyo wameuliza kwenye taarifa ya Kamati. Tunaambiwa tumejenga barabara, tumefanya moja, mbili tatu lakini hivi vitu vinakuwa havitamkwi. Tuseme kwa mwaka 2022, tunakuja kwa mwaka huu tumejenga kilometa ngapi za lami ili baada ya hapa tuseme sasa baada ya hizi kilometa tunakwenda ku-*compound* na kuongeza nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mpango unasema tunazalisha ajira kiasi gani na hizo ajira zinapatikanaje? Hivyo vitu tukivifanya kwa idadi yake na utimilifu wake, tukivifanya kwa kuvi-*quantify* tunaweza kuona mabadiliko ambayo yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninadhani kwamba, tukijikita kwenye mabadilko na tukijikita kwenye kuwekeza kwenye uchumi ambao ni *inclusive*, uchumi wa kilimo, uchumi wa ufugaji, uchumi wa viwanda lakini vilevile watu wanalima ni lazima tupate masoko, tu-*attract* kupata *forex* kupata *foreign exchange* kwa ku-*export* nje. Leo Kagera tunalima Kahawa nadhani jana niliuza swali, tunapolima

hizo Kahawa zenyewe hauoni kwamba tunafaidika vya kutosha kwa sababu hatuwezi ku-*attract* wanunuzi wazuri wenye fedha waweze kutupatia bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa hayo machache nashukuru sana na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest. Nilimtaja Mheshimiwa Iddi Kassim, Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Bahati Kombo wajiandae.

**MHE IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana n mimi kunipatia fursa hii leo kuchangia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku ya leo na mimi kushiriki kutoa mchango. vilevile, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Viongozi wote kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza Serikali lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kuona sehemu ya Mpango huu ni kwenda kukamilisha miradi ya kimkakati ambayo inaendelea ikiwa ni pamoja na Bwawa la Mwalimu Nyerere, Ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge Railway*. Nipongeze sana kwa hatua hizi za kuipa miradi hii kipaumbele cha kwenda kukamilika, kwani tunafahamu kabisa ukamilishaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere utaenda kuwa ni kigezo kikubwa sana cha kuokoa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Mwanza na Mikoa mingine tunategemea sana ukamilishaji wa mradi huu wa reli ya kisasa ambayo itasaidia sana kuinua uchumi wetu kwenye maeneo yetu huko tuliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Msalala ni wakulima wazuri sana wa zao la Mpunga, tunatarajia na tunategemea sana masoko ya nje, masoko ya Dar es Salaam na maeneo mengine. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kuwekwa kwenye mpango wa ukamilishaji wa ujenzi wa reli hii ambayo itatoka Dar es Salaam - Mwanza kupitia Isaka, itaenda kuwa ni jambo kubwa sana katika kuhakikisha inainua uchumi wa Isaka na uchumi wa Jimbo la Msalala ambao utawezesha wananchi kusafirisha mazao yao kwenda sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye suala zima la Mpango ambao umetajwa hapa kwamba, moja ya jambo kubwa ambalo litazingatiwa kwenye Mpango huu ni kuhakikisha kwamba fedha nyingi zinaenda kutengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba unaenda ku-*support* sekta ya kilimo na Kaka yangu Bashe yuko hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nishauri kwenye huu Mpango. Tumeona kwamba Serikali itaendelea kutoa Ruzuku lakini *why* ruzuku kwenye mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba, mimi nimejaribu kufanya *research* sana. Hapo zamani tutakumbuka tulikuwa na mfumo wa uagizaji mbolea kwa pamoja, mfumo huu ulikuwa unapelekea sana kuweza kununua mbolea kwa pamoja na ulipelekea sana kutoa bei ya kununua mbolea moja kwa moja kiwandani ambayo bei yake ilikuwa chini. Baada ya hapo ule mfumo uliondolewa na ukarudi ule mfumo wa kwenda kununua mbolea kwa bei ya soko ya siku hiyo ya dunia, ambayo kimsingi utaona kabisa kwamba, kuachana na mfumo huu wa uagizaji mbolea kwa pamoja na kwenda kununua mbolea kwa bei ya soko maana yake kuna *gap* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya utafiti mdogo tu kwa mwaka 2022 nikagundua kwamba, kwa bei ya kiwandani unaweza ukapata kuanzia bei ya 400 mpaka 600. Wakati huo huo ukienda kunua kwa bei ya soko unapata kuanzia kiasi cha shilingi 800 mpaka 1,000. Sasa tatizo langu na changamoto yangu hapa ni kwamba, tumeacha mfumo ambao tungenunua mbolea kwa bei rahisi kabisa ambapo kimsingi kusingekuwa na haja ya kuongeza ile shilingi 100 ya ruzuku na tukaacha mfumo ule na kwenda kununua bei ya soko ambayo ni kubwa ambayo inaanzia 800 mpaka 1,000. Sasa hii shilingi 100 ambayo tunaongeza, kumbe tungeweza, kuwepo kwa mfumo huu tungenunua kwa bei ya kiwandani moja kwa moja na tukaokoa fedha ambayo tunaenda kuiweka kwenye ruzuku ambayo fedha hii ingetumika kwenda kuwakopesha vijana, kwenda ku-*support* shughuli za kilimo na kuwanunulia vifaa vijana wetu ili waweze kufanya shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninapendekeza kwenye Mpango huu, nimuombe Mheshimiwa Waziri aende akapitie upya kuona kama mfumo huu uliokuwa unatuwezesha kununua mbolea kwa bei rahisi uweze kurejeshwa ili tuweze kuokoa fedha ambayo kimsingi inapotea huku.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Haya, Mheshimiwa Bashe.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Iddi. Serikali haijaacha mfumo wa *bulk procurement* na mpaka sasa tunatumia mfumo wa *bulk procurement* na tunatangaza *pre-qualification* mwanzo wa msimu, makampuni yakipatikana yanaingia kwenye *tendering procedure* na baada ya hapo tunayaruhusu kuendelea ku-*import* kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba naipokea taarifa lakini kwa kusisitiza kwamba, kwa sababu kwenye bajeti iliyopita Mheshimiwa Waziri nafikiri ulisimama hapa na kutuelekeza kwamba tumeanza kununua mbolea kwa bei ya soko. Ule mfumo nafikiri kipindi hicho wakati unaingia uliondoka, kama umeundwa basi uendelee kuboreshwa mfumo huo wa kuagiza mbolea kwa pamoja ambao utasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunanunua mbolea kwa bei ya soko kwa maana ya *bulk procurement,* tuone sasa namna ya kutokuweka fedha ya ruzuku kwenye eneo hilo kwa sababu mbolea tutakayoenda kununua itakuwa ni ya bei ya chini, bei ya *bulk* na bei ya kiwandani ambayo itatusaidia sisi kuokoa fedha na fedha hiyo kwenda kuitumia kwa kuwapa vijana wetu waweze kununua vifaa vya kilimo kwenye maeneo hayo ya kwetu hususani Msalala na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la madini. Ni kweli Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa fedha amelalamika juu ya taratibu za ukusanyaji wa mapato kwamba, watu wengi wamekuwa wanakwepa kulipa kodi. Ni kwa nini? Tukae tujiulize hivi ni kwa nini watu wanaamua kutafuta njia za kukwepa kodi? Ni kwa sababu ya mazingira ambayo tumeyaweka. Mimi ninaamini kabisa kuwa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, yuko hapa na ni Profesa. Ninakuomba sana Mheshimiwa Profesa, ni wakati umefika sasa wa kukaa chini na kujiuliza ni kwa nini mtanzania hayuko hiyari kulipa kodi mwenyewe? Ni kwa sababu ya mazingira magumu ambayo sisi wenyewe tumewajengea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba kwenye huu Mpango ambao tunaenda kuupitisha hapa, mje mtuoneshe kwamba ni vema sasa ikafika hatua mje mtuoneshe kwamba ni vema sasa mkaanza kuongeza wigo wa walipa kodi wengi lakini pia kupunguza baadhi ya kodi ambazo zitawapelekea hawa wawekezaji na wafanyabiashara kwenda kulipa kodi kwa hiari. Kwa sababu itakuwa ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona nchi kama vile Kenya na maeneo mengine kuna baadhi ya bidhaa ambazo zimepunguziwa kodi. Mathalani nichukulie suala zima la *Oil (Lubricant)*. Utaona leo hii kuna viwanda vingi sana vinahama hapa wanaenda ku-*invest* Kenya, kwa nini? Kwa sababu ya kodi nyingi ambazo zimewekwa na watu wa *TRA*. Sasa nimuombe Mheshimiwa Kitila Mkumbo ushauri ni kwamba kwenye Mpango huu unaokuja hapa tuone namna bora ya kwenda kuongeza walipakodi wengi, lakini pia tuone namna ya kuleta mabadiliko ya Sheria ya kuondoa hizi kodi mbalimbali ambazo ni kikwazo na zitawapelekea wananchi wetu kuwa na hamu ya kulipa kodi wenyewe bila shuruti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nizunguimzie kwenye suala zima la biashara. Mheshimiwa Kitila Mkumbo hapa naomba unisikilize kidogo. Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha za kujenga *VETA* kwenye kila Wilaya, mimi kwenye Wilaya ya Msalala tayari fedha zipo na kile chuo kinaendelea. Lengo ni nini? Lengo ni kuwaandaa vijana kwa kuwapatia ujuzi ili waweze kujitegemea kwa kufungua viwanda na biashara zao mbalimbli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachokiona hapa kwenye huu Mpango, Mheshimiwa Kitila Mkumbo, utaona kabisa kwamba mmezungumzia habari ya kuweka mazingira bora ambayo yataleta ushindani wa uwekezaji. Sasa swali langu nataka niulize hapa Mheshimiwa Kitila Mkumbo naomba hapa unielewe kwamba ni wakati sasa umefika mwananchi ambae sisi tumemsomesha, tumempa ujuzi, tunaenda kumlinda vipi kwenye *competition* ya masoko ambayo kwa sasa utaona kabisa wawekezaji wa nje wamekuwa wakija hapa? Pia ukisimama hapa utakapokuwa unahitimisha utueleze, hivi tafsiri ya huyu mwekezaji wa nje anatakiwa kuja ku-*invest* hapa Tanzania kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani Mama Samia Suluhu Hassan anatupatia fedha nyingi, tunajenga *VETA,* watu wanakuja wana ujuzi lakini wanapoingia sokoni wanashindwa kwenda kwenye ushindani kwa sababu leo hii utaona mtu

amejifunza ushonaji, anashona mapazia lakini leo tumeleta mwekezaji ambaye ni Mchina, nae anakuja anafungua mapazia! Maana yake ni kwamba *raw materials* za huyu na utengenezaji wake atatengeneza kwa bei rahisi lakini huyu atatengeneza kwa bei kubwa, hapo *competition* iko wapi? Tunamlindaje mwekezaji wa ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuende tukaweke mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba tunawalinda wawekezaji wetu wa ndani. Pia tuweke ukomo wa wawekezaji hawa, ili mwekezaji aje kuwekeza hapa Tanzania ni lazima tuzungumze kwamba, habari ya wewe umetoka huko umekuja kuwekeza hapa mapazia, Hapana! Kazi ya mapazia ifanywe na Mtanzania, habari ya wewe kuja hapa unauza viatu, Hapana! Viatu vizuwe na mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuweke ukomo kwa wawekezaji wa nje wajue ni kiasi gani cha *capital* kuja ku-*invest* hapa Tanzania ili tuweze kulinda viwanda vya ndani na tuweze kuwasaidia wakina mama ambao wamejifunza kutengeneza sabuni ambao wanakosa soko la sabuni kwa sababu tumekaribisha wawekezaji hao hao kwa mitaji ile ile wanatoa sabuni nje na kuleta hapa kwa bei rahisi. Matokeo yake ni kwamba, wakina mama wanakosa soko la kuuza bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, tumeona kwenye mafuta. Mheshimiwa Bashe, nikuombe sana kwenye suala la mafuta, ukienda hapo Singida utaona viwanda vya mafuta ambavyo wanazalisha mafuta, sasa, ifikie kipindi Waziri kukaa na ku-*allocate* maeneo ambayo ni *potential* kwa *economic*. Kwa mfano unaweza ukachukua Singida…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi, muda wako umekwisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Bahati Kombo, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Nicodemus Maganga na Mheshimiwa Mariam Nyoka, wajiandae.

Mheshimiwa Neema Mwandabila hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii nami niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa namna ambavyo wameweka vizuri hoja yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nitakwenda kwenye ukurasa wa 20 wa hotuba ya Waziri wa Mipango ambayo ameeleza malengo ya jumla ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 kwenye *item* namba sita ambayo ameeleza kuwa, moja ya malengo ya jumla ni kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga, maji na utunzaji endelevu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye suala hili katika maeneo matatu. Moja, ni Bandari ya Mtwara; pili, ujenzi wa reli ya Kusini; na tatu ni suala la ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani - Nalasi mpaka kufika Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuiboresha Bandari ya Mtwara ambayo sasa ina hadhi kidogo ya kuweza kusafirisha mizigo mingi. Pia tunashukuru kwa kutoa tamko rasmi kwa kutumia kusafirisha korosho zote zinazolimwa kusini kwa kutumia Bandari ya Mtwara. Tunamshukuru sana kwa sababu anafanya jambo jema. Ukweli uchumi wa Mtwara na wa Kusini kwa ujumla ulikuwa umedorora, umepelekwa Dar es Salaam badala ya vijana wetu kufanya kazi katika maeneo ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, Bandari ya Mtwara ilitanuliwa ikiwa na malengo kadhaa. Moja ya maelengo ni kuweza kuitumia Bandari ya Mtwara kusafirishia mizigo na wenzetu wa jirani hasa Malawi. Pamoja na kusafirisha mizigo ya Malawi, haiwezi kutimia kwa sababu Bandari yetu kwa sasa inatumika kwa *items* mbili tu. Moja ni suala la kusafirisha Korosho na la pili ni suala la makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Bandari hii ifanye kazi vizuri, tunahitaji Mpango wa kuweza kutengeneza meli ambayo itafanya kazi katika Bahari yetu ya Hindi ili vijana wetu wa Mtwara, Lindi, Tunduru, na Songea waweze kusafirisha bidhaa mbalimbali kwenda Comoro ambako sasa kuna fursa nyingi sana. Watu wa Comoro wanapata bidhaa nyingi, mpaka nyanya na nazi zinatoka Bara. Kwa hiyo, nilidhani Mpango huu ungeweza kujieleza na kujifafanua vizuri kwa kujenga meli ambayo itatoa huduma kwenye Bahari ya Hindi kwa ajili ya kusafirisha mazao mbalimbali pamoja na Kiwanda kikubwa cha Dangote kupeleka *cement* yake sehemu tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili, Bandari hii ili ifanye kazi vizuri, tunatakiwa tufungamane na ujenzi wa reli ya Kusini. Ujenzi wa reli ya Kusini lengo lake ni kutoka Mtwara – Tunduru - Songea mpaka kufika *Mbamba Bay* kwa ajili ya kusafirisha makaa ya mawe kutoka Ngaka, Chuma kutoka Mchuchuma na makaa ya mawe kutoka Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya mipango yetu ya kuendeleza Liganga na Mchuchuma, lazima twende sambamba na mipango ya kujenga reli hii ili iweze kusaidia kubeba mizigo mikubwa ambayo inategemewa kuzalishwa katika viwanda hivi viwili kwa maana ya mradi wa Mchuchuma na Liganga pamoja na hii ya Ngaka ambayo sasa hivi inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia; moja, barabara zetu zisiweze kuharibika kwa haraka, kwa sababu magari mengi sana ambayo yanatumika kusafirisha makaa ya mawe yanapita kwenye

barabara hii. Pale Songea peke yake kwa siku ni zaidi ya malori 2000 yanapita ambayo yanabeba makaa ya mawe kwa ajili ya kupeleka Mtwara na Dar es Salaam pamoja na yale mengine yanayoenda Rwanda, Burundi, Kenya na mengine yanapita hapa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ikijengwa nadhani itasadia kwa asilimia kubwa makaa ya mawe yote kusafirishwa kwenye reli ili yaweze kufika Mtwara na Mtwara kusafirishwa kwa Bandari kwenda maeneo mbalimbali ambako bidhaa hii inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na suala la barabara, naomba sana kwenye Mpango huu, kuna barabara ya Mtwara - Pachani, inaenda Lalasi mpaka Tunduru; iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tayari imefanyiwa upembuzi yakinifu imeisha tangu 2020 na huku kuna kiwanda ambacho kinaanza kujengwa mwakani ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchangiwa *Copper* tani 500 kwa siku pale katika Kijiji cha Mbesa ambako mwekezaji huyu *MUST* pamoja na *CC Company* ya Marekani wanatarajia kujenga kiwanda kikubwa chenye thamani ya Dola milioni 15 ambayo ni zaidi ya shilingi trilioni 30 ambapo wataanza uzalishaji na ujenzi utaanza mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ambayo inapitia Mbesa mpaka Tunduru Mjini ina kilomita zaidi ya 50, inaweza kusimamisha au kufanya mradi huu utekelezeke kwa ugumu kwa sababu ya kutokuwa na barabara nzuri. Kwa kweli kama Mipango yetu itaenda vizuri na barabara hii ikatengenezwa, *copper* inayotegemewa kuchenjuliwa pale ni kubwa sana, kiasi kikubwa kinaendelea kuchenjuliwa na wafanyakazi wengi wanahitajika kwenye kiwanda kile ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua kwa kutumia *copper. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hii, tunaomba sana Barabara ya Songea – Makambako. Hii barabara ni ya muhimu sana. Mwaka 2022 kwenye bajeti mlizungumza kwamba mtaanza kuijenga upya, ina zaidi ya miaka 30 tangu

imetengenezwa mwaka 1985, mpaka leo ni miaka zaidi ya 30. Barabara hii imechoka, na pamoja na kuchoka inapitisha magari makubwa mengi ambayo yanabeba *copper*, inabeba makaa ya mawe kwenda sehemu mbalimbali za nchi yetu pamoja na nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwenye Mpango huu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tuongeze kipande kingine cha kutengeneza ili barabara ile ikamilike iweze kubeba mizigo hii kwa uhakika zaidi. Pamoja na barabara hii tunaomba kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma tuwe na *plan* au Mpango wa kuhakikisha kwamba kuna reli inatoka Makambako kwenda Ludewa ili hii chuma kwa muda iweze kusafirishwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nategemea nilizungumzie, ni suala la matumizi ya gesi ya Mtwara. Kama walivyozungumza wenzangu, gesi ya Mtwara tunayo ya kutosha, sasa tunatumia karibu asilimia 10 tu ya gesi ile. Tunashindwa kutengeneza mbolea. Kwa nini, wakati gesi tunayo? Mipango hii ni ya muda mrefu, tulikuwa tunategemea Kilwa waanze uzalishaji wa Kiwanda wa Mbolea, lakini mpaka leo tunakwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba Mpango wa kuweka Kiwanda cha Mbolea Kilwa uendelee ili tuondoe hili tatizo la upatikanaji wa Mbolea. Pamoja na suala la mbolea, kuna matumizi ya gesi kwenye magari na ujenzi wa Kiwanda cha *LNG* pale Lindi. Ni aibu kubwa sana kwa nchi yetu. Tunayo gesi nyingi, lakini tunalalamika mafuta ya *diesel* bei kubwa, wakati tunayo *Natural Gas* ambayo inaweza ikatumika kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya kuendesha magari yetu barabarani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Niliwataja Mheshimiwa Bahati Kombo, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Mariam Nyoka na Mheshimiwa Nusrat Hanje, ajiandae.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache jioni hii. Kabla ya mchango wangu, naomba niseme jambo moja; nawapongeza wanachama wenzangu wote wa timu ya Simba kwa uvumilivu mkubwa ambao tumewaonesha watani wetu wa jadi. Tunasema kwamba mambo ni kangaja, huenda yakaja. Tuliwahi kuwafunga sita bila, kwa hiyo, sisi tutaendelea kukaza kamba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati, endelea na mchango wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee katika mchango wangu. Nitajikita katika viwanja vya ndege. Pamoja na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika na Serikali, bado tuna changamoto kubwa katika viwanja vyetu vya ndege ambavyo ni viwanja vya mkakati. Viwanja hivi ni kama vile Arusha, Bukoba na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Arusha ni kiwanja ambacho kinatupatia fedha nyingi katika Taifa letu, hasa katika sekta yetu ya utalii. Kwa kweli tunakosa mapato makubwa ambapo hakuna miundombinu wezeshi, watalii wengi huondoka, yaani hukaa pale kwa muda mchache na hivyo yale mapato tunayakosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya Mpango wa Maendeleo ya Serikali inaonekana kwamba mradi Na. 42 (26) unaohusu uboreshaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa, jumla ya shilingi bilioni 18.53 zimetumika katika mwaka 2022/2023, vilevile

shilingi milioni 699.99 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024. Hakuna fedha ambayo imeelekezwa katika kiwanja kile cha Arusha. Naiomba Serikali iangalie kwa kina suala hili, kwani tunakosa mapato makubwa katika sekta hii ya utalii. Pia nampongeza sana Mama Samia kwa kukuza utalii nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika Mfuko wa *TASAF*. Mfuko huu wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ulianzishwa mwaka 2000 ukiwa na lengo la kuondoa umaskini. Sote ni mashuhuda kwamba mfuko huu umewawezesha wananchi wengi kujikwamua kimaisha. Naiomba Serikali iendelee kuusimamia mfuko huu ili wananchi waweze kuendelea kujikwamua kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Taarifa ya Serikali inayosema kwamba katika mwaka 2022 jumla ya shilingi bilioni 1.78 zimetumika katika ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu. Kwa kweli Mwanasheria Mkuu anafanya kazi kubwa, lakini sasa katika mikoa yote kuna mikoa minne tu ambayo ana ofisi zake. Naiomba Serikali kuangalia kwa kina kuweza kuweka ofisi hizi angalau kila Kanda Ofisi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mdogo. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bahati Kombo, nilimtaja Mheshimiwa Rashid Abdalla, ajiandae Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kukupongeza wewe kwa kunipatia nafasi wakati huu ili niweze kuchangia mchango huu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na kufikia kutuwekea mpango huu Mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kupeleka fedha kwenye miradi mingi hapa nchini. Kadhalika, nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutekeleza miradi mingi ikiwemo ya afya, kilimo, elimu, miundombinu ya maji na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuwa Mwanamke wa kwanza Afrika kushika nafasi hii ya Urais wa Mabunge ya Dunia ambapo ni kielelezo kikubwa cha dunia kwamba Spika wetu anatosha. Hii ni dhahiri kwamba analiongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo maana akaweza kwenda kushinda kwa kishindo kule Angola na kuliletea heshima Taifa letu, Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na heshima pekee aliyojiwekea yeye mwenyewe kwamba hii ni alama kuwa ambapo mpaka ataondoka duniani, heshima hii itakuwa inaonekana na kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu huo na hasa hapo nilipokuwa kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia, katika Mpango ambao umepangwa kutekelezwa, moja ni miundombinu ya Ofisi ya Bunge. Kwanza tushukuru kwamba Ofisi ya Bunge tayari imeshakamilisha kazi ya kukamilisha daftari la utathmini la wananchi ambao wanamiliki maeneo katika eneo la Bunge. Kazi hii imeshakamilika, lakini sasa hapa niombe tu kwamba Serikali ikamilishe haraka utengaji wa fedha kwenye huo mpango ili kazi hiyo ikamilike kwa wakati na tusije tukachelewa kumaliza ile miezi sita bila kukamilisha tukaja tukapata hasara nyingine ya kurudia kufanya tathmini nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha kazi hiyo ya tathmini, tunaona Bunge letu ni Bunge la viwango, ni Bunge linaongozwa na Rais wa Mabunge ya Dunia. Kuna haja kubwa sasa ya kutekeleza ujenzi wa Ofisi za Bunge kwa hapo baadaye. Tunajua

kwamba penye ofisi zetu za Bunge hapa wafanyakazi ni wengi, lakini ofisi ni chache. Kadhalika, hatuna maeneo ya *parking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia wenyewe hapa, Wabunge tunaweka magari yetu katika maeneo mengine ambayo siyo salama, na inafikia wakati mwingine Wabunge magari yao yanaibiwa vifaa kutokana na upungufu wa eneo kubwa la kufanya *parking* za magari yetu. Halikadhalika, hatuna maeneo kwa maana ya sehemu ya kufanya shughuli zetu za Kibunge, tunapata matukio mengi ikiwemo misiba, hatuna eneo lile la ku-*park* magari katika eneo letu hili la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku nyingine tunapata faradhi za misiba, tunaaga miili hapa mbele ya Mlango Mkuu wa Bunge, lakini kama tungekuwa tuna nafasi kubwa, tungeweza kufanya shughuli zetu vizuri na hata hii shughuli ya leo ambayo Wabunge tumeridhia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia, basi ingefanyika katika eneo kubwa na zuri ambalo lina hadhi ya Bunge linaloongozwa na Rais wa Mabunge ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika mchango wangu wa pili, ni sekta ndogo za fedha *(microfinance)*. Katika eneo hili tunajua kwamba Benki Kuu ya Tanzania imetoa leseni 1,307 na kusajili vikundi vya akiba na mikopo kwa idadi ya 42,257. Pamoja na uwepo wa sheria katika sekta hii ya fedha, lakini kuna baadhi ya upungufu na ambapo sheria hizi zinahitaji kusimamiwa. Taasisi za fedha za maeneo madogo madogo zina changamoto mbalimbali. Wananchi wetu tunajua hali zao zilivyo, wengi wanapendelea kukopa katika hizi taasisi, lakini taasisi hizi zina usumbufu mkubwa sana kwa wakopaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia wananchi wetu wakienda kunyang'anywa mpaka vitanda, kwa kuwa ndiyo ambavyo waliweka dhamana, sababu tu ya kutolipa kwa wakati au kuchelewa kufanya malipo, lakini jambo hili ni kwamba sheria hizi ambazo zimetungwa za hizi taasisi za fedha zinahitaji Serikali isimamie ipasavyo ili wananchi wetu waweze kupata hizo huduma

katika hizo taasisi, lakini na kiwango kikubwa cha riba ambacho kinatozwa na taasisi hizi. Naomba kwa kweli Serikali bado tuzishughulikie. Wanakwenda hadi kwenye asilimia 25 au 24. Ni kiwango kikubwa sana cha riba hii ambayo inatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kuna taasisi nyingine zinatoa mikopo leo na marejesho yanaanza leo leo. Hii kwa kweli ni kuwanyonya, ni kuwadhulumu wananchi. Bado huu siyo utaratibu, wananchi wanakwenda kukopa kwa nia safi, lakini sheria hizi zinaenda kusumbua sana wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu ambalo nataka kuliongelea ni suala zima la michezo. Tunajua Taifa letu linasisitiza michezo kwa kiwango kikubwa na tunaona namna Taifa letu linavyopanda. Timu yetu ya Taifa ya Tanzania inashiriki *AFCON*. Hiyo yote ni kuonesha kiwango kikubwa cha upandaji wa kiwango cha mpira Tanzania, lakini tunaona katika *list* ya kumi bora Afrika tunaikuta timu ya Dar es Salaam *Young Africans* inashika nafasi ya tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tumeona nafasi hii ya tatu haikupatikana hivi tu kirahisi, juzi tumeshuhudia hapo mtani akila tano, wakianza kugawana, kuvunja timu, kutengeneza utaratibu wa kusimamisha wachezaji. Hili jambo kwa kweli haliridhishi. Hii ni historia tu inajirejea. Tunakumbuka kwamba kabla ya uhuru, simba hawa hawa walipokea kipigo cha bao tisa kwa bila, sita kwa bila; hii yote ni kuonesha Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kukuza michezo nchini inaendelea kwa kasi. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda umeisha.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Anaongea uongo huyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na mjadala wetu, kuna tangazo moja la wageni hapa.

Kuna wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mbunge ambaye na Waziri wa Katiba na Sheria, ambao ni wajasiliamali kutoka Mkoa wa Iringa. Karibuni sana Wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu.

Pia, kuna tangazo ambalo linarudiwa mara pili hapa linatoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kuna *form* kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambazo zitapitishwa punde ili kila Mheshimiwa Mbunge aweze kujaza eneo moja lenye changamoto katika jimbo lake kwa ajili ya kujenga kituo kimoja cha afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa kutoa ushirikiano kujaza fomu hizo leo ili ziweze kurejeshwa Wizarani na kuanza kufanyiwa kazi kwa haraka. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mheshimiwa Nusrat Hanje na Zacharia Issaay, ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mpango wa Bajeti 2024/2025. Namshukuru Mungu muumba wa vyote kupata tena hii fursa ya kuweza kuchangia mchango wangu ili Serikali ikaweze kufanikiwa na mambo ambayo imeyakusudia kwenda kuyafanya kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Profesa Kitila Mkumbo, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya uchakarikaji wake na upambanaji wake tunaamini kwamba kupitia ushauri tunaompa atatutoa hapa tulipo na kwenda sehemu nyingine. Mpango wa Bajeti unaeleza shilingi trillion 47.4 ambao

Mheshimiwa Kitila Mkumbo amekusudia kwenda kuwabadilishia maisha wananchi wa Tanzania hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jimbo langu kule walikoniamini. Kwenye jimbo langu kuna changamoto bado nyingi. Vipo vitongoji havina umeme kabisa, vipo vijiji 87 katika jimbo wananchi wana matumaini kwamba tutaenda kufungua vijiji vyao. Wananchi wana matumaini na tangazo umelipitisha hapo kwamba vituo vya afya kuna baadhi ya maeneo kweli wananchi hawajafanyiwa hivyo. Leo ni miaka 60 na kitu ya uhuru wananchi wana matumaini kutoka hapa walipo. Naomba niiombe sana Serikali iweze kuniangalia kwenye Jimbo langu la Mbogwe ili iweze kuwasaidia wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya hii imekuwa na miaka mingi ikikiamini Chama Cha Mapinduzi lakini ni kweli kwamba kuna mahitaji mengi ambayo bado hayajawafikia. Niwape pole wananchi wangu Kata ya Isebya kwa kufiwa na Mheshimiwa Diwani lakini napenda niwatoe wasiwasi Wananchi wa Isebya, endeleeni kuamini tu Chama Cha Mapinduzi kiko kazini na hakuna jambo litabadilika na mimi msimamizi mkuu wa hilo jimbo niko makini kuliko jana. Kwa hiyo, nitaendelea kusukuma maendeleo kuhakikisha kwamba yanawafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije ya Kitaifa sasa, ya kiujumla jumla. Profesa nina ushauri ukurasa wa 127, nimesoma kurusa zote lakini ukurasa ambao mimi haujanifurahisha ni ukurasa na 127 kwenye hotuba yako. Unasema kwamba umekusudia kwenda kukopa tena mikopo ya bei nafuu. Ni vyema kama Nchi, kama vijana sisi tufike mahali tujiulize sasa tusimame, tunaenda wapi, tunaelea wapi? Mikopo hiyo wakati mwingine tunaikopa inakuwa haina tija. Kwa mfano, unakopa unaenda kujenga shule halafu shule hiyo itazalisha nini na kuingiza nini tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tufikirie tunapochukua hii mikopo tunao wafanyabiashara wa ndani ambapo ukichukua watu hata waliomaliza elimu ya juu hao wenye kiwango cha *degree*

ukawakopesha kama Serikali, kila mtu *at least* hata kama ni milioni 100, 100 akaingia kufanyabiashara na kuingia Serikali faida tunaweza tukairejesha hii mikopo vizuri. Sasa hivi, Profesa mikopo mingi tunadaiwa hii ya bei nafuu, ningekuomba kaka yangu kwenye ukurasa huo namba 127 ikiwezekana ubadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Nchi, hii Tanzania tuna vyanzo vingi vya mapato, ukiangalia kiuhalisia Nchi yetu ina vyanzo vingi sana, tumejaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na maziwa. Tuna maziwa mengi yanazalisha dagaa, samaki lakini tunayo migodi tuna dhahabu. Nikianza kutaja kila *design* ya madini ina maana mpaka hotuba yangu itaisha. Ni vyema tuangalie, changamoto tuliyonayo kubwa Tanzania na naungana na dada yangu, pale amemaliza kuongea, hii mipango ni kama vile ya ku-*copy* na ku-*paste*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mipango tuliyoijadili nyuma inafanafana, changamoto tuliyonayo kubwa Profesa ni usimamizi. Juzi tumejadili habari ya *CAG*, tunaona kabisa bayana watu wanatuibia. Ni vyema sasa kwenye mpango huu tuelezee tumejipangaje kudhibiti wezi wanaotuibia kwenye mapato haya tunayoyatarajia kuyakusanya. Siyo kuongeza tu vyanzo vya mapato lakini usimamizi huku tunafeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye mifumo hii ya eletroniki, tunapigwa sana tu, tena mara mbili yake kuliko hata wakati hata tukiwa *manual*. Ninaishauri Serikali iangalie kila pailipo na eletroniki na *manual* iwepo, ikizimika *POS* mtuandike kwenye daftari kwamba nimechukua hela ya mwananchi hapa kama ni milioni inaandikwa kwenye daftari. Mifumo ikija kufunguka iingizwe hiyo hesabu ya wananchi halafu na penyewe tuone ili kuweza kuepukana na hizi hasara ambazo tunazipata hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipenda Nchi yangu, naipenda Nchi yangu sana natamani tupige hatua kwa haraka kufikia mwaka 2025 ikiwezekana kila Mbunge hapa awe anatoa ushuhuda kwa kile alichokifanya kwenye jimbo lake lakini tukiruhusu huu wizi unafanyika

kwenye *POS* hata hizi shilingi trilioni 47 hatutazifikisha. Kwa sababu mpango ni kitu kingine na utekelezaji nao ni kitu kingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema sasa Serikali mimi niiombe sana, kwanza ijitahidi kutumia mawazo yetu sisi ambao huwa tunafanya. Kwa mfano siyo vya kusomea darasani ni *declare interest*, mimi ni mfanyabiashara niwasilishe hoja za wafanyabiashara nchini hasa wa mafuta wanakabiliwa na changamoto nyingi. Mfanyabiashara huyu akitaka kuanza biashara anakuatana na *TRA* kwa maana ya kwamba akakate *TIN Number* lakini ipo changamoto, cheti cha mazingira, kuna cheti cha *OSHA*, tozo kwenye muamala wake kama ana simu, kuna cheti za zimamoto, kuna leseni ya *EWURA*, kuna leseni za halmashauri, kuna *NSSF,* kuna mambo mengi mpaka muda unaweza ukaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifikirie jinsi gani inaenda kumsaidia mfanyabiashara na *service levy* nimekumbushwa lakini pia kwa watumishi kuna hili jambo la vikokotoo, ni kilio kikubwa na tukiacha kuyasema haya tutakuja kupata tabu sana huko mbeleni. Watumishi hawajakubaliana kabisa na hili jambo, Serikali ni vyema iwasikilize wananchi na iweze kufanya mabadiliko kwenye eneo hilo ili watu waweze kuishi vizuri kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kukushukuru wewe jinsi unavyotuendesha, endelea kunilindia muda wangu, nizidi kuchomekea. Sasa hivi tuko kwenye wakati wa mvua wakulima wanategemea kupata mbolea pamoja na mbegu lakini Wizara nikiangalia kama vile mipango haijakaa vizuri na mimi nimuombe Waziri wa Kilimo, huu ni wakati wa msimu, wakulima wetu wanahitaji mbegu. Mbogwe wanahitaji mbegu, wanahitaji mbolea, sukuma kwenye ofisi yako mbolea iende ili tarehe 10 tunapoenda kumaliza Bunge, mimi nikaimbe iyena, iyena halafu na mambo mengine yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri wa TAMISEMI kwenye eneo langu nina changamoto ya watumishi, aweze kuangalia kwenye halmashauri yangu anipe Wakuu wa Idara ma-

*proper* ambao wanaipenda kazi yao, ambao ni waaminifu, ambao watakuwa na hofu ya Mungu. Kwa kweli mimi Mbogwe na nizungumze kabisa hapa hewani kwamba yaani mtumishi mwizi hatatoka salama Mbogwe, tumejipanga kuhakikisha kwamba tunazuia uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga kuhakikisha kwamba watoto wetu siku wakija kuchungulia hata makaburi yetu waone kwamba kweli kuna watu walikuwa wanasimamia Serikali. Kwa hiyo, nipeni watumishi waliowaaminifu na mimi nitaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba siikwamishi Serikali lakini nitatembea na wananchi wangu kuhakikisha wananchi wangu wanasemaje, wanataka nini ili niweze kufanya kama walivyonituma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mungu akubariki sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicodemas, nilimtaja Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Priscus Tarimo, ajiandae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Mwongozo na Mapendekezo ya Bajeti na Mpango kwa mwaka 2024/2025. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa namna tulivyoshirikiana nao wakati wa uandaaji wa mapendekezo haya pamoja na mwongozo huu mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mwongozo wa maandalizi wa mpango na bajeti ya 2024/2025 ukurasa wa nne, unaeleza vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ya Serikali. Kati ya vipaumbele hivyo, kimojawapo ni mkakati wa kuongeza mapato na usimamizi wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa mkakati huo kwani tunaona dhamira nzuri ya Serikali katika kutekeleza mpango huo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga

kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 47.4 ambapo ni ongezeko la shilingi trilioni tatu ikiwa sawa na ongezeko la asilimia saba ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024. Katika ongezeko hili tumeona shilingi trilioni 1.2 inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa ufanya hivyo tunaona fedha za miradi ya maendeleo inaongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 15.3. Hii ni ishara ya kwamba Serikali yetu ina mpango mzuri wa kutekeleza miradi yetu chini ya uongozi wake imara Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo tunaona miradi mingi ya maendeleo inaenda kutekelezwa nchini ambayo ni chachu ya maendeleo ya wananchi wetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 11 wa mwongozo unaeleza mikakati ya usimamizi wa matumizi, moja ya mkakati huo ni kuelekeza fedha katika kukamilisha miradi ya maendeleo kielelezo na kimkakati kwa kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanza miradi mipya. Hapa ninaomba yatolewe maelekezo kwa ujumla hasa kwa viongozi wanaohamia kwenye taasisi zetu. Tumeona viongozi wengi wakihamia wanaanza miradi yao mipya, kwa kweli hili siyo jambo jema tunaomba miradi ile ambayo ilianzwa ikamilike na pia wataalam wetu wawe washauri wakuu hasa ma-*engineer* wahakikishe miradi inakamilika kikamilifu na kwa wakati na kwa ubora ambao tunautarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yanayoendelea kufanyika hapa nchini kwetu kuna baadhi ya changamoto hasa kwenye upande wa barabara. Kuna utolewaji wa taarifa za ujumla jumla kwenye miradi hii yaani taarifa inatolewa tangu ilipoaanza hadi ilipofikia hii siyo sawa. Kwa sababu tunataka tuone ufanisi wa taarifa zetu kwa mwaka husika. Kama mradi umetekelezwa kipande cha kutoka labda Njombe hadi Songea kwa mwaka huo iripoti hivyo na sio kupeleka taarifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hapo kuna uwepo wa wakandarasi wasio na uwezo. Kwenye hili tumeona miradi mingi

inayotekelezwa inatekelezwa kwa kiwango cha chini na hata kama ikitekelezwa kwa kiwango hiki maana yake pia inachelewa kukamilika. Hii siyo sawa, kwani tumeona mfano kwenye kipande cha barabara ukitoka Njombe kuelekea Songea. Wakati wa kiangazi, jua likiwaka unaona ile Barabara lami imeyeyuka na pia ina sababisha magari yakipita yananasa ile lami yote, sasa hii barabara inakuwa haina ubora. Kwa hiyo, tunaomba wataalamu wetu wawe wazalendo, wafanyekazi kwa kuhakikisha wanasimamia fedha hizi ambazo mama yetu mpendwa anazitafuta kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo kuna changamoto nyingine ya ucheleweshwaji wa malipo kwa wakandarasi. Pamoja na changamoto hiyo, naomba niipongeze Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 70 kila mwezi kwa ajili ya kulipa wakandarasi hawa ili kuweza kupunguza gharama kubwa za riba ambazo Serikali yetu inaipata. Pamoja na hilo ninaiomba Serikali kuhakikisha inachukua hatua kwa wale wote ambao wanasababisha kupatikana kwa hasara hizi ama kwa makusudi ama kwa uzembe. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeweka funzo kwa wataalamu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninaomba Serikali itupe ufafanuzi juu ya vijana wetu waliotoka JKT ambao wamekaa JKT kwa kipindi kischopungua miaka miwili, wamerudi kule majumbani kwetu hawana shughuli za kufanya wako wanahangaika tu hawana maelekezo yoyote. Ninaomba Waziri wa Mipango atakapokuja kuhitimisha atupe maelekezo au maelezo ya vijana hawa waliporudi kule nyumbani wana mpango nao gani ambapo wao ni nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mariam Nyoka, nilimtaja Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ambavyo niliamua kuwa mwanafunzi wa milele *(long-life learner)* kwenye maisha yangu na maisha yangu ya siasa. Nimejifunza kwamba dunia haina changamoto ya matatizo yaani dunia haina upungufu wa matatizo kutoka Kusini mpaka Kaskazini, kutoka Mashariki mpaka Magharibi hatuna chanagmoto ya matatizo lakini tuna changamoto ya utatuzi wa matatizo na watatuzi wa matatizo *(Problem solvers)* na wakati mwingine nilisema nimeamua kuwa mwanafunzi wa milele wa maisha kwenye lila kitu pamoja na uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo wakati naanza siasa, nimejifunza siasa kwenye mazingira ya wakati mwingine unatafuta ubaya hata kwenye uzuri kwa sababu ya aina ya siasa na naomba nisieleweke hivyo lakini wakati tunajifunza kutoka kwa wengine ambao tunawaona wanafanya vizuri kwa sababu kuna watu ambao ni vielelezo vyema na mnawafahamu na wengine wapo humu na wengine ni waalimu wangu wa siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikagundua kuwa siyo wakati wote siyo lazima utoe kasoro kwenye kila kitu, wakati mwingine niliona nijiweke kwenye nafasi ya kuangalia ingekuwa ni mimi kitu gani ningefanya cha tofauti kwenye jambo fulani mahsusi. Kwa sababu siamini kabisa kwamba kuna mtu ambaye ni kiongozi amechaguliwa na watu akapewa mamlaka na wenye mamlaka halafu na yeye yuko na *ambition* kwenye Maisha, yuko na *ambitions* zake kwenye maisha za kisiasa na yeye mwenyewe sidhani kama kuna mtu anataka afeli aonekane kwamba amefeli, sidhani kama kuna huyo mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamimi kabla sijamlaumu mtu ni lazima niangalie je, ame-*exhaust* kiasi gani

*remedies* zote ambazo alitakiwa azifanye, ametumia rasilimalia aliyonayo na uwezo wake wa kufikiri kiasi gani kutatua matatizo yanayomzunguka, ili mimi nifikiri je ingekuwa ni mimi ningefanya kipi cha tofauti, ili nipate uhalali ama nikose uhalali wakumlaumu. Kwa hiyo, natoa mfano huo *specifically*, nafahamu kuna watu ambao wamepewa madaraka na mwenye madaraka yake na wanakesha. Naomba niwape moyo kwa sababu Mungu anajua na ninyi mnajua na watu wanajua kwamba mnakesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa kuna wengine ambao ni *mentors* wangu kwenye siasa. Wengine ni walimu wangu kwenye siasa, tunajua kama mnafanya jitihada na kila mtu humu kuna jitihada ambazo anazifanya kwa sababu sidhani kama kuna mwanaume, mwanamke, mtu mzima mwenye akili timamu ana *ambition* kwenye maisha na anataka afeli, sidhani kama kuna huyo mtu yupo *cause* kwa sababu hata mimi sipo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatambua pamoja na changamoto ambazo zipo ninatambua kwamba mme-*exhaust*. Ninachotaka kukiongea hapa ni kile ambacho ninafikiri ningekifanya ku-*fill* hilo *gap* kwa sababu hii Nchi ni yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ninaamini kuna siku sintokuwepo kwenye hii nafasi kuna mwingine atakuwepo. Wakienda kwenye *Hansard* wakiangalia mimi nilifanya nini kwa nafasi yangu sitatatua kila kitu, hautatatua kila kitu tutasaidiana kutatuta kwa pamoja kwa sabau hii Nchi yetu, hakuna Nchi nyingine, hakuna wananchi wa nchi nyingine watakuja kutatua changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mapendekezo ya mpango, kuna mambo mengi yamezungumzwa lakini nimesoma taarifa ya Kamati nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha; nimesoma mpango na nimesoma na taarifa ya Kamati. Miongoni mwa sababu zilizoorodheshwa kama changamoto za utekelezaji wa bajeti

iliyopita pamoja na matarajio kwamba tunaweza tukakutana na kikwazo gani? Wametaja changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ametaja ukurasa wa 20, 23 na 24 ambako wakati anaeleza nguzo 10 za utekelezaji wa Mpango ambao anau-*propose* sasa hivi, 23 na 24 ameieleza iko namba tano pale, lakini ukurasa wa 20 ameeleza pia kwenye Mpango katika mambo saba ambayo ndiyo malengo makuu ya Mpango huu, yale matano yote ukitoa mawili yote yanaathiriwa na jambo ambalo ni mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu nafikiri kama ana-*anticipate* kwamba hili litakuwa kikwazo alitakiwa aliweke katika mipango. Wasiwasi wangu kwa sababu hata Taarifa ya Kamati inaeleza jambo hili, mabadiliko ya tabianchi limekuwa likiandikwa kwenye taarifa za Kamati pamoja na mipango kwenye upande wa Waziri wa Fedha, lakini upande wa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, lakini hatuna fungu linaloshughulika na masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Sasa siyo kwamba watu wanapenda kuongea ongea tu kulalamika, sasa baadaye kwa nini tusije kulalamika hakuna mpango ambao unaonyesha kwamba hiki umeshakijua kwamba ni tishio katika utekelezaji wako wa mpango na haujakiwekea fungu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Nchi yetu bado inategemea wahisani katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, bado tunategemea kwa kiasi kikubwa wahisani. Sasa siyo sawa kwa sababu anayetoa pesa ndiyo anayechagua wimbo. Nilifikiri ni wakati sahihi sasa katika wakati tunakuja kwenye bajeti tuje na fungu mahususi *(vote)* kwenye Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira linalohusiana na *climate financing* ya ndani ambayo itakuwa inatokana na fedha zetu za ndani siyo kusubiri wawekezaji ili itusaidie kupanga, ili itusaidie kuwa na miradi ambayo sisi tunai-*own* ndani, tuijue tunaipeleka wapi kwa sababu mwekezaji pia anaweza akaja akachagua wapeleke wapi na wakaja wawili, watatu tofauti na wakataka wapeleke eneo moja kwa sababu si yeye anakuwa na hizo fedha na yeye ndiyo anachagua mradi aupeleke wapi?

Kwa hiyo ni muhimu sana kuwa na *vote* (fungu) mahususi la kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende haraka haraka; kundi kubwa tukiangalia kwenye *integrated labor force review* ya mwaka 2021, kundi kubwa la nguvu kazi ya Taifa ni 57% ambao ni vijana, lakini kwenye mpango hapa tumeangalia uwezeshaji wananchi kiuchumi utazungumzwa uwezeshaji wa vijana kiuchumi pekee. Mpaka sasa hivi Ofisi ya Waziri Mkuu masuala ya vijana ndiyo waliopewa fungu linalohusika na sheria na masuala ya vijana, linalohusika na sera pamoja na masuala ya 10%; Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini naomba nitoe ushauri mahususi, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango hili jambo wakalitafakari na wataalam wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hatujaweza kutatua changamoto ya kuwawezesha vijana kiuchumi kwa sababu tumeweka masuala ya sera kwenye sehemu moja. Naomba kila Wizara iwe na *department,* iwe na viongozi kama ni Mkurugenzi kwenye hiyo *department* inayohusika na masuala ya vijana kila Wizara, tuone namna gani Wizara ieleze kila mwaka wa fedha imetoa ajira kiasi gani kwa vijana, imetoa miradi gani kwa vijana ambao wamewekeza kwenye masuala ya uwekezaji, tuone kuna *project* gani ambazo vijana wameshinda hizo *tender* wana-*supply* kwenye Serikali na nini. Tuone na kila Wizara ieleze; watu wa utalii watuambie vijana wamepata ajira kiasi gani, miradi ya maendeleo tuone kwa *figure* tumepata ajira kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara zote ziwe na *department* maalum ambayo ina-*deal* na vijana kila moja ili sasa wale Wakurugenzi kutoka Wizara zote wawe wanaripoti sehemu moja hata kama wanaripoti Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini tuwe tuna uwezo wa ku-*trace* ni kwa kiasi gani vijana wamesaidiwa katika uwezeshwaji wa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, katika Taarifa ya Kamati ukurasa wa 50, Kamati imeeleza changamoto kwamba idara,

Wizara kutoshirikiana kupanga na kutekeleza miradi; kwangu hii kitu siyo sawa. Mheshimiwa Waziri wa Mipango hili jambo ni lako. Wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengine hapa pia na mimi naomba nilisemee.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ambazo zinahusiana; Wizara ya Maji, Kilimo, Uvuvi, Ufugaji…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat kuna taarifa kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mchangiaji Mheshimiwa Mbunge, lakini pia katika mchango wake kwa kumwongezea ubora wa hoja yake anayoijenga tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa agizo la kila mwaka wa fedha Bajeti ya Serikali inapotolewa, kila Wizara lazima ifanye *justification* ya ajira ngapi ambazo itazitoa za moja kwa moja na ajira ambazo siyo za moja kwa moja katika mwaka wa fedha na kuna fomu maalum fomu namba 15A na 15B ambazo huzijaza kila Wizara kuweza kuangalia *commitment* yake kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mchango wake ni mzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea japo alitakiwa ailete *before* hapa kwa sababu tunazungumza hatujui. Hata Mheshimiwa Mbunge wa vijana pia kutoka Chama Cha

Mapinduzi juzi alizungumza hapa, kwa sababu mimi kwangu 10% ni *peanut* yaani tukianza tukae tuzungumze 10% turudishe zile pesa tulizoibiwa hiyo ni *peanut,* tunataka *the big fish* kwa sababu sisi tuko ni asilimia kubwa ya *labor force survey* ya Tanzania. Sisi vijana ni asilimia kubwa, kwa hiyo tunahitaji hiyo *portion* yetu ambayo ni ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Kidunda. Mradi wa Kidunda ni mradi mkubwa na mradi wa kielelezo na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwenye hili kwa sababu ule mradi ni tangu mwaka 1975 sijui upo, umekuja kutekelezwa katika kipindi chake. Kwa hiyo niwaombe pia wasaidizi wake kwenye upande huu; huu mradi utekelezwe, fedha zimeshatengwa na miradi mingine kama hii itekelezwe kwa sababu huu ni mradi wa kielelezo. Huu mradi una *component* nyingi za uzalishaji; kuna mabwawa ya ufugaji, kuna mabwawa ya kulisha mifugo kwenye mradi huu mmoja. Kuna mradi wa kuzalisha umeme hapa hapa, kuna kilimo cha umwagiliaji hapa hapa na kuna bado maji ya kutumia, kuna *tank* la ujazo wa mita milioni 190. Kwa hiyo ni *project* ambayo ni kubwa na tunapongeza sana kwa hili na naomba tuwe na *project* nyingi za *design* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira hebu wazungumze haya mambo yanatekelezeka. Bajeti yetu tukitapanya *efforts* tunashindwa, wakati Serikali ni moja. Wazungumze wamalize tupange fungu moja kuchimba mabwawa yawe na tija, tuchimbe visima vya maana viwe vina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. Nilimtaja Mheshimiwa Zacharia Issaay; Mheshimiwa Priscus Tarimo,

Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mheshimiwa Japhet Hasunga wajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema aliyetupa nafasi hii leo. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa kweli; hatuzungumzi kwa lugha ya ushabiki. Serikali imefanya kazi kubwa sana na tumepitia Mpango huu umegusa mambo mengi. Mchango wangu utajikita kwenye kusisitiza baadhi ya mambo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tuna changamoto kubwa nchini ya wagonjwa wa figo. Nadhani ni wakati pekee sasa Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuangalia namna ya matibabu ya kusafisha figo nchini. Huduma za *dialysis* katika hospitali wanazopata wagonjwa wa figo zimekuwa na gharama kubwa sana. Kwa mfano, kwa wiki tu mgonjwa anatakiwa awe na Sh.900,000 lakini kwa mwaka mzima anaweza kwa fedha hizo za wiki mara wiki nne ya mwezi mara majuma 52; huyu mgonjwa anatakiwa awe na fedha isiyopungua kwenye eneo hilo tu shilingi milioni karibu ya 200, 180 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni gharama kubwa sana kwa huduma ya mwananchi na kwa kipato cha Kitanzania. Hivyo basi tuone hata hospitali za mikoa na kanda tuweze kuwapata wataalam lakini pia kununua vifaa kwa ajili ya huduma hii muhimu sana na kwa sababu hiyo wagonjwa hao wako katika hali mbaya kwa nchi nzima. Mara nyingi wanapopokea huduma hizi, hali yao inazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia eneo lingine, tunaipongeza sana Serikali, Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha, tunawashukuru mmeleta huu Mpango kama mwanzo wa kuendeleza Mpango ambao mwakani katika Mpango wa Bajeti tutaingia nao katika Mipango yetu ya Maendeleo. Mpango huu

tumepanua miundombinu mingi katika Sekta za Afya, Elimu, Maji na huduma zingine kama vyuo vya *VETA* pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni moja kwa moja linahitaji ajira mpya kwa vyovyote kwa sababu kadri tunavyojenga shule mpya za sekondari, tunavyojenga shule mpya za msingi, shule shikizi lakini pia tunavyojenga vyuo vya *VETA* na vituo vya afya pamoja na sekta zingine katika upanuzi wa kuleta huduma bora kwa wananchi. Kuna haja kubwa sasa ya Serikali katika Mpango unaokuja uangalie namna ya kuongeza idadi ya ajira ili maeneo haya yapate wataalam kwa sababu katika halmashauri nyingi tulishakuwa na nafasi wazi nyingi na sasa tulipoweka hatua ya upanuzi wa miundombinu tayari tumezalisha mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuwa uwezo wa Serikali hauwezi kutekeleza kwa mara moja, lakini lazima tuangalie kadiri tunavyopanua utoaji wa huduma, lazima tuwe na utaratibu mwingine wakati ule sasa tunapoenda kwenye mwaka wa bajeti wa kila mwaka mmoja mmoja katika miaka mitano ili kuweza kupata eneo hili na kuweza kutoa huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri wamejitahidi na Serikali imejitahidi, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hata kwenye Jimbo langu la Mbulu Mjini kuna mambo yalifanyika yalikuwa hayapo kwenye Ilani, yakaenda kutekelezwa na haijapata kutokea sura kama hiyo ya miradi mikubwa ambayo inakuja kutokea, lakini tulikuwa tunasita hata wakati wa kuomba kura namna ambavyo hiyo miradi itatekelezwa na sasa imetekelezwa. Tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili kwa vyovyote taka tusitake kuna miradi mikubwa. Kwa mfano, Jimbo la Mbulu Mji na Wilaya ya Mbulu tuna hiyo Barabara kubwa inayotoka Karatu – Mbulu hatimaye Hydom na kule Sibiti. Barabara hii tumesaini mkataba lakini eneo la Mbule kwenda Garbabi la kilometa 25 kwa sasa linasuasua sana kwa sababu utekelezaji wake umekuwa na wakati mgumu kutokana na mkandarasi kutokutekeleza kwa wakati. Mengine ni ya

mkandarasi, mengine ni yetu sisi kumwezesha fedha ili yeye pia akipata pesa aweze kutekeleza huu mradi kwa wakati na athari kubwa tunayopata katika eneo hilo ni kwamba kadri tunavyokaa na kadri ambavyo mkandarasi anatekeleza huo mradi na mradi unasuasua unakuwa zaidi ya muda wa utekelezaji, mwisho wa siku tunakuja kuingia kwenye gharama za ucheleweshwaji na gharama za mkandarasi ambazo ataleta baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaiomba Serikali iangalie hii miradi ambayo inagusa maeneo mengi na ni miradi mikubwa, tunapotenga fedha basi kwa mwaka kama huu sasa, Barabara ile ya Karatu kuja Mbulu hadi Hydom – Sibiti itengewe fedha za kutosha ili wakandarasi wale waweze kutekeleza huu mradi na kwa sababu wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa sana. Barabara hii ni kiungo muhimu sana kwa Wilaya ya Mbulu na Wilaya za jirani pamoja na majimbo yote saba yaliyokuwa yanaguswa na barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunakumbuka kuwa wakati ule wa bajeti iliyopita kulikuwa na mipango mingi. Katika Bunge hili nilizungumza nilisema kwa kweli bajeti imegusa maeneo mengi. Katika Jimbo langu nawapongeza Mawaziri wote wa Kilimo, wa Fedha, wa kila sekta, nikitazama kwa kila sekta, kila Waziri alijitahidi, lakini changamoto zinazotokea sasa ni baada ya ile miradi kuanzishwa, kwa mfano, mradi huu wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mbulu Mjini mwaka huu wakati ule wa bajeti nilikuwa navutana na Waziri Ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba. Vijiji vyote tayari tumesimika nguzo, vijiji vingi vimesimikwa nguzo lakini nyaya hazijaunganishwa na umeme haujashushwa kwa wananchi yapata zaidi ya miezi sita. Hii ni dhahiri wazi kwamba hata zile nguzo zinaharibika kule ardhini zilipowekwa kwa maana ya kusimikwa lakini pia wananchi wana hamu kubwa ya kupata huduma hii ya umeme na hii inachangiwa na pengine wakandarasi wale au wazabuni wale wanaotekeleza huu mradi wa *REA,* fedha wanazopewa pengine ni kidogo ama usimamizi wake ni duni pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba angalau yale maeneo yote kwa sababu kama tunasimika nguzo kwenye kijiji zaidi ya miezi sita wananchi wanasubiri umeme na mkandarasi anatoweka ama anashindwa kutekeleza ule mradi harudi tena *site,* wananchi wanategemea angalau hiyo huduma ipatikane. Kwa hiyo miradi kama hiyo iwekwe kwenye mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri wazi kwamba kila jimbo nchini tuna viporo vingi vya miradi. Kuna nyumba za Walimu, madarasa, zahanati, vituo vya afya ambavyo vimeanzishwa na wananchi kwa nguvu zao wenyewe. Ushauri wangu katika eneo hili ni kwamba walau basi sisi kama Serikali au Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha kupitia halmashauri zetu na maeneo mbalimbali katika mamlaka zile, wachukue ile miradi viporo ambayo ilianzishwa lakini ina zaidi ya miaka mitatu, minne haijakamilishwa kwa sababu kuna nguvu za wananchi ziliwekezwa huko, basi kuna kila sababu ya hiyo miradi kuingizwa kwenye Mpango huu wa mwaka huu ili iweze kutoa huduma kwa sababu tayari wananchi walishawekeza ama wadau wengine. Saa hizi kwa kuwa haitoi huduma athari yake ni kwamba kwanza inapungua thamani lakini la pili; huduma tuliyotarajia tunashindwa kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashauri kama itawezekana jambo hili la viporo, miradi viporo nchini tungeweza kuingiza kuliko kuanzisha miradi mipya ambayo ile ya viporo haitoi huduma na walengwa wanaotegemea kutumia miradi hiyo wanaangalia tu ikiwa haitoi huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hili la kuanzishwa kwa maeneo ya utawala. Tumeanzisha maeneo ya utawala kwa mfano Jimbo la Mbulu Mjini tuligawa maeneo ya utawala kwenye vijiji na kata lakini eneo la mitaa na vijiji hatukuajiri watendaji toka 2009 kwa zaidi ya 50%. Kwa hiyo kila tukiomba ajira wanatolewa pengine 10 kati ya 30, tano kati ya 20, matokeo yake yanazidi kuwa mabaya zaidi. Kwa hiyo katika Mpango huu ambao tunaenda, tuangalie viashiria vya mambo ambayo kwa vyovyote vitatusaidia huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Michezo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Muharami Mkenge na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka wajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa na nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja iliyoko mezani. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili ambao wanadumisha uhusiano kati ya Mkoa wa Singida na Kilimanjaro maana wote hao ni wakwe zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwa haraka haraka katika maeneo ambayo nimeona ni ya muhimu nitoe ushauri. Nianze kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Profesa Kitila hasa pale kwenye malengo ya Mpango huu kwenye ukurasa wa 20 nianze na lile lengo namba mbili. Lengo namba mbili kwenye kujitosheleza kwa chakula nadhani ni jambo ambalo nilishawahi kulitolea ushauri mara kadhaa hasa nikichangia katika Wizara ya Kilimo na kwa sababu Mheshimiwa Bashe yuko hapa na anafanya vizuri sana katika kulisukuma hilo, naomba nitoe mawazo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa chakula yapo mazao ambayo tuna-*import* bado. Tujikite hapo suala la sukari tuna-*import* sukari, suala la ngano hasa ya viwandani, suala la mafuta ya kupikia na suala la mbolea, wamegusia wengi na Mheshimiwa Bashe wakati kipindi kile cha Bunge lililopita sikuwa Mbunge, nadhani alikuwa amekaa kiti hiki hiki

alielezea kutokusomana kwa mifumo ya Wizara. Bajeti iliyopita tuliongeza nguvu katika uzalishaji wa ufuta pamoja na *sunflower* lakini wakati huo huo tukatoa *zero tax* kwa watu wanaoleta mafuta ghafi ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hapo ni kama tunaongea vitu ambavyo haviendani. Kwa hiyo kama tunaenda kupunguza haya ni lazima i-*reflect* kwenye bajeti kwamba maeneo haya sasa mafuta ghafi kwa mfano yasiwekewe tena *zero tax,* tuweke *tax* tu-*limit* huku ili viwanda hivi au mazao haya ya kwetu yaweze kupata soko. Vinginevyo wafanyabiashara wao wanatafuta faida ya haraka, kwamba wewe ukimwambia alete *crude oil* kwa ajili ya mafuta ya chakula, halafu wakati huku umezalisha alizeti analeta mafuta ambayo tayari ni *refined.* Yeye anafaya *packing* tu, kwa nini aanze kuchukua mafuta huko shambani sijui ufuta akamue? Kwa hiyo suala hilo naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lengo namba sita pia la Mpango wa Mheshimiwa Profesa Kitila kwenye ukurasa wa 20, wamesema kupanua na kuimarisha nyanja za usafiri, miundombinu ya usafiri. Sasa hapa nilipenda sana nione kwamba kwa mfano mwendokasi tumefanya nini? Mwendokasi Mheshimiwa Musukuma alisema hapa tatizo la urasimu wa Serikali. Serikali kwenda kununua *bolt* moja ambayo imeng'oka kwenye basi ni mchakato mrefu sana, lazima tubadilishe uendeshaji wa mwendokasi ili tuweze kuona tija yake. Tumpe mtu binafsi au tumpe kwa *share* au kwa makubaliano maalum lakini vinginevyo tutaendelea kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeshakubali bandari sasa inaenda kuwa inazalisha sana, inaongeza *volume;* sijaona kwenye huu Mpango *TAZARA*. Nimesoma tu kwenye vyombo vya habari kwamba *TAZARA* amepewa Mchina andeshe. Kama kweli ni Mchina tuone *efficiency* yake itakuwaje kwamba reli yetu sasa ifanye kazi. Hii bandari inaenda ku-*complement* vipi *SGR,* mizigo i-*move in bulk,* inaenda ku-*complement* vipi maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Profesa Kitila, pale Moshi tumepewa shilingi bilioni 12 kurekebisha *airport,* lakini sasa katika ile *airport* tuna watu walivamia pale nyumba kama sita; upande mmoja kuna nyumba 50 nimeona pale tutaharibu mpaka siasa, upande wa pili kuna nyumba sita ambazo zinahitaji ziwe *compensated* ili ile *runway* iwe na urefu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda anayetekeleza mradi ni *TANROADS*. Unaongea na *TANROADS* anakwambia ongea na *TAA,* unaongea na *TAA* anakwambia ongea na Wizara. Ni lazima kuwe na watu ambao wanaweza wakazi-*coordinate* na kufanya maamuzi ya pamoja ili tulete tija. Mradi ule ukishakwisha kuja kutoa hiyo *compensation* itakuwa ni ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye gesi. Hii gesi asilia katika uendeshaji wa magari, *the numbers are there,* yaani kilo moja ya gesi shilingi 1,550 na inaendesha gari umbali gani. Hii yenyewe inaweza kutusaidia kupunguza kero ya mafuta. Mafuta tunanunua kwa bei ghali, mafuta hayapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali kwanini isiamue Miji mikubwa Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Mbeya kuwe na vituo hivyo vya gesi vya kutosha na magari yawe yanabadilishwa. Sikubaliani kabisa na wazo la Mheshimiwa Mwigulu la kusema hawa watu wa Serikali wakopeshwe magari. Wakikopeshwa hawatayatumia, watayatunza kwa sababu anajua naenda ku-*retire* nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia rahisi kama Dangote aliweza kuweka magari yake yote yale makubwa mfumo wa gesi, hivi Serikali ikiamua kuweka mfumo wa gesi kwenye magari yake yote ita-*cost* kiasi gani? *Efficiency* pale tutaokoa hela nyingi sana, lakini hebu angalia wapo watu kama *Bhanji Transport* wana *fleet* kubwa wanawezaje ku-*manage?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameweza ku-*centralized* matengenezo lakini pia *movement* ya gari inajulikana, kwa sababu

tunaweza tuka-*out source* tukawa tunatuna *service center* ya kuangalia magari ya Serikali yanakwenda wapi, muda gani, yanafanya nini? Badala ya kuwasubiri *TEMESA* pia tuna-*out source* matengenezo. *TEMESA* hajui kutengeneza, hana *man power* na hana uwezo. *TEMESA* ni *specialist* wa kuharibu magari badala ya kutengeneza, kwa hiyo gharama inaonekana kubwa kwa sababu tunaenda kwenye muda ambao ni mrefu ambao unapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongelea wakati naongelea taarifa ya *CAG,* ni kweli lengo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Kitila anataka asilimia 30 ya wananchi ikifika 2025 vijijini wawe na Bima ya Taifa ya Afya – *NHIF, very well* sina shida na hilo, lakini tumeshatibu tatizo lililoko kwenye ile Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya *CAG* ile Bima ina shilingi bilioni 210 ambazo zimekopwa na Serikali hazijarudishwa. Shilingi bilioni 129 zilikopwa kujenga Hospitali ya Benjamin Mkapa haikurudishwa, shilingi bilioni 17 ikaenda *NIDA* haikuurudishwa, shilingi bilioni 18.2 ikaenda *MOI* haikurudishwa na shilingi bilioni 45 ikaenda Mambo ya Ndani haikurudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuwa na Bima ya Afya kwa wote na hata hii kama Serikali haita-*be controlled* kwamba ikikopa irudishe hii nayo tutaenda kuua watu. Serikali itachukua hela kule, kama ilivyochukua hela kwenye mifuko ya jamii ikaja ikaleta kikokotoo, ni lazima tuwe na sheria za kuzichunga hizi hela kuhakikisha zinarudishwa kwa wakati hata kama zikikopwa, lakini tuzuie zisikopwe hasa kwenye Mifuko ya Jamii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, Wizara ya Utalii wakati inatuletea semina kipindi cha Bunge lililopita, walielezea kwamba utalii wetu bado umejikita kwenye *natural resources* hatujakwenda kwenye *man made*. Nashinda kuelewa, kuna utalii wa mikutano, *AICC* wana-*concentrate* kujenga ukumbi mkubwa palepale Arusha na wakati tayari wanao, lakini Moshi kuna jengo la *NSSF* halifanyi kazi, kwa nini wasiwekeze ukumbi mwingine pale? Watu wakija kwenye utalii, *conference tourism* wakimaliza wataenda huko

mbugani. Tujenge kituo kikubwa cha utalii Zanzibar watu wakija kwenye mkutano pale wataenda kutalii. Kanda ya Kusini tuwe na ukumbi mkubwa wa mikutano. Mwanza pia karibu na Serengeti tunakuwa na kumbi, hiyo ni sehemu moja, *conference tourism* tuachane na hawa wanyama tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili kuna *medical tourism,* Mheshimiwa Rais anataka kujenga *Apollo* hapa Tanzania, ni namna gani tuna-*attract* hawa watu wa pembeni waje watibiwe hapa, *medical tourism*. Akishapona anaenda Zanzibar kutuliza akili, anakwenda Serengeti au anakwenda Selous na kwingine. Pia kuna *sports tourism,* kulikuwa na shindano moja lilikuwa liwe *financed* na Serikali la *golf*. Pale Maji ya Chai kuna *golf course* ya kisasa kabisa, *Kili Golf*. Tunaita hawa watu wa *PGA* tunagharamia wanacheza *golf* pale, upande huu wanaona Mlima Kilimajaro na upande huu wanaona Mlima Meru, wakimaliza wataenda huko, *sports tourism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda leo zile *sports facilities* ndiyo zinasababisha michezo ya Kimataifa inafanyika pale. Wale watu wakishakuja kwenye michezo lazima hela iwe inazunguka. Watu wa utalii wasijikite tu na mbuga na kuhifadhi, tuangalie hilo suala la *medical,* tuangalie suala la *conference* na suala la *sports tourism*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Tarimo. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na mchangiaji anayefuata naomba niwakumbushe kuna tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa *TWPG,* Mheshimiwa Shally Raymond, anawakumbusha Wabunge wote wanaume na wanawake pamoja na wafanyakazi wote wa Bunge kuhudhuria mchapalo maalum ulioandaliwa kwa ajili ya kumpongeza Dkt. Tulia Akson kwa kupata nafasi adhimu ya Urais wa *IPU*. Kwa hiyo, mnaombwa wote muwepo na msikose kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na baadae Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nawapongeza Mawaziri wote wawili ambao wamehusika katika kutuletea Mapendekezo ya Mpango huu wa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba taasisi zote za Kimataifa na zile ambazo zinaheshimika duniani zinaonesha kabisa kwamba uchumi wa Tanzania unaendelea kuimarika. Sababu zinazotolewa ni kwamba kumekuwa na mageuzi makubwa katika uchumi wetu, mageuzi hayo yanaimarisha uchumi lakini yanafanya tuwe *competitive* na vilevile yanatufanya tuwe shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote linaloelezewa ni kwamba Serikali yetu imeendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kwa hiyo, sekta binafsi imepewa nafasi yake kwa kiasi kikubwa sana, lakini la tatu ni imani kubwa ambayo wawekezaji, taasisi za Kimataifa, taasisi za fedha na wadau au wabia mbalimbali wameonesha kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutupeleka vizuri na dunia kutufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na mapendekezo ya mpango kwa sababu yanaongelea kuchochea ukuaji wa uchumi, kuleta uchumi shirikishi na kupunguza umaskini hasa maeneo ya vijijini, vilevile, kuzalisha kwa wingi ajira na kuchochea mauzo ya bidhaa kwa kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo yake ni hayo hayo na napenda niongelee maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo la sekta ya madini kwa kifupi, vilevile niongelee eneo jingine la muhimu sana la sekta ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini ukiangalia katika mpango inaonesha wazi kabisa ni sekta ambayo imeendelea kuwa bora na kwenye tathmini ya 2021/2023 inaonesha ni sekta ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu asilimia 56 ya mazao yanayokwenda nje au mapato yanayotoka nje ya fedha za kigeni yametoka kwenye sekta hii. Tunaipongeza sana Serikali kwa hilo. Naamini kabisa sisi tuna tabia hasa Watanzania, tuna tabia ya kuridhika sana na matokeo ya haraka. Sasa ninauhakika kwamba sekta hii inaweza ikachangia zaidi na zaidi kwenye uchumi wa nchi hii kama tukijipanga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiridhike na tunachokipata tuangalie kwamba mpango huu kwa ku-*relay* kwenye sekta hii bado una *weaknesses* nyingi ambazo ni lazima tuanze ku-*address* sasa. Moja ya matatizo makubwa ambayo nayaona ambayo lazima tuya-*address* ili mipango ya mbele iweze kukaa vizuri. Hatuwezi kuwa na sekta ambayo inategemea zaidi zao moja la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa kiasi kikubwa tunategemea dhahabu. Siku dhahabu ikiponyoka hali yetu ya uchumi itakuwa siyo nzuri. Kwa hiyo, mimi napendekeza, napenda kuona mpango unaokuja ambao kwa kweli uta-*focus* kuona kwamba tunarudi kwenye *fundamental* ya kuleta sekta ya madini ambao ni kuwa na utafiti wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unataka fedha nyingi. Tumemsikia Waziri na Mheshimiwa Rais siku za karibuni akiongea kwamba sasa tunakwenda kufanya kitu kinaitwa *high resolution physical airborne survey,* siyo jambo baya. Tuelewe kwamba *airborne survey* haitatusaidia sana kufika kule ambako tunataka kwa *speed* tunayoitaka, kwa sababu yenyewe inakupa picha za kipi kipo wapi na ni kitu gani. Haikuoneshi kinaupana gani, kiko chini kiasi gani, kina ukubwa gani kina mtawanyiko gani, kina mlandaro wa aina gani, maana yake ni kwamba bado hata ukifanya *physical airborne survey high resolution* unatakiwa bado uende ukafanye

utafiti, *exploration*. Uende *site* ufanye *drilling* uteremke chini, upeleke mitambo ili waweze kujua mashapo tuliyonayo ni ya kiasi gani, yako wapi na utaya-*mine* kwa njia gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana tujitahidi ku-*focus* kwenye suala la utafiti na utafiti siyo kwamba hakuna watu wanaweza kufanya utafiti. Utafiti unataka uwekezaji wa hali ya juu na ni *high risk*. Kwa hiyo, wawekezaji wanaoweza kutoa fedha ya utafiti siyo wengi na benki siyo nyingi. Mara nyingi inafanyika na wanahisa ambao wanachanga fedha zao wako tayari ku- *risk* kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi nini kinatuzuia tusiende kwenye utafiti, nini kinatuzuia tusipate watu wa kutusaidia kufanya utafiti wa kina ambao ni muhimu kwa ajili ya *sustainability* ya hii sekta? Sekta hii inafanya vizuri kwa sababu kuna migodi, kwa sababu kuna uzalishaji lakini kuna watu walifanya utafiti siku nyingi sana. Miaka 10, 20 na 30 iliyopita ndiyo maana leo tunapata matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri tukatambua kwamba ni vizuri tuanze kuwekeza kupata watu watakaofanya utafiti. Kinachotuzuia ni kwamba bado sheria zetu na taratibu zetu hazisaidii au hazivutii watu wa kufanya utafiti wa uhakika. Tunashukuru kwamba na katika hilo ni kwamba bado mtaji unaokuja kwa ajili ya utafiti unatozwa kodi, jambo hili duniani halipo, lipo Tanzania peke yake! Kwa hiyo, uchumi shindanishi ambao tunagombea mitaji ni lazima tuangalie hili jambo ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, bado uchumi wetu unatakiwa uende kwenye madini mengine na nimeona Mheshimiwa Waziri katika mpango wake analiongelea hilo, anasema tunakwenda kwenye madini sasa yale ambayo tunasema *critical minerals*. Madini haya ni muhimu ni madini ya karne ya sasa, ni madini yanayotaka masuala ya kuzuia na ku-*protect* mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutambue kwamba tumesaini mikataba ya kutosha siku za karibuni katika mtazamo mpya wa *mining industry*. Bado wawekezaji wana-*struggle* kutafuta na kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza hiyo migodi. Kwa hiyo, tutengeneze mazingira ambayo kwa hakika watakwenda kuanza kuchimba haya madini ya aina nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivyo maana yake ni kwamba tutaendelea kuwa na mikataba ambayo uchimbaji wake haufanyiki. Napenda kusema tatizo linarudi kule kule, kumekuwa na *dialogue* kubwa zikiendelea kwenye sekta ya madini kuona ni namna gani tunaweza ku-*improve* vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya kazi kubwa nzuri mwaka 2019 tukaja na sheria nzuri ya madini lakini nimesema na nitaendelea kusema na nitarudia kusema kwa sababu kama mtu ninaefahamu sekta naamini miaka saba baada ya kupitisha sheria ni wakati wa kutathmini. Bado tunapoteza wawekezaji wazuri wengi ambao wangeweza kuja lakini masharti ambayo bado yapo katika sheria zetu mengine yanawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri tukayaangalia hayo kwa makini. Tumesikia kuna kitu kinaitwa *vision 2030* ya sekta ya madini. *Vision* yoyote ina-*involve stakeholders* wengi. Sasa sifahamu kwa kiasi gani *vision* hiyo ni mkakati mzuri kutusaidia kwenda mbele. Napenda kusema tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba sekta hii ina-*sustain* inaenda mbele lakini tunahakikisha tunafanya yale masharti ya muhimu kuhakikisha yanakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu, napenda kusema nimefurahishwa kuona kwamba tutaendelea kuimarisha miundombinu ya anga na usafiri, na katika mpango wa sasa inaonekana kwamba tulipanga mpango wa miaka mitano ilikuwa tununue ndege 19, tumenunua ndege 17 mpaka muda huu. Naipongeza sana Serikali lakini ndege ya mwisho kununuliwa ni ile Boeing 767-300 ndege ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kununua ndege ya mizigo ni pamoja na kuhakikisha tunafanya biashara ya ndege. Biashara ya ndege siyo biashara ya abiria peke yake ni hasa ya mizigo. Kwa hiyo, naomba sana miundombinu katika maeneo husika lazima itengenezwe kwa haraka. Napenda kusema ukienda Njombe tuna uzalishaji mkubwa sana wa parachichi, kwa sasa tuna viwanda saba vya parachichi. Siyo hilo tu, Mzalishaji mmoja wa parachichi peke yake anaweza akazalisha parachichi ya kujaza ile ndege kila wiki kwa sababu ni tani 160 kwa wiki anaweza akawa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege yetu inachukuwa tani 53, kwa hiyo tunaomba sana uwanja wa ndege wa Njombe najua Serikali imeahidi lakini napenda niliseme kwa sababu kwenye kupanga mipango, kupanga ni kuchagua. Tuchague kujenga viwanja maeneo ambayo ni ya kiuchumi kwanza na Njombe ni moja ya eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Muharami Mkenge na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka wajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika maeneo machache. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuletea mwelekeo wa bajeti ya mwaka ujao. Kwa kweli *document* zao zimekaa vizuri na nimezifurahia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 ina vipaumbele Sita. Hivyo vipaumbele Sita vinakuja kutafsiriwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka

Mitano na ule mpango tunautafsiri kwa mpango wa mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri mpango huu wa mwaka mmoja uwiane sawia kabisa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi lakini na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao tulishaupitisha. Vile vipaumbele lazima viwiane. Sasa kuna takwimu hapa zinanifurahisha ambazo Mheshimiwa Waziri amezitoa. Zinatupa picha kwamba kuna mambo ya kujifunza na kuna mambo ambayo inabidi tukae chini na tutafakari tuone kama tunafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika Mashariki Mheshimiwa Waziri ambazo anaeleza kwenye ukurasa Na. 7, Mwaka 2023 anasema hivi; "Nchi ya DRC uchumi ulikua kwa asilimia 8.7. Nchi ya Uganda uchumi ulikua kwa asilimia 6.4, Nchi ya *South Sudan* uchumi ulikua kwa asilimia 5.3, Nchi ya Kenya uchumi ulikua kwa asilimia 4.8, Nchi ya Tanzania uchumi ulikua kwa asilimia 4.7 na Nchi ya Burundi uchumi ulikua kwa asilimia 3.1". Takwimu hizi maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nchi yetu tuna rasilimali nyingi, ni nchi kubwa yenye utajiri mkubwa, lakini ukuaji wa uchumi bado ni mdogo ukilinganisha na rasilimali tulizonazo, hiyo inatupa somo kwamba tukae chini tuone wapi hapajakaa sawa ili uchumi wetu uweze kukua ulingane na ukubwa wa nchi yetu tuliyonayo. Kwa hiyo hapo utaona nchi yetu ni wa pili kutoka chini kabisa tunaishinda Burundi tu katika ukuaji wa uchumi. Maana yake hapo hapajakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea eneo lingine ukiangalia wastani wa mfumuko wa bei. Nchi za *SADC* mfumuko wa bei ni wastani wa asilimia 14.5, Nchi za Afrika Mashariki wastani wa mfumuko wa bei ni asilimia 11.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia huu mfumuko wa bei ukaangalia na ukuaji wa uchumi bado tuna kazi kubwa ya

uhakikisha kwamba tunachochea ukuaji wa uchumi ili wananchi waweze kuona kile ambacho tunasema uchumi unafanya vizuri. Hebu tuangalie idani ya watu inaongezeka sasa hivi kwa asilimia 3.2 kwa mwaka ukifuatana na sensa. Asilimia 65.1 wanaishi vijijini, hebu tuangalie mchango wa hawa watu katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema Pato la Taifa Mwaka 2023 lilifikia shilingi trilioni 141.9 hebu tuangalie sekta gani zilichangia kwa kiwango kikubwa kwenye hilo Pato la Taifa. Utakuta kilimo kimechangia asilimia 15.9, sasa asilimia 15.9 wakulima hao, watu ambao wanalima ni zaidi ya asilimia 70 ya wananchi lakini kwenye Pato la Taifa wamechangia asilimia 15 peke yake. Hii inaashiria kwamba kuna tatizo kwa sababu kama idadi ya watu asilimia 70 wanachangia asilimia 15 ya Pato la Taifa, maana yake kuna tatizo ambalo lazima tuliangalie vizuri kwamba hatujakaa sawa. Ujenzi ulichangia asilimia 15.5, madini yalichangia asilimia 11.9, biashara na matengenezo asilimia 9.8 na uzalishaji viwandani ulichangia asilimia 9.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi takwimu zinatupa nini, zinatufundisha nini? Kwamba mipango yetu na Wizara ya Mipango ambayo tulipendekeza ianzishwe, ambayo ndiyo *thinktank*, ndiyo moyo, kwamba sasa mkae chini mtafakari muone wapi tumekosea? Wapi hatujafanya vizuri? Mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri, ametupa mwelekeo wa Mpango wa mwaka huu mmoja, kwamba maeneo tunayoenda kufanya ni uchumi jumuishi. Kama asilimia 70 wanachangia asilimia 15, lazima tuone tutawajumuisha vipi katika uchumi huu waweze kuchangia kwa kiwango kikubwa. Amesema kuna tatizo la umaskini, amezungumzia ukosefu wa ajira ambalo ni tatizo sugu, wamezungumzia namna ya kutengeneza matajiri na namna ya kuongeza thamani ya mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri, hebu aangalie kwenye uchumi na uzalishaji. Nina maeneo matatu ambayo nafikiri ni muhimu yatazamwa vizuri sana. Eneo la kwanza ni

eneo la viwanda. Tunaposema viwanda, ambayo ndiyo sera kubwa ya ujenzi, nchi haiwezi kujitegemea. Mwalimu Nyerere alisema lazima tufike mahali tuwe ni nchi ya kujitegemea. Nchi haiwezi kujitegemea tusipoliangalia eneo la viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye viwanda hapa kuna kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, madini, viwanda mama na viwanda vya kuongeza thamani na utalii. Hivyo vyote tunaviweka kwenye eneo la viwanda. Hili eneo kwenye *allocation* ya rasilimali lazima lipate angalau asilimia 50 ya rasilimali za maendeleo ziende kwenye hili eneo la viwanda ili tuweze kuona matokeo chanya. Kinyume cha hapo, tutashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni biashara na huduma zake. Hapa kuna biashara za ndani na biashara za nje. Pia kuna huduma za biashara kama vile mabenki, bima, maghala, usafirishaji, mawasiliano, masoko na matangazo. Haya maeneo yanachochea biashara. Ni miundombinu ya kusaidia biashara zifanyike. Ni lazima tutazame vizuri tuone tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho itakuwa ni huduma za jamii ambapo tuna elimu, tutakapotengeneza rasilimali watu yenye weledi, yenye ujuzi, yenye uwezo wa kufanya kazi. Pia, kuna afya na maji. Katika maeneo haya, tukiyatazama vizuri, tukaelekeza rasilimali zetu kwenye huduma za jamii tuweke *20 percent* kwenye *allocation* ya rasilimali na kwenye biashara asilimia 30. Tukipeleka hivyo, inaweza ikatusaidia nchi yetu kutoka haraka hapa tulipo na tukaweza kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Waziri mtakaa chini myatafakari kwa undani muone namna tunavyoweza kuboresha, muone namna mipango yetu inavyoweza ku-*drive* ili tuweze kuhakikisha miundombinu inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbozi kuna maghala yamejengwa yana miaka mitano mpaka sasa hivi hayajakamilika, Mkandarasi alishakimbia. Yale maghala ya kisasa, vihenge vya

kisasa havijakamilika. Vinatakiwa vikamilike vile. Vikikamilika vitatusaidia. Ile bandari kavu pale Tunduma ni lango kubwa la *SADC*, pana biashara kubwa. Ile biashara inaweza ikaongezeka kama uwekezaji utakuwa mzuri na mpangilio utakaa vizuri, *dry port* itakaa pale, nchi zote za *SADC* zitakuwa zinachukulia mizigo pale na mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Nilimtaja Mheshimiwa Muharami Mkenge na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuindeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, katika kipindi kifupi miradi ya maendeleo mingi sana tumeipata katika majimbo yetu na maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Pili, nataka niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wao mzuri ambao wameufanya. Kwa kweli ninavyoona, sasa hivi Tanzania inaelekea mbali tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 15 mwezi wa tisa Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji alikuja kwetu Bagamoyo kwa ajili ya kuzindua *masterplan* ya kongani ya viwanda ambayo itagharimu karibu shilingi trilioni 11. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo uliifanya siku ile. Kwa kweli hii inaonesha kabisa kama hii kongani ya viwanda ambayo iko

pale maeneo ya Bagamoyo Zinga itaanza kufanya kazi, nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa sana katika maendeleo ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uzinduzi wa kongani ya viwanda, pia naishukuru Serikali na kuipongeza. Ile *project* ya kongani ya viwanda wameshaanza kuifanyia kazi kwa namna moja au nyingine. Zaidi ya shilingi bilioni sita zimewekezwa pale kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ambazo zitakuwa zina-*allocate* viwanda sehemu ambazo vitajengwa. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hii *masterplan* ya *EPZA* ya viwanda Bagamoyo, vile vile kuna jambo ambalo nataka nilizungumze kidogo katika mpango wenu Mheshimiwa Waziri. Bagamoyo pale, Serikali imechukua ardhi ya watu na mpaka sasa watu wengi sana hawajui wafanye nini kwa sababu hawawezi kuuza ile ardhi, hawawezi kufanya chochote kile. Katika ile *masterplan* ilionesha kwamba Serikali itatenga karibu shilingi bilioni 75 kwa ajili ya kufanya *compensation*. Naomba Mheshimiwa Waziri katika mpango wako wa mwaka huu 2024/2025, hebu jaribu kuiingiza hii shilingi bilioni 75 ili wananchi wale tuachane nao, tubaki na eneo letu kama Serikali tuweze kuwekeza katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi katika upande wa bandari. Katika miradi ya kielelezo Serikali imeeleza kwamba inataka kuendeleza miundombinu ya msingi katika bandari pamoja na maziwa makuu. Nimwambie Mheshimiwa Waziri, bandari ni lango la kibiashara katika nchi yetu na ni sehemu inayotuingizia pesa nyingi sana. Juzi juzi tu Serikali imeingia mkataba na *DP-World* kwa sababu ya uboreshaji wa Bandari yetu ya Dar es Salaam, lakini tuna bandari nyingi sana katika nchi yetu ambazo zinaweza zikatuingizia kipato kikubwa sana, mojawapo ni Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Bagamoyo ina mizigo mingi inayoshuka pale kutoka sehemu mbalimbali. Wenzetu wa Zanzibar biashara yao kubwa wanafanya na Bagamoyo pamoja na

huku. Kwa sababu bandari ile inatuingizia pesa, kwa hiyo, ni bora ile miundombinu ya bandari ikawekewa mkazo na msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nataka kuja katika suala la uvuvi na hasa nataka kuzungumzia taasisi ya *FETA*. Hii taasisi ni muhimu sana katika maendeleo ya uvuvi hapa Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri, katika mipango yake hii taasisi iongezewe nguvu ili iweze kusomesha watu wengi na hasa walioko kando ya pwani ya Bahari za Bagamoyo, Pangani, Tanga, Kilwa na sehemu nyinginezo ili watu wengi waweze kupata ujuzi kwa ajili ya uvuvi. Leo hii taasisi ya *FETA* kama itaingia makubaliano na Halmashauri zetu kutoa mafunzo na walimu wakawa wanakwenda kule kuwapa mafunzo vikundi mbalimbali, kwa kweli uvuvi wetu utaboreka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nataka kuzungumza kuhusu masuala ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Kwa kweli tuna changamoto kubwa sana. Nimeona hapa katika suala la mifugo imezungumziwa jinsi ya kuboresha mifugo, kuweka majosho na kadhalika lakini bado sijaona mkakati maalum wa Serikali kutenga eneo kwa ajili ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji ni ndugu zetu, ni wenzetu na kwa kweli nawaonea huruma, wanahangaika sana. Kila wanapokaa ni moto tu. Naiomba Serikali, Serikali ina maeneo mengi ya hifadhi, hebu tujaribu kufumba macho tuue japo hifadhi moja kubwa katika nchi yetu tuwagawie wafugaji waende kuishi kule wafanye kazi zao na wafuge kwa amani kuliko hivi kuhangaika hangaika, leo wako huku, kesho wako huku. Hiyo siyo sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pale kwangu Bagamoyo Mjini, utakuta kuna wafugaji kutoka sehemu mbalimbali katikati ya mji wanachunga ng'ombe zao. Kwa maana hiyo tutakuwa hatufiki kwa kweli. Ni jukumu la Serikali kupanga mpango mahususi kabisa kuwaandalia wafugaji eneo maalum. Huo mpango unatakiwa

uwekwe kwa sababu vinginevyo kila siku itakuwa ni ugomvi, migogoro kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia suala la mwisho kuhusu nishati ya kupikia. Kumekuwa na changamoto kubwa sana sasa hivi kwa nishati ya kupikia. Watu wengi wanatumia mkaa katika nchi yetu. Serikali kwa makusudi kabisa ipange mpango maalum kabisa, matumizi ya gesi yawe *compulsory,* kusiwe na kikwazo kingine tena. Kwa sababu leo hii mtu akikata mkaa, akifika getini anakamatwa, mkaa unapigwa faini. Watu wanajitafutia riziki mambo yanakuwa magumu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, tubadilishe utaratibu. Ikiwezekana, kama tunavyotoa ruzuku ya mafuta, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hebu liangalie kwa makini kabisa. Toa ruzuku ya gesi *at least* mitungi ya gesi iingie mingi ya kutosha katika nchi, watu watumie gesi badala ya kutumia kuni na mikaa. Yatasababisha migogoro kwa watu, migogoro na Serikali, misitu yetu itakufa na kuangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru. Naipongeza tena Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Muharami Mkenge, nilimtaja Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru jioni hii kuchangia mpango ulioko mbele yetu. Kwanza nawapongeza Mawaziri wawasilishaji wote wawili. Naomba niende moja kwa moja, nianze na kitabu hiki cha mipango ukurasa wa nne. Wanasema hapa, kuna mgawanyo wa vipaumbele na wametaja kama migawanyo mitano hivi. Kuna kuchochea uchumi shindanishi na shirikishi, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu, kuendeleza rasilimali watu na kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma. Huo ndiyo mgawanyo wa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee kwenye mgawanyo huu wa tatu na wa nne, kuhusu kuendeleza rasilimali watu na maendeleo ya watu. Hivi ni kweli tunayo mipango thabiti kwenye nchi ambayo tuna watu wengi tunaowaita wafugaji? Mimi sipendi kuwaita wafugaji, wachungaji. Nini mpango wa Serikali hii juu ya hawa wachungaji ambao sisi tunawaita kama wafugaji, lakini ni wachungaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja niliongea na Mbunge mmoja humu akaniambia, kama vile ilivyo kwa wachungaji, basi hata kwenye kilimo wanaotumia jembe la mkono, nao ndio kama wale. Yaani kuna wakulima wanaotumia kilimo cha kisasa na kuna wafugaji wanaofuga kisasa. Kuna wachungaji ambao wanafananishwa na wale wakulima wa majembe madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona mpango wa Serikali namna ya ku-*manage* hawa wachungaji na wafugaji. Leo ukiingia pale; nitoe mfano kwa Mkoa wa Lindi kwenye Wilaya za Liwale, Kilwa, Nachingwea na Wilaya ya Tunduru, wakulima mazao yao yasipoliwa na tembo yataliwa na ng’ombe. Wananchi wasipojeruhiwa na tembo watajeruhiwa na wachungaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, nataka nione huu mpango unakwenda kufanya nini juu ya hawa wafugaji tulionao ambao mimi nawaita kama wachungaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia kwenye miradi ya kimkakati au miradi ya kipaumbele, imetajwa pale *LNG* na miradi mingine. Mheshimiwa Waziri huu mpango ni wa pili kutoka mwisho kwenye mipango ya miaka mitano. Kwenye mpango wetu wa mwanzo mradi wa reli ya Mtwara – *Mbamba Bay* ulikuwepo. Leo kwenye mpango huu sijauona. Tunazungumzia Mchuchuma na Liganga, bila kuimarisha Bandari ya Mtwara na reli yake, hii Mchuchuma na Liganga tunakwenda kuitekeleza vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamwelewa Mheshimiwa Waziri. Nataka kuona ile reli ya *Mbamba Bay* – Mtwara imefikia wapi? Nimewahi kuuliza swali hapa kuhusu hiyo reli ya *Mbamba Bay* jibu niliambiwa hiyo reli itajengwa kwa *PPP*. Sasa huu ni mpango wa pili kutoka mwisho, ina maana tunakwenda mwisho. Sasa Mheshimiwa Waziri, nina karatasi hii hapa, huyu ni mwekezaji ameiandikia Serikali, nia ya kuwekeza kwenye hiyo reli ya Mtwara – *Mbamba Bay*. Barua hii imeandikwa tarehe 19 Septemba mwaka huu, 2023. Tarehe 10 Oktoba amejibiwa. Pamoja na kwamba wameandika kizungu, lakini mimi nilisoma zamani kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali wanasema Serikali bado haijawa tayari, tutakapokuwa tayari na wewe tutaku-*include* kwenye *PPP*. Maana yake ni kwamba Serikali mpaka leo hawajui hata gharama za ujenzi wa reli. Upembuzi yakinifu bado na mambo mengine ya kihasibu mnajua ninyi, bado. Sasa huyu mtu yuko tayari, Serikali haiko tayari. Tukiuliza Wabunge hapa, mnatuambia hiyo reli itajengwa kwa *PPP*. Lini? Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa uniambie, ni lini mradi huu unakwenda kuanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hii, nchi yetu tunajua asilimia 60 ya Watanzania ni wakulima. Kwenye mipango hii sijaona mazao ya wakulima yanalifikiaje soko? Kuna miradi ya barabara imetajwa hapa michache, lakini sijaona zile barabara za vijijini ambapo ndipo yanapotoka mazao kupelekwa sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule kwangu tunayo barabara kubwa sana. Nimeona miradi mingine ya barabara imetajwa hapa, lakini Barabara ya Nangulukulu – Liwale sijaiona na huu ndiyo mpango. Sasas nataka nijue, kama tunaendeleza rasilimali watu, tunawaendelezaje kama hatujafikia hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Awamu ya Tano tulikuwa na *slogan* kwamba tunakwenda kwenye viwanda. Mheshimiwa Waziri, keshokutwa ukija hapa kuhitimisha, naomba nipate takwimu, mpaka leo tunavyo viwanda vingapi vipya vilivyotekelezwa kwenye nchi

yetu, vinavyokuja na sera hii? Kati ya viwanda hivyo, ni viwanda gani ambavyo vitakuwa ni vya kuchakata mazao yetu ya kilimo? Kwa sababu lengo letu kubwa la kuanzisha viwanda ni kuchakata mazao yetu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu sijaona hata zao moja lililowekwa kwenye mkakati kwamba mwaka huu tunakwenda kujenga kiwanda hiki na hiki kwa ajili ya kuchakata chikichi, parachichi au korosho. Sijaona! Inawezekana mimi sijaona, lakini Mheshimiwa Waziri utakapokuja, naomba kupata maelezo, kwa sababu leo ni mwaka wa tatu mfululizo zao la korosho linashuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungekuwa kweli na mipango mizuri, madhubuti ya kuangalia zao letu la korosho linashuka, tufufue viwanda, tungekuwa tumesonga mbele, lakini mpaka leo tunapiga danadana tu, kwamba tunapanga mipango, lakini bado hatuko vizuri. Tumejenga viwanda vingi, tumeambiwa kuna viwanda vya vioo, sijui mara vingine vya *juice,* nami nataka niwaambie, viko viwanda vya *juice* nchi hii, mchuzi wanatoa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Pwani kuna mananasi yanaharibika hapo, ukienda Tanga machungwa yanaharibika hapo, ukienda kwa ndugu zangu Mkuranga pale mananasi na machungwa yanaharibika, lakini viko viwanda vinaagiza mchuzi kutoka nje; na hawaagizi bure, lazima wapate kibali. Wanapopata kibali, mnajua ndiyo hapo wanatumia fedha za kigeni kuagiza mchuzi kutengeneza *juice*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema mtakapokuja, mtuambie kama hivi viwanda vinavyochakata mazao yetu ni vingapi? Vinavyochakata mali ghafi kutoka nje ni vingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya vijijini nimezungumzia, mradi wa *Mbamba Bay* tayari nimezungumza, lakini kuna barabara hapa tumesaini tarehe 16 mwezi wa Sita, *EPC+F* bado leo ni

kitendawili. Mwezi wa 11 huu, na inawezekana ikafika Januari *EPC+F* haijaanza. Naomba tuone namna gani tunakwenda kuyatekeleza haya mambo? Haya mambo ndiyo yanagusa watu wetu, nasi humu tumekuja kwa ajili yao. Kwa hiyo, hayo ndiyo niliona niseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, inawezekana watu wasijue ng'ombe wamekujaje Lindi na Mtwara? Wakati wachungaji hawa wamehamishwa Ihefu, kabla hawajahamishwa, walikuja wataalam wa Idara ya Mifugo, Wizara ya Mifugo wakasema tunaomba Lindi kwa sababu ninyi mna eneo kubwa tulete mifugo. Sharti mojawapo la kwanza ilikuwa ni kutanguliza miundombinu kabla mifugo haijaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Liwale tulitenga maeneo. Tuna kata zetu tatu; Kata ya Kimambi, Kata ya Mlembwe na Kata ya Lilombwe, hizo tulitenga mahususi kwa ajili ya kukaa wafugaji. Leo hizo Kata zote ninazozisema hakuna miundombinu. Kimambi juzi tumejengewa josho ambalo hata wachungaji wenyewe hawaiti lambo, wanaita karo. Wale wafugaji tuliowajengea lile lambo, wanasema ni karo, lakini fedha za Serikali zimekwenda pale, hakuna anayefuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kweli tunataka kudhibiti, tunataka miundombinu na elimu kwa wafugaji. Nami nataka nikwambie kwamba hakuna mgogoro wa wafugaji na wakulima.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi, muda wako umemalizika.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho siku ya Alhamisi, tarehe 9 Novemba, 2023 utafanyika uzinduzi rasmi wa *Bunge Marathon* katika ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge.

Uzinduzi huu utashirikisha Wabunge na wadau kutoka taasisi mbalimbali nchini ambazo zinatarajiwa kudhamini *Marathon* hii. Mgeni rasmi katika uzinduzi huu atakuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria uzinduzi huu muhimu ili kufanikisha *Marathon* hii ya kwanza katika historia ya Bunge. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Bunge linarejea.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zetu za leo zimekamilika na hakuna la ziada, kwa hiyo, nawatakia jioni njema. Tukutane kwenye mchapalo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*